

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Arobaini - Tarehe 6 Agosti, 2003

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza, kwenye *Order Paper* ya leo kuna uchaguzi wa Wajumbe wa kwenda kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Saalam. Napenda tu kutangaza waliogombea, ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. Kuna wagombea watano, lakini nafasi ziko tatu. Uchaguzi utafanyika baada ya kipindi cha maswali.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga kwa mwaka 2001/2002 (*The Annual Report and Accounts of The Tanzania Civil Aviation Authority (TCCA) for the year 2001/2002*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 389

Barabara ya Omagakorongo - Murongo

MHE. ELIZABETH N. BATENGA aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Omagakorongo - Murongo - Kituntu - Mabira - Bugara - Businde - Murongo ni mbovu sana; je, Serikali ina mpango wa kutengeneza barabara hiyo ili iweze kupitika kwa nyakati zote?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA
aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Omagakorongo hadi Murongo iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe na ina urefu wa kilometra 80.5. Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali iliidhinisha barabara hiyo ifanyiwe matengenezo ya kawaida ya kilometra 40 na matengenezo ya sehemu

korofi kilometra 26. Jumla ya shilingi 14,660,000/= zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na jumla ya shilingi 21,015,800/= kwa ajili ya sehemu korofi. Matengenezo ya sehemu korofi yamefanyika kulingana na ratiba ya utekelezaji. Aidha, matengenezo ya kawaida katika barabara hiyo hayakuweza kufanyika kwa sababu fedha iliyokuwa imetengwa ilikuwa haijatolewa mpaka kufikia mwezi Mei, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 barabara hiyo imewekwa katika ratiba ya utekelezaji ili ifanyiwe matengenezo na iweze kuitika wakati wote. Hivyo, Serikali itaendelea kufanya matengenezo ya barabara hii kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu ili kuwaondolea wananchi kero.

Aidha, mwezi Juni, 2003 mgao wa fedha za barabara kwa Halmashauri ya Karagwe imetolewa kwa asilimia 94 ambapo kiasi cha shilingi 137,600,000/= kimepokelewa. Hivyo, ni mategemo yangu kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe sasa itatoa fedha zilizotengwa ili barabara hiyo iweze kufanyiwa matengenezo ya kawaida.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Lakini namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa barabara hii inakwenda kwenye mpaka wa nchi yetu na Uganda; na kwa kuzingatia matatizo ya mipakani na historia ya Mkoa wa Kagera. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba hiyo ni sababu kubwa na ya kutosheleza barabara hii ikawa barabara ya Mkoa?

La pili, kwa sababu hizo hizo nilizozitaja kama barabara hiyo haiwezi ikawa barabara ya Mkoa Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba Wilaya hii inapaswa kutengewa fedha nyangi ili kusudi barabara hii iweze kutengenezwa kikamilifu na ipitike wakati wote kwa kuzingatia matatizo niliyoyataja?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii inapita karibu sana na mpaka kati yetu na Uganda. Lakini siwezi nikamjibu swalı lake vizuri, kwa sababu suala la barabara kupandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa ni zoezi ambalo bado halijafanyika mpaka sasa na linasimamiwa na Wizara Ujenzi. Lakini maadam Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alishalieleza jambo hili, nafikiri tuvute subira baada ya sheria inayohusika kurekebishwa zoezi hilo litafanyika.

La pili, ni kweli kabisa kwamba tunatenga fedha katika Halmashauri zetu kwa kuzingatia vigezo vingi likiwemo suala la ulinzi na usalama na tungetamani sana kwa barabara hizi hasa za mipakani kuzipa uwezo zaidi ili ziweze kuhudumiwa muda wote. Lakini kama ambavyo mara nyangi tumekuwa tunasema kikwazo kikubwa ni uwezo mdogo wa fedha ambazo zinapatikana na kutoptana na hicho kidogo ndiyo maana mnaona tunatenga fedha chache kidogo.

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba maadam barabara hiyo iko chini ya Halmashauri ya Karagwe, basi waendelee kutoa kipaumbele kwa barabara hii na kuweza kuiombea fedha ambazo wanadhani zinaweza zikatosheleza mahitaji yake na kila wakati tutajitahidi kuzingatia hilo ombi.

Na. 390

Kuanzisha Halmashauri Mpya ya Wilaya ya Kilindi

MHE. JUMA S. KIDUNDA aliuliza: -

Kwa kuwa Wilaya ya Kilindi ni mionganini mwa Wilaya mpya zilizoundwa na kutangazwa na Serikali mwaka 2002; na kwa kuwa Halmashauri ya sasa ya Handeni kama ilivyo kwa Halmashauri zote zenye Wilaya mpya inatakiwa kuandaa na kutekeleza mikakati ya Halmashauri mpya:-

(a) Je, ni taratibu gani zimeandaliwa na Halmashauri ya sasa (kabla ya kugawanywa) za kukusanya fedha na raslimali nyagine ili kufanikisha ujenzi wa majengo na upatikanaji wa mali nyangi za Halmashauri ya Kilindi?

(b) Je, utekelezaji wa mikakati iliyowekewa na taratibu hizo umefikia kiwango gani cha ufanisi?

(c) Je, ni wataalam wangapi katika ngazi ya Wilaya na wa Idara mbalimbali pamoja na nyenzo nyingine ngapi kama vile magari vimehamishiwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya Mpya ili kwa kusaidiana na Mkuu wa Wilaya ya Kilindi katika kujenga na kuendeleza Wilaya hiyo changa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kidunda, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa Wilaya mpya zilizoundwa na kutangazwa na Serikali mwaka 2002. Aidha, nakubaliana naye kabisa kwamba Halmashauri ya sasa ya Wilaya ya Handeni inatakiwa kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuanzishwa kwa Halmashauri mpya. Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imeandaa taratibu za kukusanya fedha na raslimali nyingine ili kufanikisha ujenzi wa majengo na upatikanaji wa mali nyingine inayotarajiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kama ifuatavyo: -

(i) Kutenga fedha kwenye Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi. Kiasi cha shilingi milioni 9.3 zimetengwa kutokana na vyanzo vyake vya mapato na shilingi milioni 10 kutokana na ruzuku ya Serikali kwa mwaka 2003/2004.

(ii) Wananchi wanaendelea kuhamasishwa kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi.

(b) Mheshimiwa Spika, kiwango kilichofikiwa katika mikakati na taratibu zilizoanza kutekelezwa ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imeunda Kamati maalum ya maandalizi ya Wilaya mpya za Handeni na Kilindi kama ilivyoagizwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kamati ya Kilindi ina Wajumbe 21 ambao ni Madiwani wa eneo hilo.

(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imeunda Sekretarieti ya Maafisa wanne kushughulikia na kufuatilia uanzishaji wa Halmashauri ya Kilindi, Maafisa hao ni Afisa Mipango, Afisa Maendeleo ya Jamii, Mhasibu na Afisa Kilimo.

(iii) Wataalam wa Mipangomiji wamekwishatembelea Songe na kuainisha maeneo ya kujenga Boma, Ofisi za Taasisi mbalimbali, makazi na maeneo ya viwanda na biashara. Aidha, kwa kukitumia Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi tayari base map ya Mji wa Songe imeandaliwa.

(iv) Mwaka 2002/2003 zilitengwa jumla ya shilingi 64,000,000/= katika Bajeti ya Mkoa ambazo zimetumika kununulia magari mawili kwa ajili ya Mkuu wa Wilaya na Katibu Tawala wa Wilaya. Mwaka wa 2003/2004 zimetengwa jumla ya shilingi 100,000,000/= kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, nyumba ya Mkuu wa Wilaya na nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya.

(c) Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa watumishi wa Idara za Usalama wa Taifa, Polisi na Utawala ndio wamehamishiwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya mpya. Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Kilindi na Katibu Tawala wake wamepatiwa vyombo vya usafiri ikiwa ni pamoja na Kituo cha afya cha Songe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taratibu zote ambazo zimeshaanza kufanyika naomba nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri zote mpya zitaanzishwa rasmi mwaka 2005. Hivyo, kwa kipindi hiki hadi mwaka 2005 Halmashauri za sasa zitaendelea kusimamia shughuli za maendeleo kwa maeneo yote.

MHE. JUMA S. KIDUNDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa uendeshaji bora wa Halmashauri unategemea miundombinu na zana kama kompyuta na simu na zana zingine ambazo zinatumika ofisini. Lakini kwa kuwa mpaka sasa hivi Wilaya ya Kilindi haina umeme wala haina simu. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuhakikisha kwamba umeme na simu vinafikishwa angalau Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi pale Songe mapema iwezakanavyo? (Makofsi)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ofisi yetu inatambua matatizo mbalimbali yanayoikabili Wilaya mpya ya Kilindi na kama nilivyosema juhudhi hizo zimeanza. Hili la simu pamoja na umeme bahati nzuri wahusika wa Wizara hizo mbili wote wako hapa Bungeni na bila shaka wamesikia rai ya Mheshimiwa Mbunge. Cha kufanya ni kuendelea kufanya mawasiliano ya karibu kati yetu na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Na. 391

Umeme Wilaya ya Ngara

MHE. GWASSA A. SEBABILI aliuliza:-

Kwa kuwa tangu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alipoahidi kuipatia umeme Wilaya kongwe ya Ngara mwaka 1995 mpaka mwaka 2002 ndipo zilionekana dalili za maandalizi; na kwa kuwa tangu mwanzo ilipangwa kuwa umeme huo utawashwa Mji Mkuu wa Wilaya ya Ngara ndipo usambazwe katika Mji ya Rulenge na Kabanga na kuendelea; na kwa kuwa taarifa zinazotolewa na ofisi ya *TANESCO* Mkao wa Kagera na kitengo cha *Rural Electrification* Shirika la *TANESCO* zinasema umeme utatolewa kwa Makao Makuu ya Wilaya tu: -

(a) Je, ni kwa nini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwasha umeme Wilaya ya Ngara imekuwa ikisuasua kwa karibu miaka 8 sasa bila majibu bayana?

(b) Je, ni nini ugumu wa Serikali kuunganisha umeme wa *National Grid* kwa *line za Geita Gold Mine* na *Kahama (Bulyanhulu) Gold Mine* moja kwa moja mpaka Ngara ili kupunguza gharama ya majenereta ambayo ni kubwa na ya kutoa umeme usioaminika kama wote tunavyofahamu hivyo?

(c) Kwa kuwa Serikali inafahamu kuwa *Nickel* ya *Kabanga Nickel Company* inashindikana kuchimbwa kwa takriban miaka 40 baada ya uchunguzi kukamilika. Serikali haioni kuwa inazidi kukumbatia umaskini wake yenyewe na wa raia wake kinyume kabisa na kauli yake ya mara nyingi humu Bungeni na kwingineko kuwa inaupiga vita ujinga, maradhi na umaskini, kwa vile Kampuni hiyo haiwezi kuchimba madini hayo magumu yaliyoko kina kirefu kuzimuni kwa kutumia jenereta?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara unatarajiwu kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2003. Ujenzi wa jengo la kituo cha kuzalisha umeme upo katika hatua za mwisho. Mitambo ya kuzalisha umeme itasafirishwa kutoka Kondoa kwenda Ngara hivi karibuni. Kazi ya kupima *line za umeme* Mjini Ngara imekamilika. Baadhi ya nguzo zimeshawasili na zingine ziko njiani. Kazi ya ujenzi wa *line za usambazaji* umeme katika Mji wa Ngara itaanza mara tu baada ya kazi kama hiyo kukamilika huko Wilayani Biharamulo hivi karibuni. Kukamilika kwa kazi ya kupeleka umeme Ngara kutahitimisha ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais.

(b) Mradi wa kuunganisha umeme wa *National Grid* katika Wilaya ya Ngara kwa *line* ya kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu na *Geita Gold Mine* ni mpango wa muda mkubwa. Majadiliano kati ya *TANESCO*

na *Geita Gold Mine* yanaendelea. Gharama za kuufikisha umeme wa gridi ya Taifa katika Wilaya ya Ngara na Wilaya jirani baada ya umeme kufika Geita ni kiasi cha shilingi bilioni 37 ambazo bado hazijapatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu madini ya *Nickel*, napenda kumwarifu Mheshimiwa Gwassa Sebabili na Bunge lako Tukufu kuwa uchunguzi wa machimbo ya *Nickel* ya Kabanga bado unaendelea. Takwimu zinaonyesha kuwepo *Nickel* ya kiasi cha ratili bilioni 1.678 ambazo ni sawa sawa na tani 762,900. Aidha, Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* inaendelea na utafiti wa njia ya uchorongaji (*drilling*) na itakapokamilika uchunguzi wake inawezekana uchimbaji wa *Nickel* ya Kabanga ukaanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiukumbatii umaskini. Serikali iko mstari wa mbele katika kupiga vita umaskini kwa kuimarisha miundombinu mbalimbali ya kukuza uchumi kama ndio njia sahihi ya kupiga vita umaskini. Kuhusu *Nickel* ya Kabanga, mara Kampuni ya *Nickel* itakapokuwa tayari kuchimba madini hayo, Serikali itafikisha umeme wa uhakika hata kama ni kwa kuikaribisha Kampuni hiyo kuchangia gharama kama ilivyofanyika kwa Kampuni ya Madini ya Kahama yaani *Kahama Mining Company*. Tatizo ni kwamba, kwa kuwa Kabanga iko mpakani na nchi jirani, vita vinavyoendelea katika nchi jirani na matukio ya ujambazi yanayofanyika dhidi ya *Kabanga Nickel Company* imewafanya watafiti hawa wasitishejisitishe shughuli za utafiti wa madini na hivyo kucheleta kuanza uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Serikali ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kutafuta suluhisho la vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi hiyo jirani kwa manufaa ya majirani hao, lakini pia kwa maendeleo ya Tanzania na hivyo kupiga vita umaskini.

MHE. GWASSA A. SEBABILITY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametamka kwamba umeme utawaka mwishoni mwa mwaka 2003; na kwa kuwa tatizo lilokuwepo ilikuwa ni kupata fedha ya kufikisha umeme katika Mji wa Rulenge. Kwa kulingana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, sasa zitapatikana shilingi bilioni 4 badala ya shilingi bilioni 400 kama ilivyokuwa hapo awali. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutaja hapa Bungeni kwamba sasa umeme utafika katika Mji wa Rulenge ili wananchi wa Ngara waweze kufurahia ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahadi ambayo Serikali inaitoa Bungeni na kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi ni kwamba ifikapo mwishoni mwa mwaka 2003 umeme utawaka katika Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara. Kuhusu Rulenge tunafahamu mahitaji ya umeme ya Rulenge na tumekuwa na mawasiliano ya karibu sana na Mheshimiwa Mbunge na pia na viongozi wa Chama cha Mapinduzi akiwemo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Kagera. Lakini kwa sasa hivi tunatoa ahadi ya kufikisha umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara, na hapo baadaye fedha zitakopatikana umeme utafika Rulenge.

SPIKA: Sasa hii ni Wilaya ya Ngara. Sasa wa Wilaya nyingine mnasimama kutafuta nini?

Na. 392

Kupeleka Umeme Lupa Tingatinga

MHE. NJELU E. M. KASAKA aliuliza: -

Kwa kuwa mawasiliano kati yangu na Serikali na Kampuni ya Ugavi wa Umeme ya *TANESCO* ni kwamba *TANESCO* ilikubali kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Lupa Tingatinga ambacho hakiko mbali sana kutoka Makongorosi ambako sasa kuna umeme: -

(a) Je, mradi huo utatekelezwa lini?

(b) Je, tatizo la vifaa kama vile mita na nyaya ambalo lilikuwa linaikabili ofisi ya *TANESCO* Chunya litaisha lini?

(c) Je, ni lini ofisi ya *TANESCO* Chunya itapatiwa gari la uhakika la kutoa huduma nzuri kwa eneo kubwa wanalohudumia?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenyehemmu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Lupa Tingatinga maarufu unahusu ujenzi wa njia kubwa ya umeme wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 40 kutoka Makongorosi ambako kuna umeme, ufungaji wa transfoma na ujenzi wa njia ndogo za umeme pia inakadiriwa kuwa utekelezaji wa mradi huu utahitaji jumla ya shilingi milioni 568.

Mheshimiwa Spika, ni vigumu Serikali kuahidi ni lini hasa mradi huu utaanza kutekelezwa. Hata hiyo, Serikali ikishirikiana na *TANESCO* inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kugharimia mradi wa kupeleka umeme katika Kijiji cha Lupa Tingatinga. Ni kwamba Serikali inatambua sana juhudzi za Mheshimiwa Mbunge za kufuatilia mradi huu.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya hali ya kifedha ya *TANESCO* kuboreka vifaa vingi kutoka nje ya nchi viliagizwa na vifaa vyote vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ambavyo vilikuwa vimeadimika kwenye ofisi ya *TANESCO* Chunya vimepelekwa kutokana na mahitaji ya ofisi hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mita zilizopelekwa Chunya ni 225 na idadi ya mita zilizofungwa ni 203, nyaya za ukubwa wa *MM* za mraba 50 za *Aluminium* zilizopelekwa Chunya ni meta 11,910 na zilizotumika ni meta 11,000. Pia nyaya za ukubwa wa *MM* za mraba 25 za *Aluminium* zilizopelekwa Chunya ni meta 6,809 na meta zilizotumika ni meta 6,715 na nyaya za ukubwa wa *MM* za mraba 16 za *Copper* zilizopelekwa Chunya ni meta 1,122 na zilizotumika ni meta 1,000.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu gari la uhakika ni kweli kama ilivyo kwa ofisi nyingi za *TANESCO* gari la Chunya limechakaa. *TANESCO* imeshaanza kushughulikia zabuni za ununuzi wa magari kwa maeneo ambayo magari yake ni machakavu. Hata hiyo, kama hatua ya muda mfupi ofisi ya *TANESCO* Chunya imepatiwa gari kutoka ofisi ya *TANESCO* Mkoani Mbeya ili kuhakikisha kwamba huduma nzuri inaendelea kutolewa kama kawaida.

MHE. NJELU E. M. KASAKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

La kwanza, kwa kuwa hivi karibuni kuna taarifa kwamba mapato na makusanyo ya fedha katika *TANESCO* sasa ni mazuri. Kutokana na hali ya makusanyo ya fedha kuwa nzuri, sasa mradi huo Mheshimiwa Naibu Waziri anakadiria unaweza ukaanza lini ili kutuhakikishia angalau watu wapate matumaini kwamba kwa kuwa hali ni nzuri mradi huo unaweza ukaanza?

La pili, ni kwamba gari la pale Wilayani ni mbovu sana na Wilaya ya Chunya ni kubwa sana. Kutoka Chunya mpaka Makongorosi ni parefu. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri aweke mkakati rasmi wa kupeleka gari ambalo ni jipya na ni nzuri kwa ajili ya matumizi katika Wilaya ya Chunya.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika siku za hivi karibuni mapato ya *TANESCO* yameongezeka na ndiyo maana wakati najibu swal la Mheshimiwa Mbunge nimesema kwamba kutokana na kuboreka kwa mapato imewezekana sasa kununua vifaa na kuvipeleka katika maeneo mbalimbali na hususan ikiwa kwenye Ofisi ya *TANESCO* Chunya. Lakini pamoja na hayo ni kwamba mapato haya kuboreka pia ina maana *TANESCO* ina uwezo wa kuweza kulipia mambo mengine ya uendeshaji. Lakini kuhusu ofisi ya Chunya kwa kweli ni uthibitisho wa kuboreka kwa mapato hayo hapo awali isingewezekana pengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitashirikiana naye kuhakikisha kwamba Chunya *TANESCO* inapata gari bora zaidi. Lakini kama nilivyo sema awali hivi sasa *TANESCO* Chunya ina gari hilo ambalo inaweza kufanya kazi kwa kipindi cha sasa. Tutajitahidi kuhakikisha Chunya *TANESCO* kulingana na ukubwa wake inapata gari bora zaidi.

Na. 393

Soko Huria ni Kero

MHE. LYDIA T. BOMA aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa soko huria nchini ulikuwa na lengo la kumsaidia mkulima lakini sivyo mambo yalivyo badala yake umekuwa kero kubwa na umeathiri maendeleo kwa ujumla hasa wakulima wa Korosho Mkoa wa Mtwara:-

- (a) Je, Serikali inajua kuwa soko huria limekuwa kero kwa wakulima kwa ujumla?
- (b) Je, ni hatua zipi zinachukuliwa za kumlinda mkulima kiuchumi na pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA (k.n.y. WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha mfumo wa Soko huria kwa lengo la kushindanisha wanunuizi mbalimbali wa mazao likiwemo zao la korosho ili mkulima aweze kupata bei ya juu inayoweza kupatikana katika soko la dunia. Pamoja na lengo hili nzuri baadhi ya wafanyakishara binafsi wamekuwa wakikiuka kanuni na taratibu zilizowekwa na Serikali na hivyo kusababisha fujo na vurugu katika soko huria ambayo kwa ujumla wake huwa ni kero kwa wakulima. Katika kuhakikisha kuwa kero hiyo inadhibitiwa Serikali imekuwa ikisimamia kanuni na taratibu zilizowekwa kwa kuwataka wakulima na wafanyakishara kuuza na kununua mazao katika masoko ya maeneo rasmi vikiwemo Vyama vya Ushirika. Vile vile Serikali inahimiza kufanyika kwa ukaguzi wa ubora wa mazao ili kudhibiti ubora wa madaraja yaliyowekwa hatua ya kusaidia kuleta uwazi katika biashara na kuepusha wakulima wasipunjwe bei.

Aidha, kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali inahakikisha kuwa Halmashauri za Wilaya zinatunga na kuzitumia sheria ndogo ndogo zitakazowadhibiti wafanyakishara wanaokiuka kanuni na taratibu za masoko na kuondoa uholela na fujo katika ununuizi wa mazao ya wakulima.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa kumlinda mkulima kiuchumi pamoja na Pato la Taifa kwenye zao la korosho ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha kuwa ununuizi wa korosho unalenga katika kumpatia mkulima bei nzuri kwa kuwakutanisha wadau wote katika kikao cha pamoja kinacho jumuisha vilevile wenye viwanda vya kubangua korosho na maafisa wa Wizara ya Kilimo na Chakula na Ushirika na Masoko ili kupanga bei ya kuanzia majadiliano yaani *floor price* kabla ya ununuizi kuanza.

(ii) Serikali inahamasisha ubanguaji wa korosho ili ziweze kuuzwa moja kwa moja kwa walaji na hivyo kupata bei nzuri badala ya kuuza korosho ghafi. Ili kutekeleza azma hii Viwanda viwili vya korosho (Kibaha na Masasi) vimekarabatiwa na kukodishwa kwa wawekezaji.

Aidha, Makampuni mengine matatu yamewekeza katika ubanguaji wa korosho. Makampuni hayo ni *Premier Cashew Industries Limited*, *Mohamed Enterprises Limited* na *Olam (T) Limited* ambayo katika msimu wa 2002/2003 hadi kufikia mwezi Aprili, 2003 yamebangua tani 705.9 na kuuza nje tani 505.9 ambazo thamani yake ni dola za Kimarekani 1,484,436.

(iii) Kuwezesha Vyama vya Ushirika vya Msingi kupata fedha ya kununulia korosho na hivyo kutatua tatizo la Vyama hivyo kukosa mitaji. Kwa mfano katika msimu wa 2001/2002, Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Nakopi, Mpowora, Nanganga, Nangoo na Lukuledi vilipata fedha kutoka Benki ya *Exim* kwa dhamana ya Halmshauri ya Wilaya ya Masasi ambapo kila Chama kilipata shilingi milioni 24 na viliweza kurejesha mikopo hiyo.

Kwa Vyama vingine vya Ushirika vya Kahawa na Pamba msimu wa 2002/2003 vilipata fedha ya kukusanya mazao hayo kutoka *CRDB Bank* kwa dhamana ya Serikali mara tu baada ya kuanzishwa Mpango wa *Export Credit Guarantee Scheme (ECGS)*, mapema Julai, 2002 na kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyoleza katika hotuba yake ya Bajeti, Mpango huo utaendelea kutekelezwa pia mwaka huu wa 2003/2004 kwa kushirikisha vyombo mbalimbali vya fedha ikiwemo Mfuko mpya wa kudhamini wakulima wadogo, wavuvi na wafugaji utakaoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro kadhaa zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sera ya Soko Huru ambazo Serikali inaendelea kuzirekebisha; kwa ujumla wake sera imeonyesha kuleta mafanikio katika kuboresha biashara ya mazao ya wakulima.

MHE. LYDIA T. BOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na Majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Moja, je, kwa kuwa Serikali imeondoa ushuru kwa nia njema ya kuwaondolea wananchi usumbufu na kero mbalimbali. Ni mikakati gani mizuri zaidi ambayo sasa hivi Serikali inaiweka katika kuondoa usumbufu wa watu ambaa wanazunguka bado kwa njia za panya?

La pili, kwa nini kusiwe na mfuko wa *STABEX* katika zao la Korosho sawa na mazao mengine kama ya kahawa kwa sababu bado zao hili linasumbua? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuzuia njia ya panya hilo ningependa kutoa mwito kwa Serikali za Vijiji kushughulikia kudhibiti tatizo hilo. Kwa sababu Wizara kutoka Dodoma kusimamia maeneo yenye korosho haiwezi kufanya shughuli hii peke yake.

La pili, suala ambalo linahusu *STABEX* ninachowenza kusema ni kuwa naomba suala hili uliletu upya kusudi tuweze kulijibu vilivyo. (*Makofî*)

MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la msingi lina uhusiano na kujenga Vyama vya Ushirika na kwa kuwa siku za nyuma Vyama vya Ushirika vyenyewe vilikuwa vinapanga bei katika maeneo yao yaliyosajiliwa na wanapoweka bei walikuwa wanaweka kanuni kwamba mkulima mwanachama wa chama hicho hawezi kuuza mazao yake kwa mtu ambaye si mwanachama au si *society* yake. Sasa kwa utaratibu wa sasa soko huria ambalo halifungi na halipi vyama haki hiyo; haoni kwamba sababu hiyo inavia Vyama vya Ushirika? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa utaratibu huu wa ushirika unafanya kazi vizuri kama wananchi wote wangkuwa wanachama wa ushirika. Kinachowafunga ni ile dhana inayoitwa *Patronage* kuwa wewe mwanachama hutauza mazao zaidi ya kwenye chama chako. Lakini kwa lengo la kumpa mkulima bei nzuri katika kushindana kwa wanunuizi tukaweka soko huru sisi wenywewe.

Sasa kwa hiyo, dhana haiwezi tena kufaa kwa sababu tumeondokana na kule katika kutoa bei ya kufunga wanaouza mazao. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kuwa kwanza tufanye jitihada kila inapowezekana kuwahamasisha wananchi tuwe na ushirika nchi nzima kusudi pasionekane na watu wanaweza kupenyeza na kuvuruga soko la ushirika. (*Makofî*)

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa makusudio ya Serikali kuweka soko huria ilikuwa makusudi kwa ajili ya kuweka ushindani kwa wafanyabiashara. Lakini kwa kuwa sasa wafanyabiashara hao wanajipangia bei zao wenyewe, je, Serikali haioni kama kuna umuhimu mkubwa wa kuvisaidia Vyama vya Ushirika kuwapa mikopo ya kutosha ili kununua mazao ya wakulima ili kuweka ushindani katika soko? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali imeliona hilo na imeweka utaratibu wa kuwakopesha wanaushirika fedha. Ninayo orodha hapa ambayo inaonyesha vyama mbalimbali ambavyo vimeomba mikopo kupitia Benki ya *Exim* na *CRDB*. Inawezekana naomba tena kutoa mwito uvihimize hivi Vyama vya Ushirika vishirikiane na Wizara ya Ushirika na Masoko kupata hiyo mikopo kama sio kupitia Benki ya *Exim* kama vyama vingine vinavyofanya, basi vitumie *SACCOS* na *SCCULT* ipo karibu sana. (*Makofi*)

Na. 394

Kero ya Taa za Kuongozea Magari Barabarani

MHE. PETER KABISA aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na kwamba swalii hili limeulizwa mara kwa mara hapa Bungeni na majibu mazuri kutolewa lakini bado kero kubwa ya taa za kuongozea magari barabarani kuingiliwa na Askari wa Usalama wa Barabarani linaudhi na linaathiri *Smooth Traffic flow* kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam kama vile taa za kwenye Makutano ya Barabara za Ali Hassan Mwinyi, Kinondoni, Morogoro na *Kawawa Road* na kadhalika; na kwa kuwa kama tatizo nililoeleza hapo juu na mifano yake kama linatokana na msongamano wa magari wakati wa *rush hours*:-

(a) Je, taa hizo haziwezi kuwa *programmed* upya ili ziruhusu magari kwa muda mrefu zaidi kama dakika 3 hivi badala ya dakika 1 ya kawaida upande wa barabara yenyе msongamano wa magari mengi, ili kazi ya Askari wa Usalama Barabarani ibakie kulinda usalama, kwa kuhakikisha madreva wanaaheshimu sheria za barabarani na kuongoza magari pale tu viongozi wakuu wanapopita au dharura nyingineyo?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kutekeleza hayo nililoeleza kwenye sehemu “a” ya swalii hili ili kuondoa kero, maudhi na kutoathiri *Smooth Traffic Flow*?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa msongamano wa magari katika barabara mbalimbali Jijini Dar es Salaam umekuwa kero kubwa kwa wenyе magari na watumiaji wengine wa barabara hizo. Msongamano unakuwa mkubwa zaidi katika Makutano ya Barabara Kuu kama vile kwenye Makutano ya Barabara za Ali Hassan Mwinyi na Barabara ya Kawawa, Barabara ya Nyerere na Mandela na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa uwekaji wa taa za kuongoza magari kutoka Wizara ya Ujenzi wametoa maelezo kuwa inawezekana taa za barabarani kuwa *programmed* ili ziruhusu magari kutoka upande wenyе msongamano yapite kwa muda wa dakika usiozidi mbili (dakika 2) dhidi ya dakika 1 kwa magari yanayotoka upande usio na msongamano.

Aidha, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Mkoani Dar es Salaam (*TANROADS*) wanaendelea kufanya utafiti wa kina katika barabara zote kuu za Jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kuangalia alama za barabarani na taa za kuongozea magari kwa lengo la kujua jinsi ya kuboresha usafiri katika barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti kuhusu hali ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam uliofanywa hivi karibuni na wataalamu kutoka Japan, unaonyesha kwamba ufumbuzi wa kudumu na wa uhakika wa tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam utapatikana tu pale barabara za

katikati ya Jiji zitakapopanuliwa na katika baadhi ya maeneo kujengwa barabara za juu kwa juu (*Flyovers*). Hivyo pamoja na hatua za kuweka mpangilio mzuri wa taa za kuongoza magari, pia zinahitajika hatua za ziada za kuboresha hali ya barabara za Jiji la Dar es Salaam.

Kwa kifupi tatizo la kurekebisha barabara za Jiji la Dar es Salaam, pamoja na msongamano wa magari, linafanyiwa kazi na Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Napenda kuuliza je, pale ambapo kuna upendeleo wa upande mmoja wa magari je, raia ana uwezo na anaruhusiwa kumsogelea askari anayeongoza magari kwamba aangalie na upande wa pili pia? (*Makofî/Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama inatokea kuna hisia kwamba askari aliyopo hapo katika barabara fulani anapendelea si shauri kwamba umsogee, umnong'oneze, umkonyeze maana inaweza ikaashiria mambo mengine.

Ninachoshauri mimi kama hitilafu hiyo inaonekana kuna mtu anayefanya kitendo kama hicho kwa makusudi kabisa anazua magari ya upande mwengine ili kupendelea naomba mtoe taarifa kwa viongozi wake ili hatua zichukuliwe kuliko kwenda kumsogelea, kumnong'oneza au kumkonyeza hiyo itaashiria mambo mengine. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa moja kati ya sababu za huo msongamano wa magari Dar es Salaam hasa wakati wa saa za kwenda na kutoka kazini kwenye barabara kama za Bagamoyo, Kilwa na Morogoro ni magari mazito ambayo yanakwenda *speed* ndogo sana. Je, Serikali iko tayari kupokea ushauri kwamba ipige marufuku magari makubwa na yanayokwenda polepole kutembea wakati wa saa za kwenda kazini na kurudi kazini ili watu wawahi kazini? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, katika mpangilio wa sasa wa barabara za Jiji la Dar es Salaam magari yale makubwa yenye mizigo ambayo mara nyingi yanatoka upande wa Bandarini kubeba mizigo halafu yanaleta huku Bara yametengewa barabara maalum ambayo inaitwa *Port Access Road* au Barabara ya Mandela. Kwa kweli ile ndio barabara rasmi ya magari yote makubwa yenye mizigo mizito yanayotembea pole pole katika Jiji la Dar es Salaam. Sasa kama kuna watu wenye mizigo, magari kama hayo yanaonekana katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwa kweli hiyo ni dosari. Ushauri wako tunaupokea na tutawaambia Askari wa *Traffic* wayakamate magari kama hayo kwa sababu iko barabara rasmi ya magari hayo na sio huko kati kati ya Jiji.

Na. 395

Wataalam wa Zimamoto

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA aliuliza:-

Kwa kuwa mara kwa mara yanapotokea maafa ya kuzuka kwa moto katika majengo yetu hasa katika maofisi yenye maghorofa marefu, huelezwa kwamba tunao wataalam wazuri wa Zimamoto ila tatizo ni upungufu wa vifaa vya kuzimia moto:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na suala hilo nyeti la Kitaifa?

(b) Je, kwa hivi sasa Serikali inategemea Taasisi gani binafsi kushirikiana nayo inapotokea janga la moto, hasa katika majengo marefu?

(c) Je, Serikali imeshatumia kiasi gani kuilipa Taasisi hiyo katika maafa hayo kwenye kipindi cha 2000 - 2002?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Moja ya matukio yanayohatarisha maisha ya wananchi na mali zao ni maafa ya moto ambayo hutokea mara kwa mara. Mikakati inayochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na tatizo hili ni kama :-

(i) Kuviongeza uwezo wa kupambana na moto vikosi vyote vya Zimamoto katika Viwanja vya Ndege, Bandari na katika Halmashauri za Miji kwa kuvipatia vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na magari ya Zimamoto.

(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu namna ya kujiепusha na majanga ya moto na pia namna ya kutumia vifaa vidogo vidogo vya kuzimia moto (*Portable Fire Extinguisher*).

(iii) Kuimarisha Chuo cha Mafunzo ya Zimamoto kilichopo Dar es Salaam ili kuongeza ujuzi wa askari wa Zimamoto katika vikosi mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa ipo Kampuni moja tu ya binafsi yenye kikosi cha Zimamoto inayoitwa Knight Support iliyoko Dar es Salaam. Kampuni hii imewekeana mikataba na watu na Makampuni binafsi kutoa ulinzi pamoja na kinga dhidi ya majanga ya moto. Hata hivyo inapotokea tukio kubwa la moto, kikosi hiki huitwa ili kushirikiana na vikosi vya Serikali katika kuzima.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijaingia Mkataba wa kuzima moto na Taasisi yoyote binafsi. Mikataba na Kampuni ya *Knight Support* ya kuzima moto hufanywa kati ya watu binafsi au Taasisi wao wenye kwa makubaliano ya wenye kwa wenye. Hivyo, kwa kuwa Serikali haijaingia Mkataba na Kampuni yoyote kuzima moto, hakuna gharama zozote zilizotumika kulipa Kampuni hiyo kwa kipindi cha mwaka 2000/2002.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza suala dogo.

Kwa kuwa ajali za moto katika Ofisi za Serikali na Taasisi zake imekuwa kama mchezo wa kuigiza. Je, Serikali inalichunguza suala hili kwa namna gani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ajali za moto sio mchezo wa kuigiza ni tatizo hasa la kweli kweli. Kwa upande wa Serikali wala hatulifanyii mzaha kwa sababu tunajua kiasi cha hasara ambayo inapatikana kutokana na moto. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi na hata katika Bajeti yetu tulioisoma mbele ya Bunge hili tumetaja hatua mbalimbali za kuongeza dhana. Tatizo kubwa linalotokea katika suala hili ni kwamba vikosi mbalimbali vinakosa na zenyewe ni ghali sana hasa vile vikosi ambavyo viko kwenye Halmashauri za Miji.

Kwa mfano mwaka uliopita tulitenga shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya kununua magari mawili kwa ajili ya Dar es Salaam. Katika gari hilo moja ni lile lenye ngazi ndefu kwa sababu Dar es Salaam majengo yamekuwa marefu zaidi magari ya kuzimia moto yanafika mwisho mita 30 wakati kuna majengo yana mita 60 sasa hivi pale Dar es Salaam kwa hiyo, gari kama hili limeshaagizwa litafika hivi karibuni. Dar es Salaam vile vile tunaongeza magari matatu ili kila Manispaa ipate gari ya kuzimia moto. Manispaa ya Morogoro imepata gari jipya hivi karibuni na katika Bajeti hii vile vole Mji wa Mwanza utapatiwa magari mawili ya Zimamoto, hizi ni jitihada za Serikali za kuongeza dhana katika vikosi vyetu ili tupambane sawa sawa na majanga ya moto.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wafanyakazi wengi hivi sasa wanafundishwa jinsi ya kupambana na majanga ya moto. Je, kuna mkakati gani wa sisi Wabunge kufundishwa jinsi ya kupambana na majanga ya moto? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa hivi Kikosi cha Zimamoto kinafanya mafunzo katika maeneo mbalimbali ya namna ya kuzima moto, karibu kinamaliza Wizara zote kutoa mafunzo hayo. Nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba muda si mrefu Kikosi hicho kitafika hapa Dodoma katika moja ya vikao vijavyo ili kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu bila mafunzo hayo wakati mwengine moto unaanza ukiwa mdogo sana. Sasa kama watu wamefundishwa kutumia vifaa hivi vidogo vidogo na nina hakika katika Ukumbi huu. Mheshimiwa Spika, alishatuhakikishia kwamba viro vifaa vidogo hayo ni mafunzo muhimu sana kwa sababu tunaweza tukaudhibiti moto. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge tukae katika mkao wa kufundishwa namna ya kuzima moto hivi karibuni. (*Makofit*)

Na. 396

Utaratibu wa Kulinda Ajira za Walimu wa Kike

MHE. MARIA D. WATONDOHA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kwamba walimu wa Shule za Msingi sasa wataajiriwa na Halmashauri; na kwa kuwa walimu ni wa kike na wa kiume; na kwa kuwa walimu wa kike si lazima waolewe na walimu wenzao:

Je, Serikali itaweka utaratibu gani thabiti wa kulinda ajira za walimu wa kike pale watakapolazimika kuwafuata waume zao amba si walimu toka Halmashauri moja kwenda nyingine bila kuathiri ajira zao?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeamua kwamba walimu wote wa Shule za Msingi katika hatua ya mwanzo watakuwa wanaajiriwa na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Halmashauri hizo zina madaraka ya kuajiri walimu, lakini ajira zao zitaendelea kulindwa na Tume ya Utumishi ya Walimu (*TSC*) na hawataathirika kwa namna yoyote katika maslahi yao yote ambayo yatafanana nchi nzima kwa walimu wa kila ngazi.

Aidha, pale ambapo walimu wanawake wataomba uhamisho ili kuwafuata waume zao waliopata uhamisho, walimu hao wanawake watapaswa kufuata taratibu za kiutumishi Serikalini kama zilivyoainishwa na Tume ya Utumishi ya Walimu (*TSC*) pamoja na Mikataba yao ya ajira. Utaratibu uliopo kuhusu uhamisho ni kwamba Mwalimu mwanamke ataruhusiwa kuhama kumfuata mume wake lakini ajira kule anakohamia itategemea nafasi. Endapo nafasi haitakuwepo ataruhusiwa ama kuingizwa katika orodha ya kusubiri nafasi kwa utaratibu wa aliyetangulia kupewa kwanza, *First In, First Out (FIFO)* au kubakia alipokuwa mpaka nafasi iwepo kule anakohamia. Wizara imetoa maelekezo ya utaratibu wa uhamisho na upangaji wa walimu katika Waraka wa Elimu Na. 4 na Na. 10 wa mwaka 2001 na ufanuzi wa utekelezaji umetolewa katika Waraka wa Elimu Na. 17 wa mwaka 2002.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na ufanuzi wake juu ya taratibu zilizopo. Je, kumtenganisha mume na mke wake kwa kipindi kirefu kutohana na kukosekana nafasi katika kipindi hiki cha janga la Ukimwi haoni ni athari mbaya, Serikali itaweka utaratibu gani? (*Makofit*)

Pili, kwa kuwa ilisikika katika baadhi ya vyombo vya habari viongozi wa elimu wakisema uamuzi ni wa mwanamke ajira au kumfuata mume. Serikali iko tayari kurekebisha kauli hiyo kama kweli ilitolewa? (*Makofit*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, la kwanza kama kweli ni sahihi kumtenganisha mke na mume kwa muda mrefu katika kipindi hiki.

Mimi napenda nikubaliane naye kwamba si vizuri, lakini anayeamu kwamba uwepo utenganisho huo sio Serikali, ni taratibu za kazi. Mtu umeajiriwa unaweza kupata uhamisho. Mwanamume anaweza kupata uhamisho na mwanamke anaweza kupata uhamisho.

Kwa hiyo, Serikali kama mwajiri inachofanya ni kuweka utaratibu wa kuruhusu sio wa kukataza. Napenda niwe wazi hapa utaratibu uliopo unamruhusu mke ahamishwe kwenda kule ambako mume wake amehamia. Sasa kama imetokea aliyelama ni mwanamke na mwanamume anataka kuungana naye akiomba ni jambo linaloweza kufikiriwa. Tunayo mifano kuna wanaume wameomba kuhamishwa kwenda walikokwenda wake zao. Mimi nafahamu mwanamke aliyepewa nafasi ya kuwa *RAS* na mume wake yuko katika Wizara ya Elimu tulipoomba kumhamisha tumemuhamisha tulifanya utaratibu wa kumhamisha ili awe karibu na mama. Kwa hiyo, taratibu zipo tunaweza kuzichukua.

Sasa katika hilo suala la pili kwamba ilisikika katika vyombo vyahabari kwamba tumesema mwenye kuamua ni mwanamke. Mimi sijui alisema nani jambo hili. Lakini ninachosema mimi utaratibu ni huu nilioueleza na utaratibu huu umefanuliwa kwenye zile nyaraka za elimu nilizozitaja. Sasa wakati mwagine vyombo vyahabari hutafsiri vibaya maneno haya. Mimi napenda tuzingatie taratibu zilizotolewa katika nyaraka za elimu na maelezo niliyoyatoa hapa Bungeni. (*Makofit*)

Na. 397

Matatizo ya Maji Mji wa Mtwara

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni muhimu sana kwa maisha ya wanadamu; na kwa kuwa maji hutolewa kwa mgao katika Mji wa Mtwara na kusababisha wakazi wa Mji huo kutokupata maji ya kutosha:-

(a) Je, ni sababu zipo zinazosababisha maji yatolewe kwa mgao na kusababisha wakazi wa mji huo kutokupata maji ya kutosha?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba kutokana na tatizo hilo wakazi wa Mji wa Mtwara wanaathirika sana ki-afya?

(c) Je, ni lini tatizo hilo litatatuliwa ili wananchi wa Mtwara Mjini waondokane na kero hiyo?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maji yanatolewa kwa mgao katika Mji wa Mtwara kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Umeme unaopatikana kutoka *TANESCO* unawezesha kuendesha mitambo ya kusukuma maji wastani wa saa 15 kwa siku badala ya 24 zinazotakiwa. Mitambo hiyo ikiendeshwa kwa muda wa saa 24 bila kusimamia, hutoa maji kiasi cha lita 8,500,000 kwa siku badala ya lita 5,300,000 za sasa. Kiwango hicho kingeweza kukidhi mahitaji ya maji ya hivi sasa ambayo ni lita 16,000,000 kwa asilimia 50 badala ya kiwango cha hivi sasa cha asilimia 33.

(ii) Uchakavu wa baadhi ya mitambo ya kusukuma maji ambayo ilifungwa zaidi ya miaka kumi iliyopita.

(iii) Miundombinu ya uzalishaji maji ina uwezo mdogo wa utoaji maji ukilinganisha na mahitaji. Uwezo wa juu kabisa wa kutoa maji wa vyanzo vilivyopo ni lita 8,500 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kama unavyoona Serikali inalielewa vyema tatizo hilo pamoja na athari zake kiafya. Hivyo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Mjini Mtwara, Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kupunguza kero ya maji kwenye mji huo:-

(i) Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2000/2001 hadi 2002/2003 Serikali imechukua hatua za muda mfupi ili kuboresha huduma za maji ikiwa ni pamoja na kununua pampu mpya 7. Mwaka 2000/2002 pampu (*Booster Pumps*) 3 zilifungwa katika kituo cha kusukuma maji Mtawanya. Katika mwaka 2002/2003 pampu mbili zimenunuliwa kwa ajili ya kituo cha kusukuma maji cha Magamba pamoja na pampu (*Submersible pumps*) mbili kwa ajili ya visima virefu nya Mtawanya.

Pia, mabomba yenye urefu wa kilomita 2.8 yamenunuliwa kwa ajili ya kufikisha mtandao wa usambazaji wa maji kwenye maeneo ya Magomeni Mbezi. Aidha, Wizara imepeleka shilingi 9,000,000/= kwa Mkurugenzi Mtendaji Maji Mjini Mtwara ili kufanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi na kuchimba kisima kirefu kimoja. Jumla ya shilingi 76,295,452 zimetumika kwa miaka hiyo miwili.

Mpango wa muda mrefu ni pamoja na kufanya upembuzi yakinfu wa uondoaji Majitaka. Mradi huu unatarajiwa kugharimiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

(ii) Mamlaka imewasiliana na *TANESCO* Makao Makuu na wanatarajia kununua jenereta mpya ambayo inatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Septemba, 2003. Baada ya kufungwa jenereta hiyo tunatarajia kwamba mitambo ya kusukuma maji itawenza kupatiwa umeme kwa saa 24 badala ya 15 za sasa.

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini pia niishukuru *TANESCO* kwa mpango wa muda mfupi wa kuleta mashine ya umeme Mtwara.

Ninalo swali dogo la nyongeza kwamba maadamu kuna uhaba wa maji lakini pia kuna matatizo ya maji katika maeneo kadhaa ya Mjini Mtwara kwa mfano Mkangala, Mbawalachini, Naliendele, Kilimahewa na Mitengo. Je, Wizara ipo tayari sasa kuisaidia Bodi ya Maji ya Mjini Mtwara ili kuweza kupeleka maji katika maeneo niliyoyataja? (*Makofî*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nampongeza kwamba anafuutilia sana tatizo la maji katika Mji wa Mtwara. Nampongeza na kumshukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema Serikali inatambua tatizo la maji Mtwara na tunahangaika kulishughulikia. Ndiyo maana katika kipindi cha miaka miwili iliyopita tumetoa zaidi ya shilingi milioni 76. Tutaendelea kuhangaika na tatizo la maji Mtwara mpaka tuhakikishe vijiji hivyo unavyovitaja na vyenyewe vinapata maji.

Na.398

Vyanzo vya Maji Wilaya ya Masasi

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Masasi imebahatika kuwa na vyanzo vingi vya maji zikiwemo chemchem za Mwiti, Mwena, Ndanda, Liputu, Mbwinji, Nahinga na kadhalka; na kwa kuwa vyanzo hivyo vinaweza kutosheleza mahitaji ya maji safi na salama katika Wilaya ya Masasi na pengine Wilaya jirani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani ama *Master Plan* gani ya kutumia vizuri raslimali hii ya chemchem ambayo ipo kwa uhakika ili kuondoa uhaba mkubwa wa maji katika Wilaya ya Masasi?

(b) Je, Serikali itaanza lini kutekeleza mpango wa kufufua visima vilivyoziwa, kukarabati mashine za maji, na kufufua malambo katika eneo la Masasi Magharibi katika vijiji vya Nanyindwa, Chilala, Mpanyani, Namajani na kadhalika?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu uhaba mkubwa wa maji unaowakabili wananchi wa Masasi Magharibi kuanzia Namajani mpaka Chingulungulu, Mihima mpaka Lukuledi na Mtakuja ili waweze kujuwa endapo matatizo haya yapo katika kipaumbele cha kutatuliwa?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Serikali iligharamia na kuandaa Mpango kamambe (*Water Master Plan*) wa Mkoa wa Mtwara kati ya mwaka 1976 na 1978na kufanyiwa mapitio mwaka 1986. Mpango huo uliainisha na kutathmini vyanzo vyote vya maji kwa Mkoa ikiwa ni pamoja na Chemchem za Mwiiti, Mwena, Ndanda, Liputu, Mbwinji na Nahinga vilivyoziwa Wilaya ya Masasi. Mpango huu ulielekeza pia matumizi bora ya raslimali za maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango huu Chemchem za Mwena, Ndanda na Liputu zinahudumia baadhi ya Vijiji vya Wilaya ya Masasi.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na matunzo yasiyordhisha na miradi ya maji katika Wilaya ya Masasi baadhi ya visima na mitambo ya maji haifanyi kazi. Ili miradi ya maji iwe endelevu, sera ya Maji inawataka wananchi wenyewe wasimamie na kutunza Miradi ya Maji Vijijini na Serikali itasaidia Wananchi ambao wataonyesha kuwa wanaweza kumiliki, kutunza na kugharamia uendeshaji wa miradi itakayojengwa au kufanyiwa ukarabati.

Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge wa Masasi kuwa, ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuhamasisha wananchi wa Jimbo la Masasi Magharibi ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Nanyondwa, Chilala, Mfanyani na Majani ili waunde Kamati na Mifuko ya Maji. Serikali itakuwa tayari kutenga fedha kwa ajili ya kufufua visima, mashine za maji na malambo kwenye Vijiji ambavyo vitakuwa vimejiandaa vizuri kama Sera inavyosema.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la maji katika Jimbo la Masasi Magharibi na imekuwa ikichukua hatua za kupunguza tatizo hili. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa, karibu kila Kijiji katika Jimbo la Masasi Magharibi lilikwischimbibiwa kisima kirefu au kifupi katika jitihada za kusambaza huduma ya maji. Baadhi ya visima hivyo havifanyi kazi kutokana na matatizo niliyoyaeleza hapo juu. Serikali itaendelea kugharamia miradi ya maji katika Jimbo la Masasi Magharibi, katika Vijiji ambavyo vinajiandaa na kushiriki.

SPIKA: Mheshimiwa Raynald Mrope, muda wa maswali umekwisha na kwa kuwa unashubiri majibu ya umeme wa Masasi nina hakika hutalalamika.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo kwa leo. Kwa hiyo, Katibu endelea na *Order Paper*.

KAULI ZA MAWAZIRI

**KAULI KUHUSU SERIKALI KUPELEKA UMEME KATIKA
VIJIFI VYAMWENA, CHIKUNDI, CHIGUGU, CHIKUKWE, NAMAKONGWA, NANGANGA
NA NANGOO**

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Agosti, 2003, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, aliwasilisha Bungeni maelezo yake binafsi akihoji ni lini Serikali na Shirika la *TANESCO* watapeleka umeme katika Vijiji vya Mwena, Chikundi, Chigugu, Chikukwe, Namakongwa, Nanganga na Nangoo.

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa miaka ya 1980, *TANESCO* iliamua kuunganisha umeme toka Masasi mpaka Lindi ili kutumia umeme wa ziada uliokuwa unazalishwa na jenereta ya Masasi. Lengo kuu

liliwa kuupatia umeme wa kutosha Mji wa Lindi pamoja na Kiwanda cha Korosho kilichoko Mtama. Mji wa Lindi haukuwa na umeme wa kutosheleza mahitaji yake kwa wakati ule. Hata hiyo, lengo la mradi halikutimia kutokana na uhaba wa fedha. Laini ya umeme ilijengwa toka Masasi hadi Ndanda ambayo ilikamilika mwaka 2000. Kutokana na uhaba wa fedha ulioikabili *TANESCO*, laini hii haikuweza kuendelezwa hadi Kijiji cha Nyangao, mahali laini ya umeme kutokea Lindi ilipoishia.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa mashine za Masasi wakati zimefungwa tu ulikuwa ni kuzalisha umeme kiasi cha *megawatts 41/2*. Sasa hivi mashine hizo uwezo wake wa kuzalisha umeme umepungua hadi *megawatts 3.65*. Kwa wakati huu mahitaji ya umeme Masasi yamekua hadi kufikia *megawatts 3.5*. Mashine hizi za Masasi zinatoa umeme kwa Viwanda vya Kubangulia Korosho pamoja na Mji ya Masasi, Newala, Nachingwea, Tandahimba na pia pampu za maji za Mkunya na Makondeko. Kwa hiyo, kiufundi siyo busara kuendelea kuunganisha umeme huu wa Masasi kwa kupeleka maeneo mengine hadi hapo uwezo wa kufunga mashine zingine mpya utakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Shirika kuhusu Vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Raynald Mrope, ni kwamba, *TANESCO* kuitia ofisi zake za Mkoa wa Mtwara, ilishafanya upembuzi yakinifu kuona uwezekano wa kupeleka umeme katika Vijiji vya Mwena, Chikundi, Chigugu, Chikukwe na Namakongwa. Matokeo ya upembezi huo ni kama ifuatavyo: -

(i) Ili kufikisha umeme katika Vijiji vya Mwena na Chikundi zinahitajika jumla ya shilingi milioni 42.5 ili kuweza kufanya kazi za ujenzi wa laini ya kilovolti 33, urefu wa 1/2 kilomita, ujenzi wa laini ya kilovolt 0.4, urefu wa kilomita 4 na kufunga vipoza umeme viwili vya uwezo wa *KVA 200 33/0.4 KV* na *KVA 50* katika Vijiji vya Mwena na Chikundi.

(ii) Mradi mwingine ni wa kufikisha umeme katika Vijiji cha Chigugu, Chikukwe na Namakongwa unaokadirwa kugharimu kiasi cha Shilingi milioni 41.1. Kazi za mradi huu ni ujenzi wa *line* ya kilovolti 33 yenye urefu wa 1/2 kilomita, ujenzi wa laini ya kilovolti 0.4, urefu wa kilomita 4.5 na kufunga vipoza umeme vitatu. Kila Kijiji kitafungiwa kipoza umeme kimoja chenyе uwezo wa *KVA 100 33/0.4 KV*.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, miradi hii itakayogharimu kiasi cha shilingi milioni 84 inatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004. (*Makofi*)

(iii) Ili kufikisha umeme kijiji cha Nanganga ambacho kiko umbali wa kilomita 22 kutoka Ndanda jumla ya Shilingi milioni 440 zinahitajika.

(iv) Ili kufikisha umeme Kijiji cha Nangoo chenyе umbali wa kilomita 11 zinahitajika shilingi milioni 220. Fedha hizi zinatarajiwa kupangwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005 na kuendelea hadi 2005/2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye hotuba ya Wizara yangu ya Nishati na Madini Bungeni tarehe 24 Julai, 2003, Sera mpya ya Nishati nchini inasisitiza umuhimu wa Serikali kuendelea kujishughulisha ipasavyo na usambazaji nishati Vijijini hususan umeme. Chini ya programu ya *Institutional Support* Wizarani kwangu inayofadhiliwa na Serikali ya Sweden, tunafanya maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Agency*) pamoja na Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund*), Asasi ambazo zitasimamia kwa niaba ya Serikali uendelezaji wa nishati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, miradi ya umeme inagharimu fedha nydingi sana, kwa sababu fedha hizo hatunazo za kutosha, basi inabidi tutekeleze miradi hiyo kwa awamu na hivyo nawasihi Wananchi wavute subira. Aidha, naomba kuwashakishia Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kuwa, Serikali inatafuta Wawekezaji binafsi na Wafadhili watusaidie kupeleka umeme Vijijini na kwenye Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya nchini kote mapema kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

UCHAGUZI WA WAWAKILISHI WA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeshawatangazia majina ya wagombea. Nadhani kwa utaratibu wetu huwa hawajielezi kwa sababu tunafahamiana. Kwa hiyo, sasa namwomba Katibu aanze utaratibu wa kugawa karatasi za uchaguzi (*ballot papers*).

Napenda kukumbusha tu kwamba, yanahitajika majina matatu kati ya wale niliwasomea na yame pangwa kwa mujibu wa *alphabet*, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, ndio wagombea wetu.

(Hapa Karatasi za Kupiglia Kura Ziligawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, naomba nijue maelekezo.

SPIKA: Mheshimiwa, kuhusu nini?

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu, sina uhakika ndio maana nimeomba maelekezo kwamba, kwa mfano hapa kuna wanaume na wanawake amba wanagombea, lakini huwa naona mahali fulani tunakuwa na utaratibu kwamba, kuna nafasi ile ya lazima labda ya mwanamke. Sasa, katika hii ipo ama haipo?

SPIKA: Katika hii haipo.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Haipo?

SPIKA: Eeeh, haipo.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Ingawa ni muhimu. (*Kicheko*)

SPIKA: Unapiglia kura yejote watatu unaotaka waende Baraza hilo.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walianza Kupiga Kura)

SPIKA: Makatibu, leteni masanduku ya kukusanya kura.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa, naona unataka kupiga kura mara mbili.

MBUNGE FULANI: Sioni. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Huoni! Kama huoni lete mie nikupigie basi, imo hiyo Sheria ya Uchaguzi inaruhusu.

MBUNGE FULANI: Kura ni siri bwana.

(Hapa Kura Zilianza Kukusanya)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kura zinakusanya, nafikiri kila mtu ameshapiga.

MBUNGE FULANI: Bado moja.

SPIKA: Bado moja, kimbia na sanduku kule.

Utaratibu wetu unamtaka Mheshimiwa Spika atue Waheshimiwa Wabunge wawili wawe mashahidi wakati Maofisa wetu wanahesabu kura. Kwa hiyo, ninamteua Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa Estherina Kilasi, wakashuhudie kazi hiyo. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, anataka kuwa shahidi.

SPIKA: Aah, naambiya Spika ameshamaliza kuteua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, asubiri safari ijayo. (*Kicheko*)

Kura zikahesabiwe kwenye chumba cha Spika. Ni utaratibu wa kushuhudia tu, hakuna udanganyifu hapa ndani ya Bunge, watu wote wanakwenda vizuri tu. Tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu Utamaduni, Habari na Michezo (The SADC Protocol on Culture, Information and Sports)

(*Majadiliano yanaendelea*)

SPIKA: Walibaki wachangiaji watatu jana, sasa naendelea na hawa wafuatao, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai.

WABUNGE FULANI: Bado Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

SPIKA: Eeeh, nani?

WABUNGE FULANI: Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

SPIKA: Aaah, Kambi ya Upinzani walikuwa hawajatoa maoni, sawa sawa. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika hoja hii endelea.

MHE. KHAMIS ALI SALEH - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina pingamizi lolote kuhusiana na Azimio hilo. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunayo maoni machache kama kuwa malengo yaliyoainishwa ndani ya itifaki ni ya msingi kwa faida ya nchi yetu na wananchi wake. Wasiwasi wetu ni utekelezaji wa mambo yenye na hasa tukizingatia ufinyu wa Bajeti yetu kama ambavyo imekuwa ikiimbwa ndani ya Bunge hili. Tusije tukawa tunaridhia Itifaki kwa ajili ya *fashion* tu au kufuata mkumbo. Suala muhimu ni kuyafanya kwa vitendo yale tunayoyardhia. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 kuhusu mafunzo kujenga uwezo wa utafiti, inaelezwa kwamba nchi zitashirikiana katika kufanya utafiti, mafunzo kwa mawakala wa utamaduni, wafanyakazi, Sekta ya Habari na Michezo. Pia, kifungu cha 6 kinazungumza nchi husika ndani ya Itifaki hiyo kutafuta na kutenga fedha za kuendeshea mpango mzima katika maeneo ya utamaduni, habari na michezo.

Mheshimiwa Spika, wasiiasi wa Kambi ya Upinzani ni kwamba, iwapo Serikali imeshindwa kutenga fedha za kujenga Kijiji cha Michezo kwa miaka mingi sasa na sehemu hiyo kuendelea kuwa mazilio ya nyoka na panya, hizo pesa za kuingia katika mpango huu wa kiitifikasi zitapatikana wapi? (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Sanaa Bagamoyo na Chuo cha Malya, vimetushinda mpaka kungojea huruma na misaada ya *Scandinavian Countries*; je, kuingia katika Itifaki kama hizi siyo mchezo wa kutimiza mradi?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinazungumzia uboreshaji, upatikanaji mzuri na ulio huru wa habari ndani ya *SADC*. Hili linapingana na hali halisi ya sera yetu na mfumo wa habari wa ndani ambao bado ni wa kubanwabanwa. Wimbo wa Serikali kuleta mabadiliko ya Sera ya Vyombo vya Habari umeendelea kuimbwa tu bila vitendo, si bora tukatengeneza kwanza mazingira yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu kidogo cha (iii) kinasisitiza Nchi Wanachama jukumu la kuendesha kampeni za kuelezea malengo mazima ya mpango huu, shughuli zenyewe na mafanikio yanayopatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini ni ukweli usiopingika kwamba ni Watanzania wachache wanaoweza kufahamu kwa ufasaha malengo, mafanikio na matarajio ya Vyama vyetu sisi wenyewe vya michezo au vya utamaduni.

Mheshimiwa Spika, Kampeni inayozungumziwa ndani ya Itifaki hiyo ya *SADC* ni kinyume na hali halisi tuliyonayo sisi wenyewe. Mpango huo utajikita wapi ili ufanikiwe iwapo mazingira yetu yanapwaya?

Mheshimiwa Spika, *article 19*, kifungu kidogo cha (iv) kinazungumzia kuanzishwa Kitengo cha Pamoja cha Ukusanyaji Habari cha *SADC* ambacho kitakuwa kinatumia mtandao wa kisasa. Tuna wasiwasi baadhi ya nchi ambazo ziko mbele yetu kiteknolojia kama vile Afrika ya Kusini ndizo zitakazofaidika zaidi na habari zitakazokusanywa. Hali hiyo inaweza ikaua Vyombo vya Habari vya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu unaotumika wa Bunge ni kuridhia Itifaki kwa kutimiza malengo na hasa ikizingatiwa kuwa wakubwa wameshamwaga wino, Kambi ya Upinzani haina tena namna ya kuzuia, isipokuwa tukae tayari kukabiliana na changamoto tulizozitaja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii iliyopitia *protocol* hii, lakini kwa leo nitazungumzia eneo moja linalohusu habari.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla sijui hii habari wanayoiongelea humu ni habari ipi, lakini binafsi nilidhani kwamba hata *document* hii ni habari. Sasa nikianzia hapo kwamba *document* hii ni taarifa, ni habari ambayo wananchi na jamii inayolengwa inapaswa kuijua.

Mheshimiwa Spika, jana ilipotolewa nyongeza ya shughuli za leo Bungeni ndio baadhi ya Wabunge ambaو hawakuwa kwenye Kamati waliweza kupata mikataba hii na *protocol* hizi, halafu wakatakiwa wajadili. Sasa, sitaki ku-*question* tulichofanya ni nini, lakini mikataba mingine ilikuwa inakosa watu wa kujadili. Siyo kwamba Wajumbe hawana mawazo, ni kwa sababu walikuwa hawajui kilichokuwa kinaendelea. Sasa, huwezi kusema utawapa watu habari wakati hata sheria yenyewe inayotaka kuwapa habari unaificha. Kwa misingi hiyo, nataka kutahadharisha tu wale wanaohusika kwamba, haya mambo tunakuwa tunayafanyia mchezo, siku nyingine tutakuja kulaumiwa.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa unasoma dua hapo huwa nasikiliza kwa makini halafu kila siku baada ya kufunga shughuli za Bunge natafsiri. Iko mikataba ya Jumuiya ya Ulaya lazima watu wapelekewe na wajadili. Kama ni Waingereza wanajadili kuijiunga ama kutumia fedha fulani, wanajadili Taifa kama Taifa, wala siyo Wabunge tu. Sasa, watu wanajadili halafu wanafanya *referendum*, wanaweka mawazo. Lakini mikataba kama hii tunayojadili hapa, tunajadili kwa dakika mbili ipite, ipite, ipite! Inapita inakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ya utangulizi, sasa nirudi kwenye *section* yenyewe.

MBUNGE FULANI: Huo ni utangulizi!

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, nimesoma kwa makini *section* hiyo. Sasa kitu kinachokwepwa, utaangalia kwenye ukurasa wa 12 *section two, Information*. Pia, kuna *article 17*, amezungumzia *Objectives*. Amekwenda *article 18* akazungumza *Policies* na *Article 19, Availability of Information*. Lakini katika haya yote hakuna anakotaja kwamba, lazima Serikali zilizoko katika nchi za *SADC* zitunge Sheria ambayo labda ni *Access to Information Act by the Media*, hamna! Sama sana anazungumzia watunge Sera. Sasa, hiyo sera ambayo haiongozwi na sheria itakuwa hata Waandishi wa Habari, Vyombo vya Habari na watu wengine wanapata kudra za Kiongozi wa Nchi.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipowaambia watu wake kwamba: “Wapeni watu habari.” Lakini kungekuwa na sheria, basi watu wangekuwa wanalazimika kupata habari zile kwa mujibu wa sheria. Sasa sisi tunaridhia hapa ipite, ipite, hata kama hizo *policies* zitakuwepo, lakini zitakuwa hazina manufaa. Wote tumekubaliana kwamba *information is power*, kwa sababu *through information you get knowledge and knowledge is power too*.

Mheshimiwa Spika, ni bahati nzuri au mbaya kwamba watu walishaweka sahihi, lakini kabla ya kuweka sahihi wangetuletea ili na sisi tuchangie labda pengine tungekubaliana. Hawa *Heads of State* ni *Executive Branch*, wote walikwenda pale na kuna mambo ambayo wao kama *Executive Branch* wasingependa yatoke.

Sasa, unapotuletea kuidhinisha, katika kile tunachoita *public hearing*, bahati mbaya sidhani kama kuna mdaa ye yote au kuna Kamati yoyote imewaita wanasheria ama watu fulani wazungumzie hiyo, licha ya ile nilioisema kwamba Ulaya wanapelekewa wanazungumza Taifa kama Taifa. Sasa, kitu kama hiki kinaonekana kama ni mchezo tu ule wa kuigiza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokuwepo ulazima au kifungu kinachoonyesha kwamba lazima kuwepo na sheria ile ambayo inasema *Access to Information Act*, lakini vile vile katika kifungu cha 23 anazungumzia *Information Infrastructure* na sisi hapa tuangalie labda tuanze sisi.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kwangu pale Kitwe napata *TV Chad* (*Television* ya Taifa ya Chad), sijui ni maili ngapi. Lakini *TVT* wala haifiki, sasa ni aibu miaka 42 ambako mtu sasa aliyezaliwa ndiyo anapaswa kuwa Rais, huwazi kwa mujibu wa katiba yaani miaka yote hiyo, watu walioko kule vijijini hawawezi kuangalia *Television* ya Taifa watu wanasema nini hawawezi wakaangalia.

Sasa kuna Mheshimiwa Mbunge, aliuliza swali akasema hivi Serikali itaonaje aibu, mwingine akajibu kwamba haiwezi kuona aibu. Lakini tunajua kwamba mkosaji ye yote anapoambiwa amekosea ni waungwana wachache tu wanaweza kukubali kwamba kwa hapo anaona aibu. Lakini sisi tunachosema ni kwamba *infrastructure* tunayoizungumza kama huwezi kupeleka hiyo *TVT* ikafika kule na sijui tatizo ni nini kwa sababu mtu mmoja *in individual Television* yake inaweka nchi nzima, inakuwaje hapo hapo ni kitu gani tunachosita?

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza *information infrastructure* tuangalie hapa Bungeni wananchi ambao tunawasemea wametutuma unakaa hapa kuanzia saa 4 mpaka saa 7 halafu baadaye saa 11.00 mpaka sijui saa ngapi yale mnayozungumza saa zote hizo Miswada ya Waziri ameyasoma ambayo wala hamuwaapelekei wananchi, mna-quote dakika mbili au mmoja.

Mheshimiwa Spika, aidha hiyo *information infrastructure* sasa hapo wamekaa kwenye *Press gallery*, mimi nadhani kungekuwa na *laptop*, kungekuwa na *computers connected* kwenye *internet* sasa wanapiga pale pale ya Serikali, habari zinakwenda, lakini sasa hivi inabidi wahame wakimbiekimbie habari nyeti zinawaacha. Nadhani katika hili tunganeanzia hapo lakini ndiyo kwa Mheshimiwa Spika, kanakwenda kwake. Labda kwenye lile jengi jipya atafikiria kufanya hivyo. (*Makofii/Kicheko*)

Sasa mambo kama haya ndiyo mambo ambayo yanatuonyesha kwamba tunachokisema kwa kweli *we are serious*. Maana hata kule Kenya nadhani wanafanya hivyo. Lakini inapofika mahali kwamba vitu hivi hatuvipi umuhimu hii ni pamoja na elimu inayotolewa na waandishi wa habari wanavyolipwa, maana

wako wengine sijui wa Redio Tanzania, sijui wanalipwa shilingi ngapi maana sijawahi kusikia wameiba hata mtambo au wamehujumu mtamba na mtu anahonga. Sasa vitu kama hivyo lazima tuviangalie kwamba tunapotaka kuweka *information infrastructure*. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kuyazungumza hayo nilikuwa naomba kwanza nadhani tumelizungumza sana hizi *protocol* tunazoridhia ni mali ni mali za wananchi wanapaswa kuwa nazo. Sasa hii ya kuletwa dakika za mwisho mikataba mitano yote *as if mme-foresee* kwamba hawatachangia. Mimi mwenyewe inaninyima raha najisikia vibaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa masharti kwamba hicho kipengele waende wakakirudishe na hata kama hamkirudishi kule na wale wanaohusika na habari Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, yuko hapa, tunataka sheria hapa inayowapa waandishi wa habari na wengine habari kwamba wana-address na wanahaki na yule anayezikatalia anashughulikiwa.

Sasa ukisema *address*, Mbunge anasema anataka Mkataba kuuona unaambiwa toka, Mbunge, anataka Mkataba unaambiwa wewe hutauona halafu unafika huku unakaa pale pale unasesma tunasema tumekubaliana tutawapa taarifa na hapa habari ipo wakati Mbunge anataka Mkataba wa Shirika lake, la jasho lake, umeukatalia halafu sasa hapa tunasema eeh upite! Tena ni kweli, tena ni kitu kizuri.

Baada ya kuyasema hayo.....

SPIKA: Kwa kuwa unaelekeza maelekezo yako kwa Spika, mimi sijakatalia mkataba. (*Makofsi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nilisahau kueleza kwamba wagombea uchaguzi nao wana haki ya kuteua mashuhuda wao.

Sasa wawili wamependa kuteua amba ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, amemteua Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud na Mheshimiwa Ruth Msafiri amemteua Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, sasa wanaombwa waende kwenye chumba cha kuhesabu kura. (*Makofsi*)

MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hili sina tatizo ninasema naunga mkono. Ila nilikuwa napenda kuongeza mawili, matatu, katika hii mikataba. Ni kweli ushirikiano wa *SADC* ni mzuri, lakini wasiwasi wangu unakuja katika kupeana habari (*Information*). Wenzetu wameamua kuondoa ushuru wa karatasi kwa sababu habari kwa dunia ya sasa zinavuka mipaka kwa kupitia vitabu au magazeti. Ukienda kwa nchi kama Kenya, Uganda hawana ushuru wa karatasi za kuchapisia magazeti, karatasi za kuchapia vitabu.

Sasa nikawa nadhani kwamba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, angewasiliana na Waziri wa Fedha waone uwezekano wa kuondoa ushuru wa karatasi ili iwe nafuu kwa kuchapa vitabu na magazeti ili tupate hizi habari mpaka vijijini.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine naelekeza kwenye michezo. Michezo yote tuliyonayo hivi sasa duniani inatoka katika nchi za wenzetu za Ulaya na Marekani. Sasa nadhani pia tuna haja ya kuangalia ni michezo ya asili iendelezwe. Tunaweza kuiendeleza tukajikuta pia tunakuwa na michezo miwili mitatu kwenye dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, majuzi tu mimi nilikuwa nafanya kama mzaha, *nili-draft* mchezo mdogo unaitwa *The Limbo*, nikachora chora nikaingiza kwenye *computer* nikawapelekea wataalam huko lakini wamenijibu wamesema ni mchezo mzuri unaitwa *The Limbo*. Kwa hiyo, nahofu kwamba si mbali sana tunaweza kuwa na huo mchezo. Chimbuko lake litakuwa ni kutoka nchi za dunia ya tatu ambayo ni Tanzania.

Kwa hiyo, naomba nitoe taarifa katika Bunge lako Tukufu kwamba tayari nimeshauandika huo mchezo unaitwa *The Limbo*, Limbo ni mkono na mguu, kwa hiyo, unaweza ukachezwa. Nimeshau-design.

Kwa hiyo, hii ni hamasa kwamba hata sisi tunaweza tuka-*design* michezo tukaipeleka kwa wenzetu na nimepeleka kuna shirika moja linaitwa *Hard Does* wameomba nipeleke nakala ya pili wanasema nipeleke kanda ya namna unavyochezwa na tayari nimeshaandaa vijana kwa ajili ya kufanya mazoezi ya huo michezo ili nipeleke hiyo kanda. Kwa hiyo, suala linaonekana kama ni utani lakini *serious* kwa sababu nimelifanyia kazi na hii huenda ikawa ni sifa ya nchi yetu kwamba tumegundua michezo unaitwa *The Limbo*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni kazi ndogo tu ni kwamba ni baada ya kazi zingine za Bunge na kadhalika, naaka, naona badala ya kukata mitaa naamua kuandika andika. Kwa hiyo, naomba nisisitize kwamba umuhimu upo wa kuendeleza michezo yetu.

Mheshimiwa Spika, naona nchi yetu imejikita sana kwenye michezo wa mpira. Tumesahau michezo mingine kama *tennis*. Mimi naamini michezo kama *tennis* ni rahisi sana kuliko mpira wa miguu. Mpira wa miguu ni mgumu ukichukulia kwamba ushindani wake ni mkubwa mno. Lakini kama tutaelekeza michezo mingine kama *tennis* tunaweza tukaibua akina Serena Williams wengine hapa hapa Tanzania. Kwa hiyo, basi naomba katika mikataba hii tusisitize pia nchi yetu, kuibua vipaji vyta vijana wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu utamaduni. Kwa kweli hivi sasa tuna dunia moja wanasema dunia imekuwa ni kijiji kikubwa. Kwa maana hiyo, tumeingiliana tamaduni. Kwa hiyo basi, inatakiwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kuwa makini kwa hili kwamba tunaporidhia hii mikataba tuwe makini, tusipokee tamaduni zingine ambazo zinawenza kutupeleka pabaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho ya kuchangia juu ya hoja iliyo mbele yetu.

Kwa kuanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa kumaliza ujenzi wa Daraja la Benjamin William Mkapa la Mto Rufiji. Ni kweli kwamba chama hakijengi daraja, lakini Serikali inaongozwa na Chama ndioyimejenga. Kwa hiyo, kelele zinazotolewa huko kwamba siyo CCM imejenga ni kelele ambazo ni *misdirection*. Ni Serikali za awamu mbili za CCM zimepanga na kutekeleza mpango wa ujenzi wa daraja hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa *interest* anayoonyesha katika utamaduni na michezo katika nchi hii. Yeye tunamjua ni mwana habari mashuhuri na ameonyesha *interest* kubwa sana kwa michezo hata kiasi cha kuweza kuahidi kutupatia *complex* ya michezo kabla hajaondoka madarakani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi wa hii itifaki wakuu wa hizi nchi 14 ambazo zimetia sahihi wametambua wazi katika ukurasa wa pili kwamba michezo ina sehemu kubwa sana katika kuji-*address* kwenye mambo ya kijamii, ya kiuchumi na ya kisiasa katika nchi zetu. Kwa hiyo, michezo siyo ya kufanya lelemama.

Mheshimiwa Spika, ninacho Kitabu cha Sera ya Maendeleo ya Michezo katika nchi yetu. Hiki kitabu kiliandikwa mwaka 1995 na kimesainiwa na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, wakati huo akiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kitabu kinaainisha vizuri sana juu ya Sera ya Michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu juu ya *vision* ya Serikali juu ya umuhimu wa michezo katika jamii yetu, ukurasa wa saba wa Sera ya Maendeleo ya Michezo: “Pamoja na mengine, michezo inatambuliwa kwamba inajenga na kuimarisha afya njema na maisha bora kwa wote, inajenga tabia ya ushirikiano, upendo na undugu na uzalendo, inajenga Taifa lenye nidhamu, inajenga moyo wa kishujaa na kujihami na kukuza ukakamavu” na mengine mengi ambayo yameainishwa kwenye hii sera. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hii sera imemainisha ni nani mwenye jukumu la kutekeleza sera ya michezo katika nchi hii. Ukurasa wa 10 inasema wenyewe majukumu ni Wizara yenyeye dhamana ya maendeleo ya michezo, pamoja na Wizara nyininge mbalimbali. Ukurasa wa 12 Wizara ya Elimu na Utamaduni, inapewa jukumu maalum. Naomba ninukuu kifungu (b): "Wizara ya Elimu itahakikisha kwamba mashindano ya michezo yanayoendesha katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu yanaimarishwa ili yaendelee kuchangia kupata mtaji wa wachezaji bora wa Taifa, pia wenyewe uwezo wa kuendeleza taaluma ya michezo." (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi Serikali katika kutunga sera hii ilikuwa inatambua umuhimu wa michezo katika shule zetu za msingi, za sekondari na kwenye vyuo na kwamba huko ndiko kutatokea chimbuko la wachezaji wa Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka wakati wa michezo wa mpira Tanzania, michezo *Gossage* yale mashindano ya *Gossage*, mashindano ya *Sunlight* na mashindano ya *Taifa Cup*. Wakati ule umekwisha na umekwisha kwa sababu hatusisitizi tena michezo kama tulivyokuwa tunasisitiza zamani. Michezo inaanza tangu utoto, michezo haifunzwi utu uzima. Mimi leo hii siweza kuanza kucheza michezo mpya. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika kujumuisha Mheshimiwa Waziri, atueleze hii sera ambayo ilitungwa na Serikali yenye kwamba shule za msingi, vyuo na nadhalika viwe ndiyo chimbuko na kuwe na haya mashindano ili tuweze kupata wachezaji wa Taifa imekwisha lini ile sera ya kusema kusiwe na mashindano ya vyuo na shule za msingi na sekondari imefanyiwa uamuza ngazi gani katika Taifa, wakati tuna sera maalum ambayo inasema hayo mashindano yawepo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikiendeleza hoja hiyo pia ninayo malalamiko machache. Ni ukweli usiyopingika kwamba michezo wa mpira katika nchi yetu ndiyo michezo mkubwa kuliko yote na inashirikisha watu wengi kuliko yote. Lakini ni jambo pia ambalo haliwezi kupingika kwamba sasa watu wanafunga *Television* kutazama michezo ya mpira nje badala ya kwenda kwenye viwanja vyetu kutazama mpira au kufunga *Television* kutazama michezo ya mpira inachezwa katika nchi yetu. Ni sababu kwamba kama nilivyo sema ile enzi ya Tanzania kutoka kifua mbele kwenye viwanja vya mpira imekwisha. (*Makofî*)

Sasa hivi tunayo malumbano ya *club* na *club*, tunayo malumbano ya viongozi na viongozi, tunayo malumbano ya viongozi na wachezaji, tunayo malumbano ya *club* na Wizara, tunayo malumbano ya kila aina kwenye michezo wa mpira. Serikali imejaribu, imejenga viwanja, inaweka mazingira mazuri katika kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, lakini tukiwaliza watu wanaongoza mpira katika nchi hii watupe sera ya kuendeleza mpira nchi hii hawana hiyo sera. Sasa pamoja na kwamba Rais wetu ametia sahihi itifaki hii, pamoja na kwamba Rais wetu ametambua kwamba kuna umuhimu wa kuwa na *exchange* ya wanamichezo katika hili eneo la *SADC* sisi tutabaki mpaka lini kuwa kichwa cha mwendawazimu? Tukiendelea na haya magomvi hivi na watu ambao wana maslahi binafsi kwenye michezo badala ya maslahi ya Taifa, itakuwa bado hajaitendea haki hii *protocol*. Kwa hiyo, ninashauri kwamba juhudhi zifanyike katika kuondoa ugomvi ulioko katika michezo ili tuweze kuendeleza michezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 6 ya hii *protocol* kuna suala la *mobilization* ya *sports programs*, iko ukurasa wa 8, naomba niisome: "State parties shall mobilize adequate resources for the implementation of programs in the areas of culture, information and sports." Haya ni makubaliano ambayo wakuu wa nchi 14 wameyaweka.

Kwa hiyo, nia ya Serikali ya ku-mobilize resources ipo. Ni wajibu wa vile vyama vya michezo kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba hizi *resources* ambazo zinakuwa *mobilized* ambazo ni kodi zetu zinatumika vizuri kwa faida ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ukurasa wa 9 wa hii *protocol* (e) *article 12*, wana wajibu wa kuhakikisha kwamba utamaduni una *role* kubwa ya ku-play. Tunaomba pia hivi vyama vya michezo navyo vihakikishe kwamba vinaisaidia Serikali siyo kukwamisha Serikali. Juu ya *Regional*

Integration ya Sports na Regional Tournaments Article 24 na 26, naomba nitoe rai kwamba hatuwezi kushiriki kwenye (Regional Tournaments) mashindano ya Kimataifa katika hali tuliyonayo kama vilabu na vyama vya michezo havitatulia na kama havitachukua hatua deliberate kabisa za ku-encourage sports shuleni huko ili tuweze kuwa na wachezaji wazuri baadaye. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, mwisho kuhusiana na hii *protocol* kuna suala la *copyright* ambalo ni hati miliki liko kwenye *culture* kwamba wakuu wa nchi za SADC wanasema kwamba watahakikisha kwamba wanalinda hati miliki, *intellectual property*.

Mheshimiwa Spika, hata sasa hivi tukitoka tukienda barabara za mji wa Dodoma kuna kanda zinazotembea huko za wanamuziki, watu wanafanyabiashara, wanaauza zile kanda, wana muziki wanakuwa wakiwa maskini. Hakuna jitihada yoyote ambayo inafanyika. Natambua kuna sheria ya *copyright* katika nchi hii, sheria ya *intellectual property*, lakini hiyo sheria haijatiliwa umuhimu. Ningombaa ile miziki yetu ya zamani ambayo inauzwa *very freely* na makampuni ya nje tunaomba Serikali ichukue hatua kuwasaidia wale wana muziki wa zamani amba wanakuwa hata vifo ambavyo havijulikani waweze kupata *royalties* kutoka kwenye ile miziki yao. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa wakati nikiunga mkono hii itifaki nina ombi moja kwa Serikali.

Mimi ni mwananchi wa Kunduchi, pale Kunduchi tuna eneo ambalo walifikia Waarabu wa kwanza wa Oman kuna magofu, makaburi, kuna historia kubwa sana pale. Tunaomba Serikali kwa sababu imeshindwa kuya-preserve yale makaburi wananchi wa Kunduchi tunaomba Serikali itukabidhi sisi tuweze kujenga *Museum* na *Library* pale na tuweze ku-preseve ile *area* na ule msikiti ili historia ya Kunduchi isife. Hili ni jambo ambalo pia liko kwenye hii *protocol* katika kuweka mambo ya kale. (Makofî)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, ninasema tena ninaunga mkono hii Itifaki. Ahsante sana. (Makofî)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kukamilisha hoja ya azimio la kuridhia itifaki ya ushirikiano katika masuala ya utamaduni, michezo na habari katika nchi za SADC.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Wamekuwa wachangiaji watano akiwemo Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mbunge wa Magogoni na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika masuala yanayoendana na hoja hii, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa na Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, aliyezungumza hapa mwisho. (Makofî)

Wote nawashukuru sana kwa sababu kila mmoja wao ameunga mkono hoja hii. Wametoa ushauri, mawazo na wameuliza baadhi ya maswali ambayo ningependa kuchukua nafasi hii kuyajibu maadamu yamekwisha tamkwa ni vizuri niyajibu kwa faida ya Bunge hili na pia kwa faida ya nchi. (Makofî)

Namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', katika kuwasilisha maoni ya kamati, ametoa maoni mengi mazuri ambayo nilikwisha kushukuru pia hata tulipokuwa katika kamati waliponipa ushauri.

Napenda nishukuru maoni waliyokuwa nayo kuhusu Chuo cha Utamaduni Bagamoyo ambacho tayari katika Jumuuya ya Afrika Mashariki kimekwishateuliwa kwamba ni *centre of excellency* katika suala la utamaduni. (Makofî)

Nakubaliana na pendelezo lao kwamba tujaribu chuo hiki pia kikubalike katika nchi za SADC. Tutajitahidi kufanya hivyo, kufanya wenzetu wakubali. Ni kweli kabisa wenzetu katika Jumuuya ya Afrika Mashariki wameridhika kwamba ile *approach* ya Chuo cha Bagamoyo ni maalum kwa sababu ina *approach* ya masuala ya utamaduni na fani za sanaa, yana u-*approach* u-Afrika zaidi kuliko kuchukua mambo ya kutoka kutoka nje ya Bara la Afrika. Kwa hiyo, nina hakika na wenzetu katika nchi za SADC tutakapokuwa tumewafahamisha wanaweza wakakubaliana nasi.

Mheshimiwa Spika, alitoa wazo kwamba tuwe na timu ya kudumu ya Taifa, nasema tumesikia na wana michezo wetu na wanaongoza vyama mbalimbali vya michezo nina hakika watazingatia masuala hayo, maana ni kutokana na changamoto za namna hii tunachukua hatua mbalimbali. Ningependa kwa ujumla niseme mawazo ya kamati tunayapokea.

Niende kwenye baadhi ya mambo ambayo yamesemwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, namshukuru sana kwa hatua yake ya kuamua kuunga mkono mambo yanapokuwa hayana utata, sisi upande wa Serikali tunafurahia sana kama wenzetu katika Kambi ya Upinzani wanayaona hivyo hasa mambo yanayohusu maslahi ya Taifa kwa ujumla.

Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, katika hatua ya kwanza naleta Azimio hapa anaunga mkono, inashiria kwamba tutaendelea kushirkiana vizuri katika masuala yanayotuhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuimarisha kijiji cha michezo. Napenda nimhakikishie kwamba si kwamba vinatushinda. Uchumi wetu umekuwa na matatizo mbalimbali, lakini katika miaka ya hivi karibuni hali yetu ya uchumi imezidi kuwa nzuri kutokana na mambo mawili makubwa.

Kwanza ufanisi wa ukusanyaji wa kodi umeongezeka na matokeo sasa tunakusanya zaidi ya hizo bilioni 100 kwa mwezi kwa hiyo, Serikali ina uweza wa kufanya mambo makubwa zaidi.

Kwa hiyo, Serikali ina uwezo wa kufanya mambo makubwa zaidi. Lakini la pili kwa hatua za baadaye ni kwamba tumefikisha sasa uchumi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa mara ya kwanza katika nchi yetu uchumi wetu unakua kwa zaidi ya mara mbili ya ongezeko la watu.

Hii ni mara ya kwanza tangu tumepata uhuru. Kwa hiyo, kwa kweli tunastahili kumpongeza Rais wetu na tunastahili kujipongeza sisi wote tunaohusika na jambo hili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, katika Bajeti tumekwishaanza kuweka makisio ya kurekebisha na kukarabati vyuo hivi ambavyo vilikuwa vimesahauliwa kwa miaka mingi. Naomba wenzetu katika Kambi ya Upinzani, wajitahidi kuyaona mabadiliko yanayofanyika.

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amesema hapa tunachofanya ni kupitisha tu (*ku-rubber stamp*) mimi nadhani tufike mahali sisi kama Wabunge tuelewane vizuri kidogo nini tunachofanya, tunapopitisha maazimio haya ya *ku-ratify* mikataba ambayo imekwisha kuwekwa sahihi.

Mimi napenda nimsamehe Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, kwa sababu ni mgeni hapa Bungeni, kwa hiyo, inabidi ajifunze, tupeane maelezo hapa. Wakati mwininge ndani ya Bunge humu ni kama tunapeana Semina, ni kujifunza. Kitu kimoja ambacho lazima tujifunze ni kwamba huwezi *ku-ratify* Mkataba ambaa haujawekwa sahihi.

Katika taratibu zetu, tumesema kwamba Mikataba itawekwa sahihi na kisha italetwa Bungeni kwa ajili ya kufanya *ratification*. Mkataba kama haujawekwa sahihi, huwezi ukazungumzia *ratification*. Kwa hiyo, kuna hatua kwa hatua katika kufanya mambo. Kwa hiyo, lile jukumu ambalo Bunge hili limepewa la kuidhinisha ile Mikataba, ni suala la kuidhinisha. Ni lazima tufahamu kwamba tumekubaliana ndani ya Katiba kwamba Katiba yetu ina mafiga matatu na kila figa lina kazi yake. Kuna *Executive* kwa maana ya (sijui tafsiri yake sahihi), Serikali tendaji au dola, ina kazi zake za kufanya. Ni Mamlaka ya Utawala, labda pengine kwa lugha sahihi. Mamlaka ya Utawala ina kazi zake za kufanya ambazo ni pamoja na kujadiliana Mikataba hiyo na nchi nyingine na kuikamilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge ni figa la pili, ni chombo cha kutunga sheria na sasa kimepewa mamlaka ya utawala. Ikishaingia kwenye Mikataba, Bunge nalo lije hapa litoe idhini yake, lifanye *ratification*. Chombo cha tatu, ni Mahakama ambayo sheria tunazozitunga hao wa kwenye Mahakama watakwendwa kuzitumia wanapohukumu kesi mbalimbali na kufanya maamuzi mbalimbali ya kimahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa napenda mwenzetu Msemaji Mkuu kutoka Kambi ya Upinzani, aelewé kwamba hizi ndizo taratibu. Kwa hiyo, suala la kuletwa hapa kufanya *ratification* liko ndani ya utaratibu ulio sahihi na asitegemee hata siku moja kwamba utaletwa Mkataba hapa Bungeni kufanyiwa *ratification* kabla haujawekwa sahihi kwa sababu, hiyo itakuwa ni lugha tofauti.

Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, amezungumzia suala la habari kwamba tungezingatia hata katika kuitisha, kuleta hii hoja hapa Bungeni. Amedai kwamba tumeshtukiza, tumeileta katika hatua za mwisho.

Napenda nimkumbushe Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwamba *document* hii kwa maana ya kufika katika Bunge hili, hajaja kwa kasi anayoizungumzia. Nimesema nilipokuwa nawasilisha hoja hii kwamba Itifaki hii ilikwishazungumzwa na Kamati ya Bunge tarehe 24 Julai, 2003. Imezungumzwa na Kamati ya Bunge, tumeijadili, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, alikuwepo kwenye hicho Kikao tulipojadili, hawesi akaja leo akasema anashtukizwa hapa kaiona leo, kwa sababu tulikuwa naye katika Kamati na muhtasari upo.

Mheshimiwa Spika, nadhani alijua ndivyo nitakavyojibu, naona taratibu, ameepuka, asiwemo Bungeni ninapotoa maelezo. Tulishirikiana naye, hoja alizotoa tulizijibu. Labda aliamua tu afanye *political point* lakini humu Bungeni ni vizuri tukafahamu kwamba kila unalolisema kuna mwenzako atakuja kulitolea maelezo. Kwa hiyo, ni vizuri mtu unaposema ujue lililo la maelezo, ni afadhali usiliseme. Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, nina hakika kabisa amekuwa na *document* hii na Itifaki hii pamoja na Azimio hili tangu tarehe 24 Julai, 2003. Kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba tumeshtukiza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, amezungumzia kwamba ingefaa tuwe na *Access to Information Act*. Mimi napenda nimkumbushe Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwamba ni kazi ya Bunge kutunga sheria na Bunge katika kutunga sheria sio lazima lisubiri Serikali. Kama Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, anadhani tunahitaji kuwa na sheria nyingine aliyoita *Access to Information Act*, basi anaweza akalileta wazo hilo. Anaweza akaleta Muswada wake tukatazama jambo hilo. Lakini napenda nimkumbushe kwamba ziko Sheria kadhaa ambazo zimetungwa na Bunge hili kusimamia mambo hayo hayo anayozungumzia kwamba tuyaweke katika hiyo *Access to Information Act*.

Nikumbushe kwa haraka kwamba kwanza tunayoSheria ya Habari, pia ziko Kanuni za kudumu za masuala ya habari, kuna Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976, kuna Sheria ya Utangazaji ya mwaka 1993 (*Tanzania Broadcasting Services Act*) na kuna Sheria inayoitwa *Tanzania Communication Act*. Sheria zote zinakwenda sambamba pamoja na Sheria za Usalama na Siri za Serikali. Lakini masuala ya *Access to Information Act* yote yanazungumziwa katika sheria hizo.

Kwa hiyo, napenda ajue, lakini kama anaiona kasoro bado ipo, tuwe na *Access to Information Act* anaweza kutuletea. Lakini ningemshauri kabla hajafanya hivyo, asome kwanza hizo Sheria zilizopo anaweza akakuta zinatosheleza.

Pia, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, amezungumzia umuhimu wa *information infrastructure*, hata humu Bungeni kwamba pengine na Waandishi wetu wa Habari hawana vyombo vyamitandao, lakini mimi nikitazama kule naona wengine wamekaa na *laptop* zinafanya kazi kabisa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, nadhani alivyotazama kule hakuviona, lakini mimi naona *laptop* kabisa iko pale inafanya kazi. Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakaona pia. Ningependa nimkumbushe Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwamba anapozungumzia mambo ya leo, akumbuke tulikotoka.

Mimi nimekuwepo katika Bunge hili tangu mwaka 1970, hatukuwa na mfumo wa *information* kama ambao tunao sasa wa utoaji wa habari. Nina hakika hivi ninavyozungumza hapa inawezekana Waheshimiwa Wabunge wengine walioko hata katika *Restaurant* na mahali pengine wanania na kizungumza kwa njia ya vyombo vyamitandao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze sana wewe na Wasaidizi wako kwamba tunaiiona jitihada ya siku hadi siku kuongeza masuala ya kulifanya Bunge hili liwasiliane vizuri na wananchi wake.

Napenda pia niwafahamishe wenzetu wa Kambi ya Upinzani kwamba Serikali inaendelea na juhudzi ya kuboresha mawasiliiano katika nchi na Mheshimiwa Waziri anayesimamia masuala ya Habari na Utangazaji ametuambia hapa Bungeni kwamba ifikapo mwaka 2004 na mwaka 2004 ni mwaka kesho, TTV itaonekana nchi nzima kila kona ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua kubwa sana. Miaka michache iliyopita wengine tulikuwa tunafikiri hatutaona jambo la *television* nchi nzima. Leo *television* itaonekana nchi nzima itakapofika mwaka 2004. Masuala ya kuimarisha *infrastructure* ya mambo ya michezo, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, ameitangazia nchi hii kwamba kabla hajaondoka anataka kutuacha tuna *Utra Modern Stadium*. (*Makofi*)

Napenda niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba kila juhudzi inafanywa na kwa utekelezaji unaendelea ukisimamiwa na mwenzetu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, utekelezaji unakwenda sambamba na ahadi hiyo aliyoitoa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Muttamwega Mgaya, ametuambia kwamba ameandika michezo unaithwa sijui *The Limbo*, haya kama ameandika kweli na tutuona unakwenda Kimataifa. Mheshimiwa Muttamwega Mgaya, sisi tunakupa hongera. Mtu yejote ambaye anatumia muda wake kufanya mambo ya utunzi, itasaidia sana. Waheshimiwa Wabunge maeneo mbalimbali tunakotoka kuna historia za maeneo hayo. Ninachopenda kuwataarifu tu ni kwamba tunalo Shirika sasa linalosimamia masuala haya ya utamaduni na niliwaambia hapa na nadhani waligawa na vielelezo vyao ambaa wanaweza wakatoa. Kama utafiti wako unaendana na masuala ya utamaduni wetu, unaweza ukapata *funding* kutoka katika chombo hicho, Shirika lililo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Muttamwega Mgaya, amesema pia kuhusu michezo kwamba pengine tungekazana zaidi tuwe na akina Serena Williams. Ningependa kusema kwamba katika Itifaki hii tunazungumzia mambo mawili, *Centre of Excellence* na *Centre of Talent*. Hizi zote ni juhudzi zetu katika nchi za SADC za pamoja za kuweza kuwa na utaratibu na Vituo vya kunoa wanafani wetu na wanamichezo wetu katika utaalamu wao wa masuala ya michezo. Kwa hiyo, kwa kweli Itifaki hii inaendana na mawazo haya aliyojasema.

Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwa kutukumbusha kuhusu yaliyomo katika Sera ya Michezo na wajibu ambaa Wizara ya Elimu na Utamaduni, imepewa. Ameuliza kuhusu suala la mashindano ya michezo ya shule, ametusomea hapa kwamba yamo katika sera hiyo na mimi nakubaliana naye. Ninachotaka kufafanua tu ni kwamba si sahihi kusema michezo shulenii imekatazwa. Si sahihi hata kidogo na wala sio sahihi kusema mashindano ya michezo ya shule, ziwe za Msingi, ziwe za Sekondari, viwe Vyuo yamekatazwa, sio sahihi hata kidogo. Waziri ninayesimamia masuala haya ni mimi hapa ninayezungumza. Labda watu wanachanganya juu ya mambo niliyoyarekebisha kuhusu jambo hili la michezo shulenii.

Napenda nirudie tena, kilichokuwa kinafanyika, yalikuwepo Mashirika yameundwa ndani ya Sheria ya Michezo. Shirika moja lilikuwa linaitwa UMITASHUMTA, lina kirefu chake. Kulikuwa na Shirika kwa ajili ya Shule za Sekondari linaitwa UMISETA. Tatizo ni kwamba, ukichukua UMITASHUMTA, limeundwa chini ya Sheria ya Michezo, Sheria ya Michezo sasa haisimamiwi na Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa sababu suala la *sports development* katika nchi haliko chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Hapo zamani yalikuwa pamoja.

Sasa hivi ipo Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo. Lile neno maendeleo, sio maendeleo ya Vijana tu, Maendeleo ya Vijana na Maendeleo ya Michezo katika nchi. Hili jukumu halipo tena mikononi mwa Waziri wa Elimu na utamaduni. Mheshimiwa Rais aliliondoa jukumu hilo kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni, akalipeleka kwenye Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, lakini bado Waziri wa Elimu anao wajibu wa michezo shulenii.

Mheshimiwa Spika, michezo shulenii ni sehemu ya *curriculum*, ni sehemu ya mitaala ya elimu katika shule za msingi, shule za sekondari na vyuo. Mashirika ya UMITASHUMTA na UMISETA na

lingine hilo la vyuo mimi nimeyafuta katika shule kwa sababu kwanza shule zinaendeshwa kwa kufuata sheria ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuyafuta Mashirika hayo, sijasema michezo isifanyike shulen i kwa sababu ningekuwa najipinga mwenyewe na *curriculum* ninayotakiwa kusimamia katika shule na sijasema mashindano ya shule za msingi yasifanywe. Ila maagizo yaliyotolewa na Wizara ni kwamba yanapofanywa mashindano, yasiingilie zile siku 194 zilizopangwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa ajili ya kufundisha *syllabus*. Afisa Elimu Kiongozi amepanga siku 194 na amechukua *syllabus* ya kila somo na kuipangia utaratibu wa kufundisha *syllabus* yote ifundishwe, inahitaji siku 194.

Mheshimiwa Spika, kilichokuwa kinatokea wakati wa Mashirika hayo ya UMITASHUMTA na UMISETA walikuwa wanaweza wakaondoka wanafunzi na Walimu wao mpaka siku 60 wanakwenda kufanya mashindano ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. Ukijumlahisha siku 60 katika siku 194, wanafunzi wale walikuwa hawako madarasani kujifunza na Walimu walikuwa hawako madarasani kufundisha. Walikuwa wanasema watawafundisha huko waliko wale wanafunzi waliokwenda nao. Lakini katika hali ya uhaba wa Walimu, bado wanafunzi wapo waliofeli waende Kidato cha Kwanza. Leo mjadala mkubwa hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wanaoniona ni suala la watoto waliofaulu mtihani wa darasa la saba kukosa nafasi za kwenda sekondari. Hayo ni matokeo ya maamuzi kuondoa maeneo ambayo tulikuwa tunaona mlolongo wetu au mfumo wa utoaji wetu wa elimu ulikuwa unavuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi napenda niseme kwamba hatua hizi ambazo nililazimika kuzichukua, matokeo yake yameanza kuonekana kwa matokeo ya mitihani, watoto wetu wanaofaulu ni wengi zaidi. Miaka michache katika Bunge hili tulikuwa tunajadiliana namna Waziri aruhusu watoto waliofeli waende Kidato cha Kwanza. Leo mjadala mkubwa hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wanaoniona ni suala la watoto waliofaulu mtihani wa darasa la saba kukosa nafasi za kwenda sekondari. Hayo ni matokeo ya maamuzi kuondoa maeneo ambayo tulikuwa tunaona mlolongo wetu au mfumo wa utoaji wetu wa elimu ulikuwa unavuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado narudia kusema, michezo shulen tutaendelea kuimarisha na shule za msingi, sekondari na vyuo, nasema hapa Bungeni, naingia kwenye *record* ya *Hansard*, zinaruhusiwa kushindana, kuendesha mashindano, yapangwe na *Head Teachers, Head Masters* na wasimamiaji wao ilimradi tu zisiingiliwe siku 194 za kujifunza na kufundishwa madarasani kama ilivyopangwa na Afisa Elimu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu jambo hili limeleweka na kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, tulikuwa na mashindano ya *Goss age* tulikuwa na mashindano ya *Sunlight Cup* na mimi nilipokuwa nasoma *Tabora School* nilikuwa naona wenzangu wanaondoka kwenda kwenye mashindano ya *Sunlight Cup* na wengine wanachaguliwa wakiwemo shulen i wanakwenda kwenye Timu ya *Gossage* ya Tanganyika kucheza na Timu ya Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, mashindano haya ya kuacha masomo yalikuwa hayapo. Ni kwamba wanaoanda Timu walikuwa wanaangalia ama shule wanaposhindana kwa mabweni yao, ama shule kama pale *Tabora School* na shule ya *Saint Mary's* aliposoma Mheshimiwa Edward Lowassa, zinaposhindana, wale wapangaji wa Timu ya *Sunlight* waliwaona wachezaji wazuri walioko *Tabora School* akina Marehemu Yahya Mwakitosi na wachezaji wazuri walioko *Saint Mary's* wakawachagua wakawaweka kwenye Timu ya Mkoa wa Tabora. Walipokwenda kucheza Dar es Salaam waliwaona akina Yunge Mwanasali, ingawaje bado wanasma ni wachezaji wazuri wakaingia kuchezea Timu ya Tanganyika ya *Gossage*. Kwa hiyo, utaratibu huu bado unawezekana kufanywa hata kama hatuna mlolongo wa kutoa wanafunzi shulen i kwa muda wa siku 60 waje washindane Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kusema, tutaendelea kuzungumza na Waziri mwenzangu mwenye jukumu la Maendeleo ya Vijana na Michezo, tuone namna tunavyoweza kuwa na linkage ya mashindano ya shule zetu na uundaji wa Timu za Mikoa na Timu za Wilaya na Timu za Vilabu tuwe na linkage ya namna gani ambayo haiingilii utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, amesema hakuna sera ya kuendeleza mpira wa miguu. Haipo! Sina uhakika juu ya jambo hili, sijapata ushauri wa kutosha. Lakini kama haipo ni vizuri ikawepo Ni ushauri mzuri. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, Itifaki hii inalenga kunoa ujuzi na kuwa na Vituo nya kuweza kunoa ujuzi. Nakubaliana naye kwamba katika Ibara ya Sita ukurasa wa nane, Wakuu wa Nchi wamekubaliana kufanya *mobilization* ya *resources*.

Napenda kusema kwamba Wakuu wa Nchi wakishakubaliana na sisi Wabunge tukaja hapa tukaridhia Itifaki hiyo ya makubaliano ya Wakuu wa Nchi, basi moja kwa moja sisi ambao ndio tunaosimamia *resources* katika nchi zetu ndio watekelezaji wa makubaliano hayo kwa kuhakikisha tunapanga *resources* za kutosha kama walivyoji-*commit* Wakuu wa Nchi zetu.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, ametoa maombi maalum kuhusu eneo la Kunduchi, eneo linalohusu masuala ya mambo ya kale. Nimemsikia amesema kuna Msikiti wa miaka mingi sana pale, tuwakabidhi, wauboreshe. Mimi kwa niaba ya Waziri mwenzangu anayesimamia masuala haya ya Mambo ya Kale, nafahamu miaka ya nyuma masuala ya Mambo ya Kale na Nyaraka za Kale yote yalikuwa Wizara ya Elimu, sasa hivi masuala ya Mambo ya Kale yako Wizara ya Maliasili na Utalii na masuala ya Nyaraka za Kale yako Idara Kuu ya Utumishi.

Mimi nimebakwa na Utamaduni kwa maana ya sindimba na ngoma nyingine za aina hiyo. (*Kicheko/Makofî*)

Lakini Mawaziri wenzangu wamesikia na napenda niseme kabisa kwamba, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, asikate tamaa, Serikali yake ya CCM imemsikia anachosema, nina hakika tutafuatilia jambo hili tuone namna ya kuliingiza, msianze kuitishiana michango na nini, tuone namna Idara yetu wanavyoweza kuandaa kitu kizima kinachoweza kusimamiwa Kiserikali. Nawashukuru sana kwa michango mizuri sana iliyotolewa hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Kuridhia Utamaduni, Habari na Michezo liliridhiwa na Bunge*)

SPIKA: Mheshimiwa Mto Hoja, utaratibu tuliofanya ni kwamba kama Waziri ana maazimio mawili ya kuwasilisha, basi anayawasilisha moja baada ya jingine ili yawewe kujadiliwa kwa pamoja. Sasa namwita Mto Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. (*Makofî*)

Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Afrika
(*Amendments to the Constitutive Act of the African Union*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Dharura wa Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanya Februari, 2002 mwaka huu huko Addis Ababa, Ethiopia, marekebisho kadhaa yalifanya katika Katiba ya Umoja wa Afrika. Mkutano huo uliitishwa kufuatia uamuzi uliofanya tarehe 09 Julai na Wakuu wa Nchi katika Kikao chao cha Durban mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika marekebisho hayo shabaha za msingi zilikuwa zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuleta usawa kijinsia kwa kuondoa hisia ya utawala wa mfumo dume katika lugha ya Katiba ya Umoja wa Afrika. Kwa sababu hiyo basi, neno *founding fathers* limerekebishwa na kuwa *founders* ili isionekane wanaume tu peke yao. (*Kicheko/Makofî*)

Kadhalika, kila mahali ambapo limeandikwa neon *Chairman* wamerekebisha na kuwa *Chairperson*. Natumaini mabingwa wa lugha ya Kiingereza na Waingereza wenyewe wataelewa hisia za Kiafrika za kimapinduzi kwa sababu kwa Kiingereza tulichofundishwa ni *Mr. Chairman, Madam Chairman*, Waingereza wenyewe hawajababilisha, lakini sisi Afrika tumeweka msimamo huo. (*Makofsi*)

Pili, kusisitiza nafasi ya wanawake katika Umoja wa Afrika kwa kuongeza Ibara ya Tatu ya madhumuniaya ndogo ya tatu (i) isemayo: "Kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki kwa ukamilifu kwenye kufanya maamuzi hasa katika maeneo ya siasa, uchumi, utamaduni na kijamii." (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, msingi wa tatu katika marekebiso haya ni kuwezesha Bara letu kushirikiana na Waafrika waishio nje ya Afrika na watu wenyewe asili ya Afrika popote walipo duniani yaani *the Africans in the Diaspora*. Wapo Waafrika wenzetu amba o wanaishi Ulaya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wako watu amba o wana asili ya Kiafrika amba o wanaishi nje ya Afrika. Nchi kama Brazil ukiacha Nigeria, Brazil ndiyo ya pili yenye watu wengi weusi, maana pale wapo milioni 60. Kwa hiyo, wako wengi sana watu amba o wana asili ya Kiafrika.

Sasa kilichofanyika kwenye Mikataba hii ni kuwapa nafasi maalum yenye kuwatambua kwamba wapo na kutengeneza msingi wa namna ya kushirikiana nao. Madhumuni makubwa hapa ni namna gani tunaweza kuitumia nguvu yao hii kubwa kwa maendeleo ya Arika. Wana uwezo wa kifedha, wana uwezo wa kitaalam na tumeambiwa wakati mwininge, wengine hata wanachangia *lobby* ya Kiyahudi kwa sababu hakuna *forum* maalum ya kuchangia *lobby* ya Afrika. Kwa hiyo basi, katika madhumuni kumeongezwa aya ya tatu, 3.0 inayokaribisha na kuhimiza ushiriki wa Waafrika au watu wenyewe asili ya Kiafrika waishio nje ya Bara letu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika imeongezwa aya ya tatu. Hii inahimiza ushirikiano katika masuala ya ulinzi na mambo ya nje mionganii mwa Mataifa ya Afrika. Katika Ibara ya Nne ya Kanuni kimeongezwa kipengele kipyaa kinachozuia nchi za Kiafrika kuingia Mikataba na Mataifa ya kigeni kwa mambo ambayo yatapingana ama yatatofautiana na maslahi ya Umoja wa Afrika. Wenzetu wengine wanaweza kuingia Mikataba ambayo inaweza kwa kweli isiwe kwa *interests* za Afrika. Kwa hiyo, imewekwa kabisa, kwamba nchi mwanachama isiingie kwenye *treaty* yoyote ambayo ita-affect maslahi ya Afrika au maslahi ya nchi nydingine jirani.

Kwa ajili ya kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa Bara hili linakuwa eneo la usalama na amani katika Mkutano wa Durban, Wakuu wa Nchi na Serikali waliunda Baraza la Amani na Usalama. Hivyo, Baraza hilo sasa limetamkwa rasmi katika Katiba na ni moja ya marekebiso yanayoletwa kuridhiwa.

Kwa upande wa Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali, yapo mabadiliko ya msingi yaliyofanywa. Kwanza yamempa Mwenyekiti uwezo wa kuitisha vikao vya dharura. Katiba ya sasa haina. Inazungumzia tu nchi wanachama wakifikia theluthi mbili wanaweza kuitisha Mkutano wa dharura, lakini sasa inampa Mamlaka hayo pia Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kama kuna jambo la dharura afanye uamuzi huo. Ata-consult nchi wanachama halafu anaweza kuitisha Mkutano huo.

La pili ni kumwezesha Mwenyekiti aliyepo kuendelea kwa kipindi kisichozidi kimoja zaidi katika mazingira ya dharura. Wakati mmoja ilikuwa ufanyike Mkutano wa *Organization of African Unity*, Tripoli - Libya. Kukawa na matatizo ya wakubwa kuingilia kati kutaka watu wasiende. Kwa hiyo, Mkutano ukawa na misukosuko kweli. Mnakumbuka wakati ule sisi ndio kwanza tumetoka kwenye vita tu ya Uganda na Libya ilikuwa ni moja ya nchi tuliyopigana nayo pale. Lakini Mwalimu alikwenda kwa kusema pamoja na tofauti tulizokuwa nazo na Libya, lakini tutakwenda kwa sababu hapa suala kubwa ni Umoja wa Afrika.

Baada ya Mkutano ule kushindikana, ikabidi Rais Daniel arap Moi wa Kenya, aendelee kwa kipindi kilichofuata, lakini aliendelea kienyeji. Sasa inawekwa kabisa kwenye Katiba kwamba iwapo kutatokea mazingira ya dharura, kiongozi ambaye hivi sasa ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika anaweza kuendelea kwa kipindi kimoja zaidi. Kipindi kisichozidi kimoja. Wapo watu wanaopenda iwe miaka miwili na wapo amba o wamekuwa wanashauri kwamba iachwe wazi tu na kwamba anaweza kuendelea zaidi. Hata hivyo, ikaonekana kwamba iwe *restricted* kwa kipindi kimoja.

Jambo lingine la tatu ni kutamkwa rasmi kuwepo Kamati ya kumsaidia Mwenyekiti kuendesha vikao yaani pale kunakuwa na *Bureau*. *Bureau* hiyo imetamkwa rasmi safari hii kwenye Katiba. Imekuwepo huko nyuma kwa maelewano, lakini sasa ipo kwenye Katiba yenewe ya Umoja wa Afrika. Halafu la nne, ni kuwa umewekwa utaratibu wa kumpata Mwenyekiti iwapo vitafanyika kwenye Makao Makuu ya *African Union*. Kwa sababu ya mazoea kama nchi mwanachama inawaalika wenzake kuja katika Mkutano, nchi ile Mwanachama ndiyo inayokuwa Mwenyekiti. Tumekubaliana katika Katiba hii kwamba kila baada ya Mikutano miwili, mmoja lazima ufanyike Makao Makuu Addis Ababa. Je, ukifanyika pale Addis Ababa, utaratibu wa kumpata Mwenyekiti unakuwa vipi? Imetamkwa kwamba utakuwa utaratibu kwa nchi kuomba, lakini utakuwa pia ni kwa msingi wa *geographical rotation*. Kama safari hii itakuwa ni *West Africa* basi safari ijayo inaweza ikawa *East Africa*, iingie *North Africa* na kadhalika na hiyo ndio imetamkwa.

Kadhalika marekebisho yameweka wazi uhusiano wa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na Mwenyekiti wa *Commission* na pia uhusiano wa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na Asasi mbalimbali za *Commission* ambapo inampa mamlaka ya kuweza kuziitisha Asasi zile kufanya Mikutano. Kuhusu Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri, naye imeelekezwa kuwa atasaidiwa na Kamati itakayochaguliwa na Baraza hilo. Katika marekebisho haya pia, lugha ya Kiswahili na Kihispania imeongezwa na kuwa lugha rasmi pamoja na Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu. (*Makofsi*)

Uamuzi huo ulifanywa Durban mwaka 2002, lakini uamuzi ulifanywa hauwezi kutumika bila ya kuingizwa rasmi kwenye Katiba yenewe ya Umoja wa Afrika kwa hiyo moja au mionganoni mwa marekebisho yaliyofanywa ni kuingiza rasmi Kiswahili kwenye Katiba ili iweze kuwa ni lugha rasmi itakayotumika. Pia imeelezwa kwamba Baraza litakuwa linatengeneza utaratibu wa namna ya lugha hizo zitakavyokuwa zinatumika.

Pia imeongezwa Ibara ya 30 inayohusu nchi kusimamishwa uanachama iwapo itaruhusu ardhii yake kutumika kwa uchochezi dhidi ya nchi nyingine. Maana wapo wengine wanaweza kuwa wanageuzeu nchi zao kuwa Kituo cha uchochezi na kuhujumu nchi dhidi ya nyingine.

Kwa sasa, kama mwanachama akigundulika ana tabia hizi, Katiba iko kimya, lakini kuanzia sasa kwa maana ya marekebisho haya baadhi ya nchi za wenzetu zilikuwa zinafanya vituko ndani ya nchi nyingine, zingeweza hata kusimamishwa kwa kwenda kinyume na Katiba ya *OAU*. Imewekwa hivyo kwa kweli kujaribu kuzuia mazingira yaliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la marekebisho haya ni kuimarisha Umoja wa Afrika huu mpya na asasi zake kwa kuzifanya ziwe na nguvu zaidi, Tanzania itanufaika na marekebisho hayo.

Kwa kuzingatia umuhimu na manufaa tutakayopapat kwa kuridhia marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Afrika, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakubali Bunge letu Tukufu liliridhie marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Afrika. Sasa naomba kusoma Azimio la Kuridhia:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Afrika baada ya kutia saini Katiba ya Umoja wa Afrika Mjini Lome Togo, Julai 11, 2000 na kuridhia Katiba hiyo Aprili 6, 2002;

NA KWA KUWA nchi wanachama chini ya Ibara ya 32 wanaweza kuleta mapendekezo ya ama kufanya marekebisho au kuboresha Katiba;

NA KWA KUWA nchi wanachama walileta mapendekezo ya kurekebisha Katiba ya Umoja wa Afrika kwenye Kikao cha Kwanza cha Wakuu wa Nchi na Serikali kilichofanyika Mjini Durban, Afrika ya Kusini Julai, 2002;

NA KWA KUWA kikao hicho kilikuwa ndiyo kwanza kinazindua Umoja wa Afrika na kisingemudu kwa wakati mfupi kuzungumzia marekebisho hayo;

NA KWA KUWA Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali kiliamua kifanyike Kikao Maalum cha dharura cha Baraza la Mawaziri na Wakuu wa Nchi kujadili marekebisho hayo na kuondoa hali ya marekebisho ya mara kwa mara;

NA KWA KUWA Kikao kisichokuwa cha kikawaida cha Baraza la Mawaziri kilikutana Mjini Tripoli Libya, Desemba 9 mpaka 10, 2002 kuzungumzia marekebisho hayo kwa mara ya kwanza;

NA KWA KUWA Kamati Maalum ya kujadili marekebisho hayo ilikutana Mjini *Sun City*, Afrika Kusini na kuweza kujadiliana kwa kina mapendekezo ya kurekebisha Ibara sita za Katiba;

NA KWA KUWA suala la kurekebisha lilitifikisha tena kwenye Kikao kisichokuwa cha kawaida cha Baraza la Mawaziri Mjini Addis Ababa tarehe 1 Februari ili kuitisha mapendekezo hayo kabla hayajaenda kwenye Kikao cha Dharura cha Wakuu wa Nchi na Serikali tarehe 2 Februari, 2003 kwa uamuzi;

NA KWA KUWA Kikao hiki cha Mawaziri na Wakuu wa Nchi kilijadili mapendekezo yote kwa kirefu na hususan hili la lugha kikiwemo Kiswahili;

NA KWA KUWA hatimaye kikao kilikubaliana kupata muafaka kuwa lugha ya Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika zitakuwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika;

NA KWA KUWA Tanzania imeshiriki kwa ukamilifu kwenye mjadala wote wa kuleta marekebisho muhimu kwenye Katiba ya Umoja wa Afrika;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa marekebisho hayo kwa Tanzania na Bara letu la Afrika, Bunge hili Tukufu katika Mkutano wake wa Kumi na Mbili sasa linaazimia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kuridhia mapendekezo ya marekebishi ya Katiba ya Umoja wa Afrika (*Amendments to The Constitutive Act of African Union*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuiliwe)
**Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza la Amani
na Usalama la Umoja wa Afrika (Protocol Relating to the
Establishment of the Peace and Security Council
of the African Union)**

WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba katika Kikao cha kawaida cha Umoja wa Afrika kilichofanyika Mjini Durban Afrika Kusini tarehe 9 Julai, 2002 Wakuu wa Nchi na Serikali walipitisha Itifaki ya kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alikuwa miiongoni mwa Viongozi wa kwanza kutia saini Itifaki hiyo. Nadhani alikuwa wa tatu. (*Makofii*)

Katika kuitisha Itifaki ya kuanzishwa kwa Baraza hilo ililazimika kufanya marekebishi kwenye Katiba ya Umoja huo ili kuingiza Asasi hii kama ilivyo kwenye maelezo yangu kuhusu mapendekezo ya marekebishi ya Katiba ya Umoja wa Afrika. Asasi hii imeingizwa katika Ibara ya tano ya Katiba ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Tanzania ilishiriki kwa ukamilifu kwenye mjadala wa kuitisha Itifaki ya kuanzishwa kwa Baraza la Amani la Umoja wa Afrika hasa tukitambua kwamba chombo cha awali cha Umoja wa Nchi Huru za Afrika kilichojulikana kwa *Organ for Conflicts Prevention Management and Resolution* kilikuwa kimepitwa na wakati na hivyo kilihitajika chombo bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya tatu ya Itifaki hii inaainisha madhumuni ya kuanzishwa kwa Baraza hili na kwamba jukumu lake kuu litakuwa chombo kitakachotoa maamuzi ya uzuiaji, usimamizi na usuluhisho wa migogoro kama ifuatavyo:-

Kwanza, Baraza litadumisha amani, usalama na utulivu Barazani Afrika ili kuhakikisha kinga na hifadhi kwa watu na mali zao, mazingira yao pamoja na kutengeneza mazingira yanayoleta maendeleo endelevu yaani *sustainable development*.

Pili, Baraza linatarajiwa kuzuia na kusuluhisha migogoro kwenye maeneo ambayo migogoro au vita imeshazuka na tatu, inatakiwa kuendeleza na kutekeleza ujenzi wa amani na kurejesha shughuli zile zilizokuwa zinaendelea kabla ya kuzuka vita au migogoro, *post conflicts reconstruction*.

Mheshimiwa Spika, nne, Baraza pia litaratibu na kuainisha juhudzi za Bara la Afrika katika kuzuia na kupambana na ugaidi katika nyanja zote kwa kuunda sera moja ya ulinzi kwa ajili ya Umoja wa Afrika na mwisho, litahimiza na kukuza demokrasia, utawala bora, utawala wa sheria, kulinda haki za binadamu na haki za msingi na uhuru.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 inaelezea kuundwa na majukumu ya Jeshi la Akiba la Afrika ili kutekeleza majukumu ya Baraza katika kusambaza vikundi vyta amani vya kusaidia kuleta amani Afrika. Ni dhahiri kuwa Itifaki hii ikiridhiwa na kutekelezwa na nchi wanachama, amani na usalama miiongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika itakuzwa na hasa sasa ambapo migogoro imejaa tele.

Mheshimiwa Spika hitimisho, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa tukayoyapata kwa kuridhia Itifaki ya kuanzishwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakubali Bunge liridhie Itifaki husika.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kusoma Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Afrika baada ya kuridhia Katiba ya Umoja huo tarehe 6 Aprili, 2002;

NA KWA KUWA Tanzania ilishiriki kwa ukamilifu kwenye mjadala wa kuitisha Itifaki ya kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwenye Kikao cha Kwanza cha kawaida cha Wakuu wa Nchi na Serikali Mjini Durban Afrika ya Kusini tarehe 9 Julai, 2002;

NA KWA KUWA kwa kuanzishwa Baraza hili Afrika itakuwa na chombo mahususi cha kutoa maamuzi juu ya uzuiaji, usimamizi na usuluhisho wa migogoro;

NA KWA KUWA Baraza litadumisha amani, usalama na utulivu Barani Afrika ili kuhakikishia wananchi kinga na hifadhi kwa maisha na mali zao;

NA KWA KUWA Baraza linatarajiwa kuzuia na kusuluhisha migogoro kwenye maeneo ambapo migogoro imekwishazuka;

NA KWA KUWA Baraza litaendeleza na kutekeleza ujenzi wa amani na kurejesha shughuli zilizokuwa zinaendelea kabla ya kuzuka kwa vita au migogoro;

NA KWA KUWA Baraza litaratibu na kudumisha juhudzi za Bara la Afrika katika kuzuia na kupambana na Ugaidi katika nyanja zote kwa kuunda Sera moja ya ulinzi;

NA KWA KUWA Baraza litatimiza na kukuza demokrasia, utawala bora na utawala wa Sheria kulinda haki za binadamu na misingi ya uhuru;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Ibara ya 22(3) ya Itifaki kila mwanachama wa Umoja wa Afrika analazimika kuridhia Itifaki hii kabla ya kuanza kutumika;

NA KWA KUWA Tanzania inatambua na kuona umuhimu wa kuridhia Itifaki hii kwa kuzingatia ukweli kwamba Baraza hili litakuwa chombo kikuu cha kutatua migogoro ambayo imezuka na kupashana habari kwa haraka zaidi katika kuzuia migogoro ambayo inaweza kutokea Barani Afrika;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Itifaki hii kwa Tanzania na mipango yote ya kulinda amani na usalama inayotokana na Baraza hili, Bunge lako Tukufu katika Mkutano wake wa kumi na mbili sasa linaazimia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kuridhia Itifaki ya kuanzishwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. USSI YAHAYA HAJI (k.n.y. MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu ili nami niwapongeze kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wapya hususan wale wa Chama Cha Mapinduzi na wengineo kwa kuchaguliwa kwao na kuijunga na Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Sir George Kahama na familia yake kwa kuondokewa na mtoto wao mpendwa. Nawaomba wawe na subira kwa msiba huo nzito. Tunamwombea marehemu Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 96(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje kuhusu maazimio ya kuridhia mikataba iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Maazimio hayo ni kama ifuatavyo:-

La kwanza ni Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Afrika (*Amendment to the Constitutive Act of African Union*).

La pili, ni Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza la Amani la Usalama la Umoja wa Afrika (*Protocol Relating to the Establishment of Peace and Security Council of the African Union*).

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba maazimio haya mawili yanafanana kwa kuwa yanahuusu hatua zinazochukuliwa kuimarisha Katiba na kuunda Asasi za Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu azimio la Bunge kuridhia marekebisho ya Katiba ya Afrika, maeleo na sababu zilizotolewa ni sahihi kwa kuwa zinifuata Katiba ya Umoja wa Afrika ambayo katika Ibara ya 32 ya Katiba inatoa utaratibu kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la marekebisho hayo, ni kuimarisha chombo husika Kamati inakubaliana na hatua hii ya Wizara, Serikali na Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifurahishwa na marekebisho katika Ibara ya tatu ambapo moja ya madhumuni ni kukaribisha na kuhimiza ushiriki kikamilifu Waafrika waliotawanyika ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, kutambua hali hii ni kuheshimu historia ya Mwfrika na kuikabili hali halisi ya dunia ambapo Mwfrika bado anahitaji mshikamano mkubwa zaidi kwa maendeleo yake katika mtandao wa dunia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Azimio la kutaka kuunda Baraza la Usalama kwa kuingiza asasi hii kwenye Katiba ni kujibu matakwa ya hali halisi ya nchi za Afrika ambapo migogoro lazima isuluhihwe na

Waafrika wenyewe. Aidha, hii ni kutambua kwamba kuwapo kwa hali ya amani na usalama ndiyo kutatoa nafasi ya Mwfrika kutekeleza mipango ya maendeleo na kwa mashirikiano zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo Kamati yangu inakubaliana na umuhimu na ulazima kwa Tanzania kuridhia mikataba hii na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Itifaki hizi mbili kwa maazimio ya Bunge yaliyopendekezwa.

Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya kuanzishwa kwa Baraza la Amani la Usalama la Umoja wa Afrika na Azimio la Kuridhia marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, pamoja na kukubali Mikataba hii iridhiwe na Bunge lako Tukufu kwa kuzingatia umuhimu wake kwa Taifa letu Kamati inatao ushauri ufuatao:-

Kwanza, Serikali iangalie na kuimarisha usalama wa ndani ya nchi yetu kwa kuwa hali iliyopo sasa siyo mzuri sana kiusalama kutowana na kuzagaa kwa wakimbizi nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika uhusishe juhudzi za pamoja za kukabiliana na ugaidi wa kimataifa kwa kuwa ndiyo tishio kwa sasa na athari zake kiuchumi ni kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, kwa kutanzua migogoro mbalimbali ndani ya nchi, utekelezaji wa mkataba huu ufanyike kwa umakini ili isikiuke uhuru wa nchi wanachama kujiamulia mambo yake na kuheshimu mipaka kwa mujibu wa Azimio la Cairo. Kuingilia migogoro ya nchi kufanyike tu baada ya nchi wanachama kujadiliana na kukubaliana kwa kauli moja.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama zibuni mbinu ili ziweze kudhibiti watawala wa nchi ambao kwa makusudi na pasipo sababu za msingi wanavunja amani na kuvuruga utawala wa kidemokrasia ndani ya nchi zao wenyewe na majirani zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni ya Kamati naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kuridhia mikataba kutowana na umuhimu wake kwa Watanzania na jamii nzima ya Kiafrika.

Aidha, naipongeza Serikali kwa kuleta maazimio haya katika muda muafaka mbele ya Bunge lako Tukufu ili yaweze kuridhiwa na kufanya nchi yetu kwenda sambamba na nchi nyingine za Afrika kama mukutano wa Wakuu wa Nchi uliofanyika Maputo Msumbiji tarehe 10 mpaka 12 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kama walivyofanya wenzangu na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nitoe maoni machache juu ya Maazimio haya mawili yaliyoletwala na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Napenda nianze kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nipongeze juhudzi kubwa zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa, pamoja na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake katika majukwaa mbalimbali ya kimataifa kama watetezi wazuri sio wa nchi yetu tu lakini wa Bara letu zima la Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya tatu inahusu madhumuni, hata kabla ya kuwafikiria Waafrika waliotawanyika, Umoja wa Afrika unatakiwa kumaliza matatizo makubwa yanayowakabili Waafrika walio ndani ya Afrika sasa hivi ambao kimsingi ni maskini sana. Migogoro ya nchi mbalimbali katika Bara letu

hili kama vile Burundi, Rwanda, DRC, Uganda, Sudan, Egypt, Algeria, Senegal na Liberia, Ivory Coast na nyinginezo ni muhimu itatuliwe kwanza, kwa wazee wa Afrika waliotawanyika kote duniani si jambo bayila ni lazima vipaumbele vya Serikali viwepo sawasawa.

Mheshimiwa Spika, uundwaji wa Baraza la Usalama, katika Ibara ya tano ya Asasi za Umoja, ni wakati muafaka sasa wa kulifufua wazo la mmoja wa waasisi wa AU, Marehemu Dr. Kwame Nkrumah, ambaye alipigania sio tu kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa ya Afrika yaani *United States of Africa*, bali pia kuanzishwa kwa *Command* moja ya kijeshi kwa Afrika nzima.

Mahitaji ya fedha ili kukwepa tatizo la Umoja wa Afrika kukosa kabisa fedha za matumizi ya siku hadi siku mbali ya maendeleo ni lazima Umoja huo uhakikishe unajitegemea kimapato. Umoja huu hautakiwi kuwa na kazi ya kuhamasisha uombaji wa pamoja yaani (*collective begging*) kwa wafadhilli ndani na nje ya Tanzania. Ni lazima Waafrika wenyewe wagharimie Umoja wao badala ya kutegemea watu wengine.

Mheshimiwa Spika, kati ya lugha sita za kufanya kazi katika *Africa Union*, Kiswahili kipo na hakina mpinzani yeyote mkubwa. Ni lazima juhudhi kubwa zifanyike zikiongozwa na Tanzania, Kenya na Uganda. Lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu ya kuimarisha Umoja na mshikamano kwa Waafrika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi nziri zilizopo za kuanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Afrika (*African Economic Community*) kupitia Umoja wa Afrika, ni lazima kujihadhari na mataifa makubwa ya Magharibi na vyombo vya fedha za Kimataifa hasa Benki ya Dunia na IMF, kwani kupitia kile kinachoitwa NEPAD mataifa hayo na vyombo hivyo, wanadai kuisaidia Afrika kujikomboa kiuchumi. Ileweke wazi kwamba kukomboka kiuchumi kwa Bara la Afrika kunaweza kumaanisha kuanguka kwa uchumi wa Mataifa ya kibepari.

Mgawanyo wa Kimataifa wa kazi za kibeberu unataka Afrika iendelee kupeleka malighafi katika nchi za kibebesi zilizoendelea na iendelee kuwa soko la bidhaa za viwandani za Mataifa yaliyoendelea kiviwanda.

Mheshimiwa Spika, Mwandishi maarufu aitwaye Oswad Rivelio, ambaye ni Mwanadiplomasia maarufu kutoka Peru, anaandika katika kitabu chake *kiitwacho The Myth of Development* cha mwaka 2001 kwamba leo hii IMF na Benki ya Dunia wamejitwalia nguvu kubwa za kimataifa yaani *Supranational Powers* zinazoviwezesha vyombo hivyo kuamsha na kusimamia, kuamrisha na kusimamia Sera za Kiuchumi za nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, hakuna wasi wasi kwamba wakubwa wa nchi za Magharibi wamewahi kuhujumu ukombozi wa kiuchumi wa Afrika kwa namna mbalimbali. Uchumi nzuri wa Ghana wakati wa kilele cha utawala wa Kwame Nkrumah, ambao ulitokana zaidi na uzalishaji wa Kokoa ulihujumiwa makusudi ili kumkomoa Kwame Nkrumah na wazo lake la Umoja wa Afrika. Kwa kipindi cha kati ya mwaka 1960 hadi 1965 bei ya Kokoa ililazimishwa na wakubwa hawa kushuka kutoka *pound 480* kwa tani kwa mwaka 1962 hadi *pound 60* mwaka 1965.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Januari mwaka 1999 Gazeti la Uingereza *The Times* katika makala yake nzito kuhusu Afrika lilikiri kwamba Ghana ya Kwame Nkrumah, ililazimishwa kuperomoka kiuchumi kwa kuangusha kimakusudi soko la Kokoa yake.

Mheshimiwa Spika, hakuna cha kushangaa kuona kwamba Shirika la kijasusi la Kimarekani (*CIA*) lilichekelea kama sio kudhamini mapinduzi ya kijeshi yaliyomwondo Kwame Nkrumah, madarakani mwaka 1966. Ni muhimu Afrika kuwa makini na aina ya usaidizi wa kiuchumi unaotokana na wakubwa hawa.

Mheshimiwa Spika, aidha kuhusu azimio la kutaka kuunda Baraza la Usalama yaani *Protocol Relating to the Establishment of Peace and Security of the African Union*.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kambi ya Upinzani haina tatizo hata kidogo na Azimio hili na lile la kwanza. Kwa sababu umuhimu wake unajulikana. Isipokuwa lazima utekelezaji wake uangaliwe kwa

karibu ili wale wenye nguvu wasipate fursa ya kuwaonea wanyonge. Pamoja na nia njema ya azimio hili, lakini kwa kuwa katika utekelezaji wake itabidi liundwe jeshi la kutunza huo usalama na amani kwa hiyo Kambi ya Upinzani inapendekeza Bunge hili kupata maelezo juu ya jinsi fedha za gharama hizo zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninamatka tena mara ya pili kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa niaba yangu binafsi kuwa tunaunga mkono kuridhiwa kwa maazimio mawili haya kwa asilimia moja. Nakushukuru sana. (*Makofî*)

SPIKA: Ninae msemaji mmoja kwa Azimio la kwanza, marekebisho ya Katiba ya Umoja wa Afrika. Ni Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, nampa nafasi, ninaye msemaji mmoja kwa azimio la pili, naye ni Mheshimiwa Jackson Makwetta, ajiandae.

MHE. DR. BATILDA S. BURIAN: Mheshimiwa Spika, mimi kwa heshima na taadhima naomba kukupongeza na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia azimio hili.

Kwanza kabisa naomba nimpongeze Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa niaba ya nchi yetu kuweza kuwasilisha Azimio hili. Kwani marekebisho haya ni ya muhimu sana. Mimi nitapenda tu kuchangia katika maeneo matatu ambayo marekebisho haya yanazungumzia.

Eneo la kwanza ni nafasi ya wanawake yaani umuhimu wa kuingiza kipengele kinachozingatia uwakilishi yaani uwakilishi wa wanawake na kuwawezesha wanawake waweze kushiriki katika masuala mbalimbali ya kisiasa, ya kiuchumi na ya kijamii na kuiwezesha kwamba Afrika iwe na uwakilishi sawia kijinsia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kusema kweli Umoja wa Afrika umekuwa ni umoja wa mfano kwa sababu sidhani kama kuna Umoja wowote ambao unazingatia usawa wa kijinsia kwa asilimia 50 kwa 50 kama inavyofanya katika Umoja wa Afrika hasa katika Makamishna waliochaguliwa. (*Makofî*)

Kwa hiyo, naomba nipongeze sana na kweli tuna wajibu wa kujivunia sisi kama Waafrika kwamba Afrika ndiyo chimbuko la haki na usawa wa binadamu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linajieleza dhahiri hapa ni kwa jinsi ya kulizingatia masuala ya kijinsia na ile lugha, lugha ambayo inatumika sasa hivi. Nimefurahi kuona kwamba lugha imerekebishwa kuweza kukidhi matakwa ya kijinsia. Kwa mfano kama Mwenyekiti, sasa hivi tunasema *Chairperson*.

Kwa hiyo, lugha yenewe pia imebadilika ili kuweza kuonyesha kwamba wanawake na wanaume wote kwa pamoja wana haki sawa katika kuleta maendeleo katika Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nitakalolizungumzia hapa ni lugha na hasa lugha ya Kiswahili. Ningombaa Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala haya ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na nchi yetu kwa ujumla kuhakikisha kwamba tunachukua fursa hii kuweza kuona kwamba Kiswahili kinatumika. Tuweze kushirikiana na wenzetu wa nchi za jirani kama Jumuia ya Afrika ya Mashariki na hata kuititia *SADC* kuweza kuimarisha ili basi katika level ya Umoja wa Afrika Kiswahili kiweze kikapata nafasi ya kweli kutumika kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa utaratibu uliopo sasa hivi ni kwamba nchi ile ambayo inapendekeza lugha itakayotumika itabidi wao wafanye usahili wa kuweza kuwa wakalimani. Utaratibu huu unaweza ukafanya kwamba nchi ambayo haina uwezo au hatutawenza kupata wafadhili wa kuweza kuchangia kuweza watu watakaotafsiri zile lugha zingine itashindikana kwa Kiswahili kutumika katika maeneo mengi na katika mikutano mingi. Kwa hiyo, naomba kipengele hiki cha lugha ya Kiswahili kiweze kikatiliwa maanani sana na kikazingatiwa kwa dhati kabisa.

Suala lingine la mwisho ninalopenda kuzungumzia hapa ni uhusiano wa Mwenyekiti na *Commission*. Kusema kweli hapo nyuma mtu akizungumzia Umoja wa Afrika na mwengine anaoma kwamba Umoja wa Afrika na *NEPAD* ni vitu viwili tofauti. Mtazamo huo hauwezi ukafanya Afrika

ukaendelea. Kwa sababu *NEPAD* ni chombo ambacho kimewezesha Umoja wa Afrika kutekeleza programu zake na miradi yake mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu uliokuwa ukionekana kama kuna mgawanyiko wakati Mwenyekiti anashughulika na *Commission* inayoshughulikia *NEPAD* na Mwenyekiti anayeshughulikia Umoja wa Afrika utakwisha kutokana na huu uwezo wa Mwenyekiti sasa kuwa na uhusiano wa karibu kabisa na kuweza kuzisimamia hizi *Commission* pamoja na asasi zingine zilizoko chini ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba na mimi naungana na wenzangu kwa dhati kabisa kuunga mkono hoja ya kuridhia marekebisho ya Katiba ya Afrika. Nashukuru sana. (*Makofsi*)

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Azimio la kuunda Baraza la Amani na Usalama la Afrika. Hapa niongezee machache tu katika hilo moja ni kwamba Bara la Afrika, ni Bara ambalo linaleta aibu katika Karne hii ya 21, ni Bara maskini kupita mabara mengine yote katika ulimwengu, ni Bara ambalo lina hali ya juu sana ya watu kutokujua kusoma na kuandika, ni Bara ambalo linaongoza kwa magonjwa na hasa ugonjwa wa Ukimwi na hofu ya dunia ni kwamba kama hakutakuwa na njia ya kuzuia kasi hii ya kuenea kwa Ukimwi baada ya miaka 10 Bara la Afrika litakuwa na watu wachache kuliko ilivyo hivi sasa.

Kwa hiyo, jitihada za kufanya Maazimio muhimu kama haya hazitakuwa na maana kwa Bara ambalo litakuwa halina watu, haitakuwa na maana. Kwa hiyo, moja ya mambo ya kufanya ili Maazimio kama haya yawe na maana ni kupambana kwanza na umaskini.

Mheshimiwa Spika, hakuna fahari katika umaskini na hakuna Taifa lililo na wajibu kwa kutufundisha sisi Waafrika *nobody else as a leaving* kwamba atabaki tumebweteka pale na kubaki tunaombomba tu. Hakuna aliye na wajibu huo. Tunaishi katika dunia ya wenye nguvu wapishe, dunia ya uchoyo, dunia ya mashindano. Kwa hiyo, ni vizuri Maazimio kama haya yaambatane na mikakati ya namna ya kudumisha uhuru wetu kama Waafrika.

Mheshimiwa Spika, utumwa ndiyo uliotueneza katika dunia, tumetapakaa kila mahali na kila mahali ukiangalia mimi wakati nikitembelea hizi nchi za Ulaya napata aibu sana. Maana unakuta kwenye viwanda nya kuzalisha mali wako wazungu, lakini kwenye maduka maduka na huduma hizi za kuuza uza vitu kwenye *Super Markets* ndiko tuko sisi. Hatuko kwenye uzalishaji, wenyewe wametuacha huko tu kwenye maeneo ya kuzalisha wametuondoa maana wanatujua sisi tunapenda mambo ya starehe, starehe tu na kazi hizi nyepesi nyepesi.

Kwa hiyo, nasema hili Bara wakati fulani wakati ule wa miaka kwenye karne ya 19 walisema ni Bara la giza. Kwa sababu ilikuwa halijulikani huko Ulaya, lakini sasa ni Bara la balaa. Asubuhi ukiangalia kwenye *television* unajifunza kuua, watu wanauana kama wanyama tu. Ukienda huko Ulaya neno Afrika ni *normous* na *mass butchering* na kuuwana uwana ndiyo sifa ya Afrika. Kwa kweli hii ni aibu. Sijui tutaondoaje aibu hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba Azimio hili labda ungeweza kusema kwa Kiingereza *It is dawn in Africa*, kwamba tunaanza kuona nuru sasa, tunaanza kuelewa umuhimu wa kuishi ndiyo maana tuna *come up* na Maazimio kama haya. *Lets pray and hope* kwamba *it is dawn* na kweli *it is dawn* vingineyo kila siku mikutano Dar es Salaam badala ya kuelekeza nguvu zetu na fedha kidogo kumwendeleza Mwaafrika zinaelekezwa kununua bunduki na kuuana na kusababisha njaa badala ya kutumia brains zetu kufanya mambo ya maana ni kutafuta vikao nya amani na *endless meetings* kwa sababu ya mambo kama hayo.

Kwa hiyo, mimi nimesimama kusema kwamba huenda Kwame Nkurumah, aliona mbali mno lakini nadhani sasa maneno ya Kwame Nkurumah, yanaoanwa na Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Kwame Nkurumah alikuwa ametazamwa kama ni mwota ndoto mchana maana yeche aliisema, tuamue sasa hivi tuwe na Serikali moja ya Bara la Afrika, kuwe na *President* mmoja na wengine wawe ni *Ma-Vice President*. Ikaonekana hapa ni ndoto ambazo Kwame Nkurumah, haoni

maana hatu Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alisema aah, tuanze hatua kwa hatua, Kwame Nkurumah, akasema tukianza hatua kwa hatua watu wakionja utamu wa Uhuru watakataa tena kupanua mawazo ya kujenga Afrika moja.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mtu akiishakuwa Rais anapigiwa saluti, mara Bendera na pia anapigiwa mizinga halafu umwambie tuungane anauliza, tukiungana nani atakuwa Rais?

Kwa hiyo, unakuta nalo hili ni tatizo katika Bara la Afrika, tumeungana sasa kila mmoja anabaki ku-*defence* eneo dogo tu. Tazama Tanzania na Zanzibar haya matatizo ni *part individuals* tu, watu wa kawaida wamejaa pale Makambako au Njombe huko ukwambie kwamba leo tutengane Tanganyika na Zanzibar atakuelewa?

Mheshimiwa Spika, *individuals* wanaweza kuja hapa wakasema maneno ya ovyo ovyo kwamba tutengane, ametumwa na nani? Watu wamejaa kule wanafanya kazi, wako Mwanza, Shinyanga wala hawaelewi lakini kuna watu hapa *for person hands* wana *preach* vitu vya ajabu ajabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kwame Nkurumah alisema: “*Neocolonialism is the highest stage of imperialism* na kwamba *neocolonialism was a back door colonialism.*”

Wakubwa wameondoka kwa mlango huu wa mbele lakini wamerudi kwa mlango wa nyuma ambapo wanatunyonya bila madaraka sasa tunabaki na Bendera yetu wenyewe, nembo yetu wenyewe, wimbo wetu wa Taifa na pia Makao Makuu yapo hapa hapa lakini uchumi ndio wanaoamua uendeshwe namna gani na hakuna Uhuru kamili wa nchi bila Uhuru wa kiuchumi. Sasa hili ndiyo tatizo letu kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kwame Nkurumah wakati ule alisema kwamba wenzake watafute kwanza uhuru wa kisiasa na mambo mengine yangetuata, kwa leo kama angekuwa hai bila shaka angesema kwamba taftuteni kwanza uhuru wa kiuchumi na mengine yote yatafuata. Ningedhani hiyo ndiyo ingekuwa simu, moto na ndiyo wimbo wa wakati huu tunapozungumzia Bara la Afrika ambalo sasa linaanza kuona nuru na ambapo ndiyo Bara lenye madikteta, lenye umaskini wa kupindukia, ujinga wa kupindukia, linalonyonywa kwa kupindukia na hata kuanza kutawaliwa tena kwa ujanja tu kwa mlango wa nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la lugha naunga mkono. Nadhani ni wazo zuri. Lakini kama alivyosema mwenzangu kwamba kwa Tanzania sasa hivi Kiswahili ndiyo *Lingua Franca*, ndiyo lugha ya kila mtu na kila Mswahili. Mahali pengine lugha za makabilo zimeanza kufa labda zinatumwa kwenye matambiko tu kwa sababu miungu yetu inasikia lugha ya kienyeji lakini kwa maana ya kuzungumza mbele ya wenzako watu wanakushangaa au hata ukiuliza kabila la mtu leo hii watu wanakushangaa. Njia nzuri ya kujua kabila la mtu ni kuuliza hivi, wewe unatokea Wilaya gani? Ukiuliza namna hiyo atakwambia na utaweza kubuni ni kabila fulani, lakini kwa lengo gani?

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba kwa leo lugha ya Kiswahili huna haja ya kuhangai na lugha hii, imekwishajichimbia na kinajiedesha yenye na hakuna nguvu zitakazozua lugha ya Kiswahili isiendelee. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa suala la msingi kama alivyowahi kusema Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, hapa kwamba ni kujifunza lugha itakayotusaidia kuchanganyika na wenzetu. Namna ya kuiba maarifa katika dunia huibi kwa Kiswahili, kompyuta bado mambo yake yako kwenye lugha moja ya Kiingereza. Isimaanishe kwamba tujitenge tuwe Kisiwa, hapana, tuimarishe kiswahili pamoja na lugha hiyo ambayo itatusaidia kuchota maarifa ya dunia bila hivyo tutakaa na tutabaki maskini milele, lugha sasa siyo mali ya mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa hadithi kwamba kule nyumbani kwetu kuna jamaa mmoja ambaye mtoto wake amefeli mtihani wa darasa wa saba, wazazi wakiondoka asubuhi kwenda kazini wakirudi wanamkuta amekaa pale pale walipomwacha asubuhi, wanapomwuliza vipi anasema baba sina kazi, siku nyingine ikabidi wamfundishe namna ya kuiba kwamba hata kuiba tu unashindwa. Hata kuiba kunahitaji akili, mjinga hawezi kwenda kuiba akafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema ya kwamba katika dunia ya sasa siyo ya wezi lakini ni dunia ya wajanja hii kwa kweli ni lazima tuanze kubadilika, hatuwezi tukabaki tu, siyo kusali tu lakini wakati mwingine umaskini huu nao ni matatizo kwamba katika hali ya umaskini, *opportunism* inakuwa ni *order of the day*. Watu maskini wanaishi kwa kuuwana wenyewe, kumalizana wenyewe, *capacity* ya *self distraction* katika hali ya umaskini ni *very high*. Sasa napenda kusema kwamba *our biggest enemy is poverty* haya mengine yanatokea kwa sababu ya ku-*justify* namna ya kupata mkate.

Mheshimiwa Spika, Macha Veri aliwahi kusema katika maandishi yake kwamba: “*The end justifies the means*,” yaani usijali njia unayotumia kupata kitu jali unakipata unachokitaka. Hii njia katika mazingira ya sasa ni ngumu lakini ndiyo utaratibu unaotumika sasa na wakubwa, *the end justifies the means*, usijali unataka kufika kwa Mheshimiwa Spika pale, unaweza ukaruka hapa katikati kwenye viti hapa mradi unafika kule siyo kupita njia za pembeni hizo ambazo ni ndefu na zinachukua muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuunga mkono na kupongeza Azimio hili kwamba *it is dawning in Africa*. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, naunga mkono na ninapongeza Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Marehemu Bob Marley, aliyejikuwa mwimbaji maarufu miaka 25 iliyopita aliimba wimbo wa *Africa Unite*, hakukosea. Kwa mfano, tukiangalia tatizo la hivi karibuni la Liberia wananchi walikuwa wakikimbia wakisema, ooh, *US* njoo, *US* njoo. Waafrika sisi na Umoja wetu tulionao hatukuweza kufanya jambo lolote mpaka *US* na Umoja wa Mataifa walipoingia. Kwa kweli umoja huu ni muhimu sana, ni wajibu wetu tuuridhie na tuukubali na tuunge mkono. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maneno aliyosema Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwamba Afrika itaendelea kupeleka malighafi nchi za kibeberu, maneno haya si mazuri kwa sababu wahenga wanasema: “Bora kufa, kuliko kufariki” yaani tukae na malighafi ziozeane humu au bora tuziuze ili tupate hela? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Waafrika tuwe na umoja, upendo, amani na utulivu. Afrika kwa miaka mingi inaitwa *Dark Continent* kwa sababu Vijiji vingi bado havina umeme. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu utaisaidia mpaka Zanzibar kuleta amani. Zanzibar ilikuwa kweli ina vurugu kipindi kilichopita lakini kuna msemo unasema kwamba: “*We may be small Island but we are not small people.*” (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi sisemi mengi isipokuwa naridhia na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu watano waliochangia humu ndani na mmoja aliyechangia kwa maandishi. Naomba niwatambue, kwanza, Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mwakilishi wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Abdullatif Esmail, kadhalika Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, amechangia kwa maandishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yote waliyyoyasema Waheshimiwa Wabunge wenzangu kusisitiza umuhimu wa Mikataba hii. Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, imeshauri kwamba Serikali iangalie na kuimariswa usalama wa ndani kutokana na kuzagaa kwa wakimbizi na hata kuzagaa kwa bunduki. Waswahili wanasema, wema wetu unatuponza, maana tumefanya wema kuwakaribisha wakimbizi, lakini madhara makubwa tunayapata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani sote ni mashahidi kwamba jitihada kubwa inafanyika lakini katika kushindana na binadamu ambaye ni mwenye akili inakuwa ni kazi ngumu. Lakini kama tulivyoeleza wakati tunawasilisha hoja yetu na alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, jitihada yetu kubwa tunayoifanya hivi sasa ni kuongeza kasi ya kumaliza migogoro ya Burundi ili kwa kweli wakimbizi hawa waweze kurejea makwao haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kadhalika tuna mapendekezo ambayo tumeyafikisha kwenye Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani, (*UNHCR*). Mapendekezo ambayo yakikubaliwa yatafanya marekebisho ya Mkataba ule ili yeweze kutoa uwajibikaji mkubwa zaidi kwa Jumuiya ya Kimataifa kwa sababu kwa Sheria ya sasa mkiimbizi haruhusiwi kutoka kwenye nchi moja kwenda kwenye nchi nyingine tena. Sisi tunasema haya ni makosa lakini nadhani kama marekebisho yakifanya tunaweza tukasambaza mzigo wa kupokea wakimbizi na pengine madhara yake yanaweza kupungua kwa nchi moja inayopokea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wameelekeza kwamba tuimarishe mapambano dhidi ya migogoro ya kivita Afrika. Nadhani jitihada inaendelea hivi sasa. Lakini wametahadharisha ya kwamba katika kufanya yote haya mipaka na uhuru wa nchi uheshimiwe. Hili ni jambo la kweli. Ni kweli kwamba Umoja wa Afrika una mamlaka ya kuingilia kati na hiki ndicho chombo ambacho kinaweza kutumika kuingilia kati lakini itafanya hivyo tu kwa uamuza utakaofanya katika ngazi ya Wakuu wa nchi ama kwa nchi ile inayohusika kuomba. Kama Wakuu wa nchi wakikaa wakiridhika kwamba kwa kweli hali ilivyo inastahili kuingilia kati kama ilivyo kwa Liberia ambapo wamekaa wameona kwamba kwa kweli hatuwezi tukaachilia vurugu na mauaji kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri niliweke sawa hili kwani inaonekana pale Liberia wanaoingilia kati ni Marekani. Marekani mpaka sasa hivi bado, waliokwishafika pale ni Nigeria. Ni nchi za Afrika ya Magharibi ambazo zitafanya kazi yenye ya kuingilia kati pale. Wakubwa wamesema wataleta meli zao pale Bandarini ili ziweze kusaidia kuongeza uzito lakini *hawata-comment troops on the ground*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema kwamba bado ni sisi wenyeve ndiyo tunaoifanya hiyo kazi na mwamko huo upo. Wamefanya hivyo Sierra Leone, walifanya hivyo Liberia mara ya kwanza, wenzetu hao hao wa *West Africa*. Ilifanya hivyo Lesotho wakati wanajeshi pale walipoiasi Serikali na kujitangaza wao madarakani. Afrika ya Kusini, Botswana na Zimbabwe walipeleka Jeshi pale wakawafagia wale Askari, wakakimbilia milimani hatimaye wakasalimu amri. Kwa hiyo, ni mambo ambayo yamekuwa yanafanyaika.

Mheshimiwa Spika, pia Mkataba uangalie viongozi wanaowatesa raia. Nadhani nimekwishalifanunua.

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, ameeleza mambo mengi. Pia kwamba umoja una wajibu wa kutatua migogoro kwanza kabla ya kuwafikiria Waafrika waliotawanyika huko duniani.

Mimi nadhani hatuna sababu ya kungoja. Ni vitu ambavyo tunaweza tukavifanya vyote kwa wakati mmoja. Kwenye Jeshi kuna kitu kinaitwa *concrete activity*, kwamba kuna vitu unavyoweza kuvifanya kwa wakati mmoja kama umepewa amri ya tahadhari. Wakati huo huo wengine wanakwenda kuchukua silaha *armoury* na wengine wanakwenda kufanya matayarisho ya *ration*. Basi baada ya muda ule ukifika kila kitu hukamilika kwa wakati. Usingojee ufanye kimoja baada ya kingine. Haipo sababu yoyote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninachopenda kukisema kikubwa ni kwamba wako *ma-scientists* wengi sana na pia wako watu matajiri sana ambao wana asili ya Kiafrika waliko nje. Nguvu hii bado hatujaitumia, raslimali hii hatujaitumia. Sasa tusingojee mpaka tumemaliza migogoro yote ya Afrika na kila siku unazaliwa mpya. Sijui ni lini tutamaliza hiyo migogoro. Bado haya ni mambo ambayo tunaweza tukayafanya yote kwa wakati mmoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, alisema tufikirie wazo la Dr. Kwame Nkurumah la *joint command* alilolitoa miaka mingi iliyopita. Kila kitu kina wakati, Mwalimu Julius Nyerere, alisema wakati mwingine kwamba ukipika ugali kabla maji hayajachemkahupati ugali mzuri. Kikwere tunaita mabuja, sijui Kiswahili ni nini yaani unapata yale mabonge mabonge. Nadhani sasa wakati umefika na ndiyo

maana ni suala linalozungumzika sasa na taratibu zake ndiyo zinasimamiwa na ufanuzi kamili utatolewa huu. Hivi sasa nafahamu kwamba kuna wenzetu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hawapo lakini nafahamu kuna mikutano na mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara za Ulinzi na majeshi ya nchi zetu juu ya kuunda *African Stand by Force*. Taratibu zimefika katika hatua ya juu nina hakika kwamba pengine kikao kijacho cha Wakuu wa nchi uamuzi utafanyika juu ya kuanzishwa kwa *African Stand by Force*.

Mheshimiwa Spika, suala kwamba Kiswahili kiendelezwe, tunakubaliana. Ushauri huu umetolewa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, amezungumzia pia Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Jackson Makwetta na pia amechangia Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kwa maandishi. Ndiyo dhamira yetu kama tulivyosema tutashirikiana na Wizara zinazohusika na lugha za Serikali zetu zote mbili na pia Taasisi za Luga za sehemu zetu zote mbili za Muungano kwa ajili ya kufanya maandalizi hayo. Ni jambo ambalo tumeamua kulisimamia.

Mheshimiwa Spika, gharama zipo lakini gharama hizo ni za mwanzo kwamba katika miaka miwili ya kwanza zile nchi ambazo zinapendekeza zinagharamia halafu baada ya hapo umoja wenye sasa unachukua na kuendelea nao. Tutaona gharama zenye ni kiasi gani ili kama ni kubwa sana ndiyo tutataka wenzetu tushirikiane nao. Kama ni shilingi bilioni 1.2 mimi nadhani tusijidhalilishe sana kuomba.

Wakati mwingine tunajifanya maskini kwa kitu ambacho tunaweza maana kupanga ni kuchagua tu. Unawenza ukaamua usifanye hiki ili uweze kupata shilingi milioni 800 za kipeleka *Africa Union*, kwa miaka miwili ni shilingi bilioni 1.6 na kiswahili kikaanza. Badala ya kuanza tunapeleka *SADC* ambako watu wanaanza kujadili wanasema na sasa Kizulu nacho kiwemo, sasa mnaanza kuingia mjadala mwingine. Lakini mimi naamini kwamba ni vitu ambavyo tunaviweza. Sasa hivi tunaunda Kamati ya Kitaifa ya kusimamia jambo hilo na baadhi ya watu niliowaomba wanaonekana wako tayari kushiriki kwenye hilo, wamo humu humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, ameelezea kuhusu *IMF* na *World Bank* kuwa *Supranational Powers* ambazo sasa hivi haifanyi kazi ya kuimarisha Ubepari. Lakini mimi napenda kusema kwamba si ushauri wote wa *World Bank* na *IMF* ni mbaya kwa Afrika, kuna ushauri ambao umetusaidia sana. Wakati mwingine wanapotubana kurudi kwenye nidhamu. Wakati mwingine wanatusaidia hasa kurudi kwenye *The Microeconomic Frame*, *IMF* ni hodari sana kwenye haya.

Mheshimiwa Spika, *World Bank* ni hodari sana kwenye *Structural Adjustment Programs*. Programu za kujenga misingi bora ya uchumi. *Okay* wana makosa wanayoyafanya. Si kila kitu kiko sahihi, walikuwa wana *African Development Decide* hapa ya *Kim Jay Cok* haikufika popote na Afrika bado ni maskini. Kwa hiyo, tuniseme kwamba kila chao ni kibaya, wao kama binadamu pia wana upeo wa uwezo wa kutoa ushauri sahihi na wakati mwingine wanaowaleta kushauri ni wanafunzi tu. Mimi napenda kuwapa mfano wa kijana mmoja ambaye ni marehemu sasa hivi, Marehemu Angelus Mrope, alikuwa mfanyakazi wetu kwenye Chuo cha Diplomasia. Alikuwa ni kijana *very bright*. Alikwenda kusoma Marekani *Johns Hopkins School* moja ya Vyuo maarufu Marekani. Akawa anafanya vizuri sana. Kwa hiyo, chuo chenyewe kikampangia kufanya kazi ya muda pale *World Bank*. *World Bank* ndiyo ilikuwa inatumia yule Marehemu Mrope kuongoza *mission* za *World Bank* kwenda Zambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiyo wakati mwingine usidhani kwamba wana wataalam mabingwa sana, ni hawa hawa tu. Unamwuliza Mrope vipi, anasema aah, ninaongoza mission ya *World Bank* kwenda Zambia. Unamwuliza kuna nini huko? Anasema tunaangalia *Restructuring* ya *Civil Service*. Sasa wakati mwingine nao wanazo *limitation* za namna hii katika kufanya haya mambo, kwa hiyo tusidhani kwamba majibu yao yote ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba Azimio hili la *Peace and Security* linaungwa mkono na linatambulika. Kitu kikubwa ambacho ninaweza kusema mimi ni kwamba *we are coming of age*. Huko zamani tulikuwa tunadhani kwamba matatizo yakitokea mahali ni suala la ndani tu, mtu anauwa watu, ana *brutalize* raia au anaonea watu wanasema hayo ni mambo ya ndani ya nchi. Sasa hivi tumetoka kule, tunasemana wazi, tunachukua hatua na mimi nadhani hatua hii tunayokwenda nayo itatusaidia. Kama alivyosema Mheshimiwa Jackson Makwetta, ni jambo la aibu, sasa hivi ukiona zile pitcha zinatisha. Vijana

wadogo wale kazi yao ni kupiga risasi tu, ni aibu kweli lakini tutaondoka huko, tukijenga uwezo huo pengine na watu wataanza kuogopa. (*Makofi*)

Swali limeulizwa kwamba fedha za kugharamia hilo Jeshi ni kiasi gani na tutachangia kiasi gani? Napenda nifafanue vizuri kwamba kwa sababu hivi sasa mazungumzo yanaendelea juu ya *The African Stand by Force*, taratibu zote zitaelezwa na majukumu na wajibu wa kila nchi utafanunuliwa vizuri.

Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, ameipongeza *AU* kwa msimamo wake kuhusu masuala ya wanawake. Mimi nadhani ni jambo sahihi kabisa kwamba Umoja wetu wa Afrika umeonyesha mfano mzuri. Hata wenzetu wakubwa hawajafikia hatua hii kwamba kuna ma-commissioner 10, watano wanawake na watano wanaumé.

Hata lugha ya Malkia tunaifanya marekebisho badala ya *Mr. Chairman, Madam Chairman*, unasema *Chairperson*, mimi nasema hayo ni mapinduzi makubwa. Kwa hiyo, naamini kwamba umoja wetu umepiga hatua kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa yote waliyoyasema. Pia napenda nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwa kutukumbusha kwamba bado *neocolonialism, to the highest stage of capitalism* maana siku hizi watu wanadhani ubepari hakuna, ubeberu haupo ila siku hizi kuna utandawazi tu lakini utandawazi ule upo kushamirisha mfumo wa kipebari. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Azimio la Kuridhia Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika liliridhiwa na Bunge*)

**Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi
za Kusini mwa Afrika ya Kupambana na Rushwa**
(*The SADC Protocol Against Corruption*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kubwa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuliomba kuridhia Itifaki ya Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika (*The Southern African Development Community Protocol Against Corruption*).

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe, ambayo ilipitia na kuichambua Itifaki hii na kutoa ushauri ipasavyo. Chini ya Uenyekiti mahiri wa Mheshimiwa Athumanji Janguo, Kamati ilitoa mapendekezo ambayo kwa mujibu wa Itifaki yenye yana lengo la kuboresha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika tumejifunza mengi kutokana na michango ya wanakamati na ushauri wao utazingatiwa katika kutekeleza Itifaki hii na uboreshaji wake katika wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea kwamba Tanzania ni moja ya nchi zinaunda Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na mwaka huu wa 2003 mwezi huu wa Agosti, Tanzania itakuwa ni Mwenyekiti wa Jumuiya hii ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na ni heshima kubwa kwa nchi yetu kuweza kuongoza umoja huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania ni Mjumbe wa Vyombo vyta Kupambana na Rushwa vya Umoja wa Nchi za Kusini mwa Afrika, *Southern African Forum Against Corruption (SAFAC)*. Mwezi Agosti kuanzia tarehe 4 hadi 7, 2003 Tanzania inakuwa Mwenyekiti wa Umoja huo na mwenyeji wa Mkutano wa mwaka wa Umoja huo unaofanyika Dar es Salaam.

Kwa hiyo, nchi yetu tayari inashirikiana na nchi nyingine katika *SADC* kubuni mbini bora za mashirikiano katika kupambana na rushwa. Ni kwa mantiki hii umoja huu wa nchi za Kusini mwa Afrika ulipitisha Itifaki ya kupambana na rushwa katika eneo hilo ambayo iliwekwa saini na Wakuu wa nchi za umoja huu tarehe 14 Agosti, 2001 nchini Malawi. Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliweka sahihi. (*Makosi*)

Mheshimiwa Spika, rushwa ni tatizo la dunia na ndiyo maana nchi yetu tangu ilipopata uhuru imelichukua tatizo hili kwa uzito wake na Baraza la Mawaziri liliidhinisha mkakati wa Kitaifa dhidi ya rushwa na mpango wa utekelezaji wake kuanzia Novemba, 1999 (*National Anti-corruption Strategy and Action Plan*).

Mheshimiwa Spika, nchi za *SADC* kwa kutambua hili zimejiwekea Itifaki hii ili kuona kuwa rushwa inadhibitiwa katika nchi zetu zote. Madhumuni ya Itifaki hii yametajwa katika Ibara ya pili ya Itifaki yenye kwamba kila nchi ya Umoja wa *SADC* itakuza na kuendeleza mfumo ambao utatumika katika kukinga, kutambua, kuadhibu na kuondoa vitendo vya rushwa katika Sekta ya Umma na ile binafsi.

Mheshimiwa Spika, pili, kukuza na kusaidia kwa kutumia Sheria ya mashirikiano baina ya nchi za umoja huu ili kuhakikisha kwamba upambanaji wa rushwa unakuwa wa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuendeleza na kuunganisha sera na Sheria za nchi za umoja huo kuhusiana na kuzuia, kubaini, kuadhibu na kuondoa rushwa katika Sekta ya Umma na ile ya binafsi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu likiridhia Itifaki hii mambo yafuatayo yatafanyika:-

- (i) Ushirikiano baina ya nchi wanachama katika mapambano dhidi ya rushwa utaimarika.
- (ii) Rushwa itadhibitiwa kwa ushirikiano katika Ukanda huu wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili, lichambue na kisha liazimie kuridhia Itifaki ya Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*The SADC Protocol Against Corruption*) kwa kupitisha Azimio la Bunge kuhusu Tanzania Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya Kupambana na Rushwa yaani (*The SADC Protocol Against Corruption*).

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na inatambua kuwa Utawala Bora ni moja ya nguzo kuu za kuleta maendeleo kwa jamii;

NA KWA KUWA Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika inatambua pia kwamba rushwa ni tatizo ambalo linavunja misingi ya haki za binadamu na kudhoofisha dhana nzima ya Utawala Bora;

NA KWA KUWA lengo kuu kama ilivyoeleza kwenye Ibara ya Pili na Ibara ya Nne ya Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya mwaka 2001 ni kuimarisha ushirikiano mionganii mwa nchi wanachama katika nyanja mbalimbali ikiwemo mapambano dhidi ya rushwa. Hapa napenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika nakala ya Azimio iliyosambazwa Ibara zilizotajwa ni 21 na 22, ni makosa. Ibara sahihi ni Ibara ya pili na Ibara ya nne ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya mwaka 2001;

NA KWA KUWA kwa kuridhia Itifaki hii taratibu za kupambana na rushwa nchini Tanzania zitakua na kuimarika kutokana na ushirikiano baina ya nchi yetu na nchi nyingine wanachama katika kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa vitendo vya rushwa katika sekta za umma na binafsi;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Itifaki hii kwa Taifa letu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa kumi na mbili sasa linaazimia Tanzania kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu vita dhidi ya rushwa yaani (*The SADC Protocol Against Corruption 2001*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofsi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na.70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika Dhidi ya Rushwa (*The SADC Protocol Against Corruption 2001*). Azimio hili liliwasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya hivyo, kwa niaba ya Kamati, napenda kuipongeza Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SADC na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuwa tayari kuwa Mwenyekiti wa Umoja huo kwa kipindi cha mwaka mmoja. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kulisilishi Azimio hili kikamilifu na kutoa maoni yao kama mtoa hoja alivyosema. Kwa kuwa ni jana tu Kamati yangu ilikuwa imetoa mapendekezo kuhusu Itifaki nyingine mbili za SADC, naona nisipoteze muda wa Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwataja Wajumbe hawa. Yatosha tu kusema kwamba, Kamati yangu ina Wajumbe 23 wanaohusisha Chama Tawala cha Mapinduzi na vile vile inawakilishwa na Wajumbe wachache kutoka upande wa Upinzani. Ina wazee pengine wakubwa na wenye busara kuliko Kamati zote na ina vijana na ina Wajumbe wa jinsia zote.

SPIKA: Kazi ya Spika hiyo. (*Kicheko*)

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa umakini aliuonyesha wakati alipokuwa anawasilisha Azimio hili na tulipolijadili katika kubadilishana mawazo na Kamati yangu.

Vile vile napenda niseme kwamba, Kamati hii inahudumiwa na Makatibu wawili, Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ndugu Ernest Zulu. Napenda kuwashukuru sana Makatibu hao kwa kuihudumia Kamati hii vizuri chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Msemembo Mussa, kwa kuiongoza Ofisi yake vizuri. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba, mojawapo ya madhumuni ya Itifaki hii ni kuendeleza na kuunganisha Sera na Sheria za nchi za SADC kuhusiana na kuzuia, kubaini na kuadhibu na kuondoa rushwa katika Sekta ya Umma na ya binafsi. Aidha, tulifahamishwa kwamba, Itifaki hii ikiridhiwa, rushwa itadhibitiwa kwa ushirikiano katika Ukanda wa SADC.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

(i) Kamati yangu imeridhika na sababu zilizotolewa kuonyesha umuhimu wa Tanzania kuridhia Itifaki hii. Aidha, Kamati yangu inaamini kuwa rushwa ni suala ambalo linavuka mipaka ya nchi moja hadi nyingine. Hivyo, udhibiti wake utafanikiwa kama kuna ushirikiano baina ya nchi kadhaa, hasa zenye uhusiano wa kijamii na kiuchumi kama ilivyo katika *SADC*;

(ii) Kamati inaamini kwamba, kushirikiana katika mapambano haya, ni jambo la msingi kwani nchi yetu pekee haitaweza kufanikiwa katika vita hii bila kushirikiana na nchi mbalimbali hasa nchi za jirani kama za *SADC*; na

(iii) Kamati inashauri kuwa katika hili, Serikali iwe na mikakati thabiti ya kuhakikisha kwamba, utekelezaji wake unaleta mafanikio zaidi, nataka nizidishe hapa, mafanikio zaidi katika mapambano dhidi ya rushwa hapa nchini kwetu badala tu ya kuwa kwa manufaa ya wengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kusema kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, haina kipingamizi na Itifaki hii na inaliomba Bunge lako Tukufu liijadili na hatimaye kuiridhia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, kupambana na rushwa hasa mionganoni mwa Watendaji wa Serikali ni sehemu muhimu ya Utawala Bora. Pia inaeleweka kwamba, Utawala Bora ni hitaji muhimu la demokrasia kama ambavyo demokrasia ni hitaji muhimu la maendeleo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *SADC* ni chombo kinachounganisha Mataifa ya Kusini mwa Afrika kiuchumi na kisiasa. Kushamiri kwa rushwa katika nchi moja moja ambazo ni wanachama wa *SADC*, kunazorotesha harakati za uchumi na ufanyaji biashara kwa kuruhusu rafu na michezo michafu. Kwa mfano, kukwepa kodi na ukiukwaji wa kanuni muhimu za ulinzi na usimamizi wa mazingira, rushwa pia inayo nafasi kubwa katika kufukuza wawekezaji wa maana katika eneo zima la nchi za *SADC*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kambi ya Upinzani inaona si jambo baya Tanzania kuridhia Itifaki hii ya kupambana na rushwa mionganoni mwa nchi za *SADC*, ila inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe: Ni lazima kwanza, Tanzania iimarishe zaidi mapambano dhidi ya rushwa ndani ya Tanzania, vita dhidi ya rushwa imezorota mno na imebakia katika ngazi ya Makatibu Kata na Mahakima wa Mahakama za Mwanzo tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa ni sehemu ndogo tu ya mapambano makubwa ya kupigania kuwepo kwa Utawala Bora, pia yanahitajika mapambano makali ya kupigania demokrasia ya kweli ili kuweza kuwa na Utawala Bora. Vita dhidi ya rushwa ni mwanzo wa mapambano ya kidemokrasia na sio tamati ya mapambano haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zipo nchi nyingi katika *SADC* ambazo zina demokrasia ya kiini macho tu na sio demokrasia halisi. Demokrasia ya bandia daima huzaa tawala zisizo bora ikiwa ni pamoja na rushwa, tawala za kibabe, kutowajibika, kukosekana kwa uwazi, matumizi mabovu ya fedha za umma, sera potofu za Serikali, ongezeko la matumizi ya Kijeshi, uharibifu wa mazingira na ajira za upendeleo Serikalini na kadhalika. (*Makofî*)

Kabla ya kuhangainia mambo mazito ya Kimataifa, Tanzania iendelete na kuimarisha elimu ya uraia na elimu ya demokrasia mionganoni mwa Watanzania. Jambo hili litasaidia kuwa na raia wengi wanaojua vema wajibu wao kama raia na wanaozijua vema haki zao za kimsingi za kiuraia. Raia wa aina hiyo si rahisi kupokea wala kutoa rushwa.

Mheshimiwa Spika, nchi za SADC zijitahidi kuwa na sera zenye mwelekeo wa kupunguza umaskini na zifanye kila linalowezekana kuboresha vipato vya watu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ukizingatiwa vema, unayo nafasi kubwa kufutilia mbali rushwa na kuondoa umaskini. Nchi za SADC zikipigania kuwepo kwa demokrasia makini na hilo likiwepo, upo uwezekano mkubwa wa kushinda vita dhidi ya rushwa kwa urahisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kimsingi Kambi ya Upinzani na mimi mwenyewe, tunaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Ninao wasemaji watatu walioomba kuchangia kwa mdomo nao ni Mheshimiwa Adbullatif Esmail, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Semindu K. Pawa. Namwita Mheshimiwa Esmail.

MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, naunga mkono Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuuya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya Kupambana na Rushwa (*The SADC Protocol Against Corruption*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, "rushwa ni adui wa haki", haya ni maneno ya Mwalimu Nyerere, Baba wa Taifa na Waingereza wanasema: "*Corruption is a tree whose branches are of unmeasurable length*". Nampongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa Tanzania kuwa Mwenyekiti mpya wa SADC. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna aina nydingi za rushwa, kuna rushwa ya ngono, unyanyaswaji wa kijinsia, hii haikutajwa katika Mkataba huu, lakini nina hakika itaingizwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Tanzania kuridhia Mkataba huu kwa wakati huu tulionao. Nawakumbusha wale wala rushwa wote kwamba, Wahenga wamesema: "ukila cha mtu na chako kitaliwa"! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Wamarekani wana msemo unaosema: "*When the public is corrupt the laws are broken, when the public is decent the laws are useless*". Naipongeza sana Serikali yetu ya CCM kwa kupiga vita rushwa kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MATOKEO YA KURA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wawili, niliowataja watachangia kipindi cha jioni, kwa hivi sasa napenda kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa asubuhi ya leo. Jumla ya kura zilizopigwa ni 239, ndio Wabunge waliokuwepo Bungeni wakati kura zinapigwa, kura zilizoharibika ni mbili lazima nieleze kwa nini ziliharibika. Kanuni yetu inasema kwamba, kura itahesabiwa kuwa imeharibika ikiwa mpiga kura amepiga kura zaidi au pungufu ya nafasi zilizopo. Sasa kuna wapiga kura wawili walipigia jina moja tu ndio maana zikaharibika.

Sasa matokeo ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo alipata kura 127, Mheshimiwa Monica Mbega alipata kura 128, Mheshimiwa Ruth Msafiri alipata kura 146, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa alipata kura 152 na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji alipata kura 158.

Kwa hiyo, washindi watakaokwenda kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni

(Saa 06.44 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kuhusu Azimio hili ambalo kwa kweli na Wabunge wenzangu waliotangulia wameliunga mkono na mimi naunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mambo yafuatayo, ambayo ningependa kusemea: Kwanza, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenyewe na kushukuru Uongozi wa Tanzania, viongozi wote watatu wa Tanzania kwamba, nchi yetu imeendelea kuwa na amani na Utawala Bora kwa sababu kupokezana kwa madaraka kumekuwa kwa kufuata Katiba na kwa hiari. Tatizo linalotokea sasa hivi katika nchi zetu za Kiafrika ni pale baadhi ya viongozi wanapong'ang'ania kubakia katika madaraka hata kama Katiba zao zenyewe haziruhusu waendelee na matakwa yao binafsi lakini kwetu jambo hili limekuwa na mafanikio makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vile vile ningependa kushauri kwamba, kama utakavyoona kwa mfano, Tanzania alipochukua nafasi Rais Mwinyi kutoka Baba wa Taifa, kilichofuata kizuri aliheshimu uongozi wa mwenzake aliymetangulia na mambo yakaenda vizuri na yeze alipomaliza kipindi chake amekuja Rais Mkapa, naye amemheshimu mwenzake aliymetangulia bila vijembe na kukejeliana na kutafutana roho, mambo yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina matumaini kwamba, Tanzania itaendelea kuwa mionganoni mwa nchi za mfano wa kuigwa katika Afrika kwa sababu ya namna tunavyopokezana madaraka na ndiyo maana unaona hakuna nongwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilitaka kutoa ushauri, wakubwa wetu kama wanatusikiliza wasikie, Waafrika tuna roho mbaya kila anayechukua madaraka kazi ya kwanza ni kutafuta mambo ya mwenzake bila kupanga mipango ya kuendeleza nchi aliyochukua, *priority* ni kumtafuta mwenzake aliymetangulia badala ya kuhangaika kuleta maendeleo ya wananchi. Haya mambo ambayo tunazuliana Waafrika, Marais wetu, hata Ulaya yapo. Nani amekwenda kufanya *research* Ulaya, Marekani na wapi akakuta kwamba, wale Marais wa kule hawana makosa. Nao wanayo, vitabu vinavyoandikwa sasa vinaonyesha kwamba, hata Marais wa kule nao si kamili kama Mungu, si Miungu lakini wao wanachojali kuchukua nafasi kusonga mbele. Sasa kwetu ni tatizo, kwa hiyo, inaonekana kama Afrika ndiyo kila mahali tunapata Marais wachafu tu kana kwamba, nchi zingine ni Marais watakatifu tu, ambapo si jambo la kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nataka niwashauri Marais wa Afrika, wasonge mbele, wasihangaike na mimi nilikuwa nasoma juzi niliomba kwenye *Internet* nipate *TV* ya Moi. Ukisoma *TV* ya Moi maisha yake karibu umri wake wote ameutumia katika siasa. Lakini kesho na keshokutwa mtaona anatundikwa msalabani. Kwa hiyo, hakuna anayeshukuru kwamba angalau alifanya kazi vizuri. Kwa hiyo, kitakachotokea ni kwamba, kila anapoingia Rais yule akimwandama watakaokuja vizazi hivi vinaweza kuwa na uhusiano na yule aliyeandamwa nao watamwandama na kesi nzuri ni Zambia ambako Rais Chiluba alimwandama sana Mzee aliyeleta uhuru wa nchi. Kwa hiyo, wenzake wanachofanya ni kile kile alichomfanyia yule. Mzee Kaunda alisema Mungu atanilipia, sasa ni yale yale kwa sababu hatuishi kwa kazi tunaishi kwa kutafutana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nawashauri Waafrika wenzangu, tuendeshe utawala na maendeleo ya watu ndiyo shida ya wananchi wetu, siyo habari ya kutafutana. Nani Mungu kati yetu hata humu ndani Bungeni? Hakuna. Tukianza kutafutana hakuna atakayepatikana kuwa safi, kwa hiyo, nataka

niseme suala la rushwa Waafrika wenyewe tunalizidisha, wenzetu wa Ulaya hawalizidishi. Sisi tunalizidisha wenyewe. Rushwa ya kule Ulaya siyo ya *traffic* wa barabarani ni ya hesabu kubwa ambayo ninyi hapa hamjui hata kuichunguza. Sisi tunahangaika na noti za unga, elfu kumi kumi za Hakimu wa Kijijini, Ulaya walishahama kwa noti, wapo kwenye dunia ya ulaji wa kisasa sio huu wa noti za unga. Kwa hiyo, tutamalizana bure na noti za unga na kudhani nchi ni chafu sana kumbe tunatafuta matatizo wenyewe, tunatafutana, watu hawalali kwa kutafutana. Mimi nawashauri Waafrika tusonge mbele, tunarudi nyuma kule. Hilo ndiyo la kwanza nililotaka niliseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Utawala Bora ni pamoja na kukubali matokeo ya uchaguzi. Kama wewe ni Rais, unagombea kipindi chako, bado hakiruhusu Chama kingine kikiingia wakishinda kubali matokeo na wale wanaokuja wapya wakishindwa wakubali matokeo. Sasa fujo zote za Afrika ni viongozi kutokubali matokeo. Mimi natoka Mikoa ya pembezoni, matatizo yetu sisi wa Kigoma na Rukwa ni makubwa sana kwa sababu ya tawala zisizo na heshima. Kule mimi nilikuwa *Regional Commissioner*, Burundi, Ndadaye alishinda uchaguzi, lakini Maaskari wakamwondo na aliyekuwa Rais zamani akarudi kwa *preface* kwamba, Maaskari wamemwambia rudi madarakani. Sasa nchi itakuwaje na amani wakati watu wanapiga kura, wanamchagua Rais, Rais huyo hawezi kufanya kazi anaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kutumia nafasi hii, naiomba Serikali yetu muombe Umoja wa Mataifa, *UNHCR* waje wafanye hesabu ya *damage* na hasara ambayo nchi yetu imepata ili tupate fidia. Haiwezekani tukawa tunapokea tu hawa watu wakimbizi, nchi yetu inapata hasara na hakuna anayetufidia, waje wafanye hesabu, *damage* ya mazingira iliyofanyika Kigoma, Kagera, ifanywe hesabu, Umoja wa Mataifa watufidie gharama yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuumba alikofanya Mwenyezi Mungu, tukiharibu kurudisha ni ngumu. Sasa ule uharibifu uliotokea Kigoma na Kagera nani anatufidia? Hivi ukarimu wetu unakuwa adhabu kwetu? Kwa hiyo, mimi nataka kusema hilo kwamba, viongozi wetu katika demokrasia yetu Utawala Bora ni pamoja na watu kukubali kushindwa katika chaguzi. Hata hapa kwetu mfano, hiki kitu cha Zanzibar kilichukua muda mrefu sana kwa sababu baadhi hawakukubali kwamba, matokeo yale ni halali. Mfano umekuwa pia hapa kwetu, kwa hiyo, mimi nasema tuheshimu matokeo ya uchaguzi. Hiyo ndiyo inaweza ikafanya nchi yetu kuwa na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nataka niseme naomba Viongozi wetu wa Afrika katika Umoja huu uliozungumzwa jana na hii ya *SADC* tunayozungumza sasa mambo ya *corruption*. Tufikirie na kuona uchungu namna Waafrika wenyewe wanavyokuwa wakimbizi ndani ya nchi zao wenyewe. *In their own mother land* wanakuwa wakimbizi katika nchi zao. Sasa viongozi wetu waone aibu angalau kwa hilo tu. Wasipepee bendera wakati wananchi wao ndani ya nchi zao wanakuwa wakimbizi, heshima ya Afrika iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na mzungumzaji aliyetangulia, kwa kusifu historia ambayo ilijitokeza kwa nchi za Afrika, ambapo wenyewe kutumia ubabe kunyakua madaraka na ambao wametoka katika madaraka kufikishana Mahakamani.

Kwa mfano, leo taarifa tulizo nazo, Chiluba amepelekwa Mahakamani kwa mambo ambayo anatakiwa ajibu mambo 96. Kwa hiyo, huu sio utaratibu mzuri wa demokrasia. Niliwaambia mwaka 2001 kwamba, demokrasia ina gharama lakini haina vipuri, wapo walioharibu demokrasia duniani ambao wameleta vurugu baridi, kashfa za kina na maisha ya kupigana katika nchi zao. Huu siyo mfumo wa kisiasa, tunaridhia Mkataba wa *SADC*, ambao Wakuu wetu walishakaa na kuuchambua kwa kina na nimeusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania tayari inakwenda kifua mbele katika maandalizi yenye ya neno hili la *corruption*. Labda nitoe tu taarifa ya historia kidogo ambayo jinsi Serikali ya Tanzania ilivyokuwa imefanya maandalizi hayo. Nimesema maandalizi mazuri yamesababisha treni ambayo inapita nchi kavu maji yakatoka kwenye mabomba, lakini maandalizi mabovu yakasababisha hata meli inayopita Ziwa Victoria maji yakakatika. Tanzania imetengeneza treni kwa maandalizi mazuri, mfano

mzuri ni maeneo matatu ambayo inayafanya, mikakati ambayo imefanywa na Serikali yetu chini ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niliulizwa na Watanzania kwa nini hivi rushwa inawekwa chini ya Utawala Bora, kwa nini isingekuwa chini ya shetani? Nikawaambia hapana, siyo ile Wizara inaitwa Wizara ya Rushwa, ni Wizara ya kuondoa au kupigana vita na rushwa. Kwa hiyo, vita lazima iwepo kwenye Wizara ambayo inashughulikia Utawala Bora. Kwa sababu *bad governance is equal to leadership plus work minus accountability*, unapata *bad governance*. Sasa katika upande wa Utawala Bora, tulifanya Wizara ya Utawala Bora chini ya *State House*, inafanya mipango mingi sana ya kuwakilisha masuala ya rushwa. Kwa hiyo, ndiyo maana tumekuwa kifua mbele, Rais alikwenda ku-ratify ule Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Novemba, 1999 wametoa kitabu chenye kurasa kama 29, kinachoonyesha mpango wa utekelezaji wa Jumuiya jinsi ya kuondoa rushwa nchini. Katika mpango huo utekelezaji kuna chomuifu moja, jumuifu na tondoti, katika ukurasa wa 17 jedwali namba mbili. Neno jumuifu nafikiri sasa hivi tumebadilisha tunaita mfumo shirikishi. Kwa hiyo, katika namba mbili Tanzania vile vile ilitoa kijitabu kinaitwa *the third phase government fighting against corruption brief progress on good governance* na programu ya kuanzia 1999 mpaka mwaka 2002. Ukurasa wa 20 kuna jedwali ambalo linaonyesha maandalizi maalum kuna ambayo wameeleza kuna *under time frame* na kila kitu, lakini kuna *certain places* ambazo *time frame* zake zimefikia lakini bado hajatekelezwa. Kwa kitabu kile naomba sehemu zile zipatiwe muda mwingine wa kukamilisha yale mambo. Yakikamilishwa yale tu tutakuwa tumejiandaa vizuri katika kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu namba tatu, toleo lingine lilikuwa *action plans for all Ministries* kuanzia mwaka 2001 - 2005 ukurasa wa 115. Sasa kuna *negative estimate* ambazo zilifanyika katika sehemu mbalimbali kwa mfano, kule *October out of gate* kulikuwa na *time frame*. Kwa hiyo, kuna majedwali yamepangwa kila Wizara iliambiwa jukumu na mtekelezaji halafu na mwisho wake nini halafu na matokeo yake. Lakini bahati mbaya katika maeneo hayo majedwali yale yameonyesha kuna maeneo ambayo utekelezaji ulikuwa bado. Kwa hiyo, tukifikia hatua hiyo ili twende kifua mbele tusafishe yale majedwali yalipo ukurasa ule ambao nimeutaja kwenye *Hansard* watakuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vite kuna *role of Parliamentarians fighting against corruption* ambayo ni mada moja nzito ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Pius Msekwa katika semina ali-quote *Act No. 6* ya Mwaka 1971 halafu ikawa *amended* mwaka 1974 mpaka akam-quote mtu mmoja ambaye anaitwa Edwin Gibbons, ambaye alieleza maana ya rushwa na kusababisha mpaka *Roman Empire ika-fall*. Hapo alikuwa hajutii uwoga ila alikuwa anatupa tahadhari kusudi sisi tukiwa na tahadhari tutaishi kwa matumaini katika suala hili la kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nukuu nydingine ilikuwa ni Edward Diamond Burken, ambaye katika mwaka 1729 mpaka 1796 alikuwa ametoa changamoto kubwa katika nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Tume nydingine ambayo inaonyesha juhudzi za Tanzania za kushughulikia suala la rushwa, Taarifa ya Tume ya Kero za Rushwa za Nchi ambayo ilikuwa ina kurasa karibu 216. Maelezo ya jumla walitaja vipengele kwa vipengele katika *volume* hizo, zilikuwa *volume* Na. 1, 2 na 3. Lakini kule Maktaba haupo tunaomba Na. 3 hiyo ije, nasikia kuna mambo hasa wanaeleza hata kwa jina na maeneo na wapi katika eneo hilo. Sasa walitaja makundi, kitu ambacho nilitaka ninukuu ambacho makundi hayo waliyotaja tuyafanyie kazi ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la kwanza linajumuisha wale wanaopokea rushwa kutokana na *Section A*, Tume ya Warioba ukurasa wa tatu, linajumuisha wale wanaopokea rushwa kutokana na hali yao duni ya mapato na kimaisha. Wanachopewa kusaidia kuziba pengo. Aina hii ya rushwa imeenea katika sekta zote za uchumi na huduma za jamii kwa mfano, akatoa sekta zote mpaka ya kumi na moja sitorudia. Nilitaka niseme ili Watanzania waone juhudzi ambazo Serikali hii imefanya katika kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la pili, ukurasa wa saba, *Section B*, kundi hili wanaopokea rushwa ni viongozi na watumishi wa umma wa ngazi za juu ambao kuhusika kwao katika vitendo vya

rushwa kunatokana na uroho wa kujilimbikizia mali na fedha. Hawa ni watu ambao vipato vyao halali vinatosheleza mahitaji yao ya msingi na wana mali na fedha za kutosha. Kundi hili linatumia mbini mbalimbali za kudai na kupokea rushwa kama ifuatavyo. Hizo mbini sizitaji kwa sababu tunajua tayari. Lakini hiyo ilikuwa inaainisha maeneo. Hiyo yote inaonyesha jinsi tulivyoandaa Tanzania katika kupambana na adui rushwa. Kwa hiyo basi, ndiyo maana Rais alisaini ule Mkataba kwa kuona kwamba, tayari ameandaa haya mambo kwa hiyo anaingia kifua mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natoa mapendekezo. Kama kuna watu ambao *in fact* tulishapata ushahidi tayari wa rushwa sasa tunakwenda kwa wenzetu kwamba, kwa sababu kwanza hakuna nchi ya kwenda kujifunza jinsi ya kupambana na rushwa, ukienda nchi iliyobobeaa unajifunza uharamia, ukienda nchi ambayo hawaajaanza kabisa rushwa unapeleka maasi. Kwa hiyo, hakuna kujifunza suala la rushwa ni nchi yenye katika kusimamia masuala haya. Halafu huwezi ukabuni tu ukasema kwamba, eti anakula rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lingine kwa sababu gani katika sheria za rushwa zinasema kwamba, mpokeaji na anayetoo wote wana hatia? Sasa nani atakayetuambia kwa sababu itakuwa siri yao, wanacheza dhikri bila dufu inaitwa ile. Kwa hiyo, inakuwa wanapokea mashilingi pale, wanayaweka mfukoni. Sasa anaambiwa kabisa ukienda kusema wewe mwenyeewe utakuwa na kosa kama mimi. Sasa nani atakayekuwa anasema? Kwa hiyo, hayo tumeshajiandaa vizuri sana katika kwenda huko, hayo ni maandalizi mazuri ya Watanzania katika kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile rushwa ndogo tunao uwezo wa kuwatataja na kuwaambia. Kwa hiyo, tuzitembeze zile fedha, kwa mfano, tulifanya majoribio mengi kwenye Jimbo kule. Tumekamata Mahakimu wawili, Mganga mmoja na wameshafukuzwa. Kwa hiyo, watu wenye kutoa taarifa ya fedha zile za rushwa zenye nambari na kuwapatia Watanzania, wapo tayari kuzipokea na kwenda kuzifanyia kazi. Kwa mfano, wakati huu uchaguzi wa Jumuia za wananchi, unampatia mtu fedha tu akaenda kumwona mtu yejote, akaamua mimi nataka nigombee. Kwa hiyo, akizipokea tu anakamatwa hapo hapo katika kusafisha nchi. Kwa hiyo, tutoe fedha kwa watu ambao sio wafanyakazi lakini ni watu ambao wanakuwa *agents*, Watanzania wa kawaida tu ambao wanababaishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, zipo kesi nydingi tu ambazo sasa hivi kati ya matajiri na maskini wanashtakiana kwa kudaiana ardhi, ziangaliwe hizo kwanza, kwa nini zimekaa muda mrefu, ndiyo maana watu wanasema Mahakamani kuna sheria hakuna haki. Nikawaambia haki ipo ila tu kwa sababu ya baadhi ya makundi mawili yaliyotajwa katika Tume ya Warioba ndiyo wanasabisha haki ipotee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Azimio hili liungwe mkono ili nchi hizo zinaweza kutusaidia kwa *global* ya nchi hizi katika kundi hili la *SADC*. Kama mtu anakula rushwa Watanzania hatumfahamu, nchi hizo wanafahamu, basi watuambie na sisi kama kuna mtu anakula rushwa katika nchi zao wao hawajui, sisi tunamtambua anakula rushwa pengine yupo ofisi ya Ubalozi wao, tutawaambia. Sasa tutaangalia hatua za kuchukua kama kufukuzana ili kuondoa hivi tunavyoita vimeta. Kwa hiyo, afadhalii kusafisha katika nchi hii ili kuondoa vimeta ili nchi isonge mbele na kupata Taifa ambalo tumepeewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru na naunga mkono Azimio hili. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani kwako kwa kunipatia nafasi ya kusimama tena ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, walizozitoa katika kuchangia hoja ya mawasilisho ya Azimio hili. Lakini kabla sijafanya kazi hiyo, kwa ruhusa yako, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu, ambao tumewachagua wenyewe asubuhi ya siku ya leo kutuwakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nikianza na Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, Mheshimiwa Dr. Hajji Mwita Hajji, Mbunge wa Muyuni na Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kabla sijaanza kutoa maelezo mafupi kwa hoja zilizojitokeza na ushauri, niwatambue waliochangia hoja yetu. Wa kwanza ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, aliyewasilisha taarifa na maoni ya Kamati. Wa pili,

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani. Wa tatu ni Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail. Wa nne Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya. Wa tano na wa mwisho ni Mheshimiwa Semindu Pawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru wote kwa michango waliyoitoa kuweza kutoa ushauri ambao utaiwezesha Serikali kuwajibika ipasavyo kwa mujibu wa Itifaki ambayo Azimio lake tumeliwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kweli kwa ufupi, lakini kwa uzito wa kipekee, baada ya kuridhika na sababu zilizoiwezesha nchi yetu kukubali kushirikiana na wenzetu katika Jumuiya ya *SADC*, tunayapokea. Wametushauri kwamba, ni vizuri ndani ya nchi tukaandaa mikakati itakayotuwezesha kupambana na rushwa na hivyo kunufaika na mashirikiano chini ya Itifaki hii. Ushauri wao tunauzingatia na pongezi ambazo tumezipata kupitia kwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Athuman Janguo, kwa niaba ya Kamati, tunazipokea kwa heshima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani naye tunamshukuru, tunaridhishwa na upande wa Kambi ya Upinzani kuunga mkono hoja yetu na ushauri wa Kambi ya Upinzani tutauzingatia ili kuhakikisha kwamba, usimamizi wa mikakati ya ndani ya nchi katika kupambana na rushwa inaleta mafanikio ndani ya nchi na mashirikiano yanakuwa na manufaa kwa nchi yetu. Ameweza kuzungumzia maneno machache lakini yenyé uzito kwamba, ni muhimu tuweke mkazo katika elimu ya uraia, sera za kupunguza umaskini na kuhakikisha kwamba, tunajenga demokrasia ambayo inatoa nafasi ndani ya *SADC* kwa namna ambayo itachangia katika kupambana na umaskini. Sisi tunaafikiana na ushauri wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, natofautiana naye katika eneo la kusema kwamba, Serikali katika kupambana na rushwa imezorota. Nawashukuru wachangiaji wote, ambao hawakutokea Kambi ya Upinzani. Kwa sababu wachangiaji toka Chama Tawala, wamekiri na kutambua maeneo ya mafanikio ambayo yameweza kudhihirishwa katika kupambana na rushwa, kwa hiyo, kuwapa moyo vijana ambao wapo kwenye *field* wakipambana na rushwa. Kwamba kazi inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli kama ambavyo wachangiaji waliotangulia wakiunga mkono hoja, Mheshimiwa Mzindakaya, Mheshimiwa Semindu Pawa, jinsi walivyotoa mifano kadhaa ya mafanikio katika vita dhidi ya rushwa ndani ya nchi yetu niliposikiliza nimefarijika sana kwa sababu hizo kauli zinapeleka ujumbe kwa vijana wa vyombo vya dola, Polisi, Taasisi ya Kuzuia Rushwa katika mapambano dhidi ya rushwa kwamba, kwa kweli jitihada zinafanyika katika kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kupambana na rushwa na mpango wake. Nataka kusema mimi ninaposikia kwamba, vita inazorota, huwa nashindwa kuelewa inazorota wapi kwa sababu zifuatazo:-

Nikitoa mifano michache, kwanza, kama Mheshimiwa Semindu Pawa, alivyozungumza akinukuu mapendekezo ya Tume ya Mheshimiwa Rais ya kuchambua chanzo cha matatizo ya rushwa ikiongozwa na Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba. Maeneo yaliyoonyeshwa katika taarifa hiyo ni pamoja na rushwa iliyokuwa inatokana na kuandikisha watoto shulen. Serikali ya Awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, tumefuta ada na michango kwa shule za msingi. Mimi naamini ni mchango mkubwa katika kupunguza rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, eneo lingine ni hizi kero ambazo kwa ushirikiano wa Bunge hili Tukufu, jana tu mmepitisha *Finance Bill*, Muswada wa Sheria ambao umeweka bayana maeneo ambayo Halmashauri za Wilaya na Miji hazitaruhusiwa kutoza kodi na ushuru na ni maeneo ambayo yalikuwa yanalamikiwa na wananchi kwa kiasi kikubwa kama chimbuko la rushwa na unyanyasaji. Sasa Bunge hili limeazimia likiunga mkono hoja ya Serikali, kufuta kodi nyingi tu na ushuru mwangi. Kwa hiyo, automatically tunajua tu wale waliokuwa wanapata rushwa kutokana na kodi ambazo zimefutwa na ushuru za kero hawatapata nafasi ya rushwa. Hiyo ni hatua ya kupambana na rushwa kwa sababu tunaziba mianya ya rushwa. Kwa sababu msingi wa mkakati wa kupambana na rushwa wa Serikali na mpango wake ni kuzuia zaidi na hasa kwenda kisayansi ili kuepuka malalamiko ambayo yanaweza kutokana na watuhumiwa kudai kwamba, tunakiuka haki za binadamu au tunavuruga amani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili vile vile ni kuwashughulikia wale ambao wanabainika kuhusika na vitendo vya rushwa, ambayo siyo kazi rahisi lakini vijana wanajitahidi katika maeneo yote Mahakamani, Polisi na hata maeneo ya *TRA*. Kila sehemu imeweka utaratibu Polisi wanawajibishana, wanafukuzana, Mahakamani wanawajibishana, wanafukuzana. Jana tumemsikia Waziri wa Fedha anazungumza ni hatua gani zitachukuliwa katika kuweka mitambo ya kompyuta ku-*automate* shughuli za *Tanzania Revenue Authority*, ili kuwanyima nafasi wale vijana sugu ambao tunaweza kusema ni wahanga wa rushwa, kuendelea kula rushwa, pamoja na mishahara mikubwa. Kwa hiyo, ni hatua ambazo zinaonyesha kweli si muda mrefu tutabaki na watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili hili limeidhinisha Ofisi ya Rais, kupeleka vijana wa *PCB* Wilaya zote kwa kufungua ofisi za Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Tutashangaa baadaye kuanzia pale ambapo tutakamilisha ufunguzi wa ofisi hizo za Taasisi ya Kuzuia Rushwa kila Wilaya kusikia watu wanalamika vitendo vya rushwa Mahakamani, Polisi au *TRA* ngazi ya Wilaya. Kwa sababu hapo itabidi viongozi wa Idara hizo, Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mahakama ya Wilaya yenye dhamana ya kusimamia nidhamu, atabidi awajibike kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanaendelea kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa na yeze hachukui hatua yoyote. Kwa hiyo, *OCD* na *RPC* hivyo hivyo kwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini hatua kwa hatua, nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa kuhakikisha kwamba, tumezunguza kero za rushwa na kusema kweli kama mtakavyoangalia kwenye Itifaki hii, Ibara ya tatu matendo yote yanayoainishwa kama makubaliano ya kutekelezwa, sisi Tanzania tupo mbele, tuna Sheria ya Kuzuia Rushwa ya Mwaka 1971, tumeshatunga Sheria ya Manunuzi (*Public Procurement Act*) na Sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act*). Pia tunawalinda watoa taarifa dhidi ya viongozi wanaokiuka maadili mpaka kiwango cha Bunge hili kuidhinisha kwamba, unaweza ukatoa taarifa bila kutaja jina lako wala anwani yako ili tuweze kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, kusema kweli tumeziga hatua siyo kwamba, ni kujisifu lakini hata ndani ya *SADC* na Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara, nchi yetu inahesabika mionganoni mwa nchi ambazo zipo katika mstari wa mbele kuzingatia Utawala Bora na mapambano dhidi ya rushwa tukiwa katika kundi la nchi saba bora. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi bado ipo hatuwezi kujivuna kwamba kazi imekwisha, tunajua rushwa bado ipo, tunachopenda kuwaasa Watanzania ni kushirikiana kwa kupashana taarifa na kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail, katika kuunga mkono hoja yetu, ameonyesha wasiwasi kwamba, hana uhakika kama katika Itifaki rushwa ya ngono imefikiriwa. Nimeshauriana na wataalam wangu wameniambia kwamba, chini ya Ibara ya 3(1)(e), wanasema mtooa rushwa ya ngono tuseme kwa mfano, kwenye kuomba kazi ya Afisa Mtendaji Mkuu wa *SADC*, anaweza akashughulikiwa chini ya Ibara hiyo. Labda atanusuriwa na Mahakama au *Tribunal*. Yenyewe inasema hivi kwa sababu sitazungumza sana naweza nikainukuu kwa kirefu:-

"This Protocol is applicable to the following Acts of corruption, the offering or giving, promising, solicitation or acceptance, directly or indirectly, of any undue advantage to or by any person who directs or works for, in any capacity, a private sector entity, for himself or herself or for anyone else, for him or her to act, or refrain from acting, in breach his or her duties." Mwisho wa kunukuu. Watalamu wanasema na mimi naafikiana nao, ukiahidi ngono au ukitoa ngono hapa wanaweza wakashughulikia ukapata tabu Mahakamani au ukanusuriwa na Jaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, tumezata ushauri wake kuhusu viongozi wetu wa Afrika na sisi kwa sababu tunazungumza kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, tutamfikishia ushauri huu aweze kuufikisha kwa viongozi wenzake. Kulingana na mazingira ambayo ataona kwa hekima yake yanafaa. Kama kweli kuna viongozi wanaopata madaraka wakawasaka wenzao wastaafu ili wawanyanyase bila sababu za msingi, kwa kweli si jambo jema. Lakini kama kuna viongozi ambao wamestaafu na wana makosa au wana madhambi wakifutiliwa kwa mujibu wa utaratibu na heshima itakuwa nadhani ni sahihi kabisa.

Mimi napenda tu kusema kwamba, sisi ndani ya nchi yetu tuna bahati na wengine kutokana na bahati ya nchi yetu tuliyonayo ya kuwa na viongozi wengi waadilifu wanashangaa kuona hakuna kiongozi mkubwa tunayemkamata. Hatuwezi kumkamata mtu ili kuridhisha Mataifa ya nje kwamba, tumemkamata kigogo au Mheshimiwa Rais Mstaafu au Waziri wa zamani au Meneja Mkuu wa zamani, ili tuonekane tunapambana na rushwa. Sisi tunaamini katika misingi ya haki za binadamu katika utendaji wa makosa ya jinai wote ni sawa. Anayefanya kosa dogo na kubwa wote ni sawa na wanashughulikiwa bila ubaguzi kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu inayoleza kwamba, kila Mtanzania ni sawa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunawasikitikia wenzetu ambaa wanahangaishana na viongozi wa zamani na labda hii ni kutokana na mazingira ya huko kwao. Mimi siwezi kuyasemea. Lakini katika mashirikiano ya *SADC* ni wazo la kuwapelekea viongozi wetu waweze kulitafakari. Kwa sababu wao ni viongozi wa sasa na baadaye watakuwa viongozi wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha Waafrika kuwa wakimbizi katika Bara lao. Sisi Tanzania tunapokea wakimbizi kweli na ni kero. Ushauri tumeupata na sisi tunaendelea kushirikiana kama Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alivyozungumza asubuhi hii. Katika jitihada za kuhakikisha kwamba, nchi jirani zinazofarakana na kupigana wanapata amani ili wakimbizi warudi kwao.

Mheshimiwa Semindu Pawa, ametoa pongezi na tunazipokea kwa kazi nzuri inayofanyika. Majedwali aliyyotolea mfano katika taarifa za utekelezaji wa vita dhidi ya rushwa tumeyazingatia. Ni kweli, siyo kila jambo limekamilika. Lakini tunamshukuru kwa kukiri kwamba, kazi kubwa imefanyika na yale yaliyobakia kwa ushirikiano wa Watumishi na Bunge yatakamilishwa kama alivyoshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wajibu wa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge kwa kweli mnafanya kazi kubwa sana na kusema kweli nimetoo mifano ya Maazimio ya Bunge na kupitisha Sheria ambazo zimesaidia kupunguza kwa kuziba mianya ya rushwa katika nchi hii. Huo ni mchangao wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge binafsi wanashughulika na matatizo ya rushwa katika Majimbo yao kuhakikisha kwamba, wananchi hawapati matatizo ya wale wenye vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ile rushwa kubwa kubwa katika nchi yetu kama alivyooleza Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, huwa inatofautiana kati ya nchi na nchi. Nchi zingine rushwa kubwa kubwa ni ya mabilioni ya fedha. Sisi rushwa ikifika milioni imeshakuwa kubwa. Sasa nchi zingine hiyo wanaweza wakasema labda siyo *corruption* ni *petty* na wengine hawatumii noti za unga kama alivyosema Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kwa sababu rushwa yao ni kwa waya (*electronic*), mtu anahamisha mabilioni ya fedha anapeleka nchi nyingine. Mmesikia hata kwenye Vyombo vya Habari, kesi zinazoendeshwa Switzerland

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siamini kama Tanzania kuna Kiongozi wa sasa au mstaafu, ambaye amekula rushwa akapeleka fedha nje ya nchi. Kwa sababu simjui yeoyote na mimi huwa narudia ingawa huwa inanigonganisha na watu wengi kwamba, labda naficha ukweli. Sina jina hata moja mbele za Mwenyezi Mungu kwamba, nimeletewa jina la kiongozi mstaafu au wa sasa mla rushwa aliyeficha fedha nchi za nje, kwa sababu ninafanya kazi kwa kiapo. Tunaweza kutumia utaratibu wa nchi za wenzetu, Pakistan wameweza kuwashughulikia familia ya Butto, Waziri Mkuu wa zamani na mumewe, nimesikia hukumu jana kwamba, walikuwa na milioni nyingi Switzerland. Lakini Tanzania huwa tunasikia rushwa, fedha nyingi, *Grand Corruption* kwenye vyombo vya habari, sipati jina. Mheshimiwa Rais hana majina, kwa sababu hawezi kunificha. Akiletewa jina la mla rushwa mwenye fedha nchi za nje lazima ataniambia. Kwa nini anifiche na ametupatia kazi ya kumsaidia kwa kuwafatilia hawa watu. Kama kuna Mheshimiwa Mbunge ana taarifa bila hata kutuletea sisi anaweza akamshughulikia ndani ya Bunge hili, kwa kuleta hoja binafsi au hoja maalum na hii ni kwa Kambi ya Upinzani na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa makusudi kwa sababu rekodi nzuri ambayo tunaenda nayo nchini hapa inaheshimika dunia nzima. Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wa CCM, tumeendesha Bunge hili kwa kukubaliana na kwa muafaka. Haijawahi kutokea katika nchi nyingine na leo ni siku ya mwisho naamini. Sasa nchi ya namna hiyo mtu akisema rushwa imekithiri ambayo haikujadiliwa kwenye Kikao cha Bunge cha Bajeti cha miezi miwili ikaandikwa

kwenye magazeti, ni mawili, ama Bunge liko mbali na Vyombo vyा Habari au Vyombo vyा Habari viko dhidi ya Bunge na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tupeane moyo na shime tupambane kwa pamoja tujenge heshima. Kwa sababu kinachoshusha heshima ya nchi hii ni watu wanaotoa taarifa mitaani na kwenye Vyombo vyा Habari kwenda *Transparency International* na Mashirika mengine ya watafiti. Mkisema tunaridhika kama Waheshimiwa Wabunge, wanavyoridhika *chart* yetu inapanda. Wawekezaji wanaendelea kumiminika. Nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, wawekezaji wana imani na Serikali yetu, mazingira ya uwekezaji na wanamiminika kwa nguvu sana na hii ni heshima kwa Watanzania wote siyo kwa Chama cha Mapinduzi peke yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa, kwa kunipa fursa hii na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunipa usikivu mtulivu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kupambana na Rushwa*
liliridhiwa na Bunge)

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika Dhidi ya Ugaidi wa Mwaka 1999 (The OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism 1999)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika Dhidi ya Ugaidi wa Mwaka 1999 (*The OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism 1999*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganini mwa majukumu ya msingi ya Umoja wa Afrika ni kuhakikisha kuwa kuna amani na usalama, maendeleo, umoja na ushirikiano baina ya nchi za Bara la Afrika. Ushirikiano huo unahitajika zaidi katika kujenga msimamo wa pamoja wa kupambana na tishio la vitendo vya kigaidi ambavyo vimeshamiri sana duniani kote katika miaka ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo linaloleweka kwamba, Mtandao wa Kigaidi umelikumba Bara letu. Ushahidi ni matukio ya ugaidi yaliyotokea Dare es Salaam na Nairobi mwaka 1998 na mengine ya hivi karibuni tu yaliyotokea Mombasa Novemba, 2002 na Morocco mwezi Mei, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kuitia Bunge hili tayari imekwishadhihirisha nia yake ya kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kukabiliana na ugaidi. Katika Mkutano wake wa tisa wa mwezi Novemba, 2002 Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Ugaidi. Aidha, katika Mkutano huo huo Bunge liliridhia Mikataba mitatu ifuatayo dhidi ya vitendo vya ugaidi: Kwanza, Mkataba wa Kimataifa Dhidi ya Utekaji Nyara wa mwaka 1979. Pili, Mkataba wa Kimataifa wa Kukomesha Ugaidi wa Kutumia Mabomu ya mwaka 1998 (*The International Convention for the Suppression of Terrorist Bombings*). Tatu, Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Ugharamiaji wa Ugaidi wa mwaka 2000 (*The International Convention for Suppression of Financing of Terrorism*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu ninaoomba uridhiwe na Bunge hivi sasa, ulikubaliwa na Wakuu wa Nchi Huru za Afrika Mjini Huges Algeria na kutiwa saini tarehe 14 Julai, 1999. Tanzania ni mionganini mwa Nchi zilizotia saini Mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu una vipengele muhimu vifuatavyo: -

1. Kuzuia nchi wanachama kutumiwa na magaidi kufanya shughuli zao za kigaidi.
2. Umuhimu wa kushirikiana na kubadilishana taarifa na uzoefu kuhusu makosa ya kigaidi na wahalifu wa makosa ya kigaidi.
3. Wajibu wa Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kutunga sheria zenyenye hukumu kali zinazolingana na uzito wa makosa ya kigaidi
4. Utaratibu wa kuridhia, kujiunga na kujitua katika uanachama wa Mkataba huu.
5. Utaratibu wa kusuluhisha migogoro inayoweza kutokea kati ya nchi moja na nyingine katika tafsiri au kutekeleza Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhiwa kwa Mkataba huu kutaleta manufaa yafuatao mionganoni mwa mengine katika nchi yetu:-

1. Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zitakuwa tayari kushirikiana nasi katika kuzuia na kukabiliana na ugaidi.
2. Nchi yetu itapata misaada ya kiufundi kutoka Mataifa mengine.
3. Kutakuwa na ubadilishanaji wa taarifa kuhusu mienendo ya magaidi baina ya nchi yetu na nchi nyingine. Hivyo, kuchukua tahadhari za kuzuia matukio ya kigaidi kufanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika Dhidi ya Ugaidi wa mwaka 1999, ambalo naomba Bunge likubali na kulipitisha. Azimio lenyewe linasomeka kama ifuatavyo: -

KWA KUWA Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika na iliweka saini kwenye Mkataba wa Umoja wa Afrika Dhidi ya Ugaidi mwaka 1999 (*The OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism 1999*);

NA KWA KUWA Mkataba wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika Dhidi ya Ugaidi wa mwaka 1999 una vipengele 23 ambavyo vinaweka utaratibu kuhusu kupambana na vitendo vya kigaidi Barani Afrika;

NA KWA KUWA vitendo vya ugaidi vina madhara makubwa kwa jamii, walengwa na wasiolengwa, kwa kupoteza maisha, mali au kupata ulemavu wa kudumu;

NA KWA KUWA Tanzania, inatambua madhara yanayotokana na vitendo vya kigaidi popote yatokeapo Barani Afrika na duniani kwa ujumla, inakusudia kuridhia Mkataba huo ambaa ni moja ya hatua za kukabiliana kwa dharti na vitendo vya kigaidi;

NA KWA KUWA Tanzania imekwishachukua hatua nyingine za kukabiliana na vitendo vya ugaidi duniani kwa kuridhia Mikataba ya aina hiyo iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa na ile iliyopitishwa na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) na kwa sababu hiyo haina matatizo yoyote wala pingamizi kuhusu utekelezaji wake;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia manufaa ambayo Tanzania itayapata kutoptaka na mapambano dhidi ya vitendo vya kigaidi viliviyolikumba Bara la Afrika na Dunia kwa jumla. Bunge hili katika Kikao chake cha Kumi na Mbili, sasa linaazimia kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tanzania inaridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika Dhidi ya Ugaidi wa mwaka 1999 (*The AOU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism 1999*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha mawazo ya Kamati kuhusu hoja iliyotolewa, ningependa nami nichukue nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu na Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa ujenzi wa daraja la Rufiji ambalo linaitwa Daraja la Mkapa. Kwa ujenzi wa daraja hili limefungua mlango tena mpana kwa wenzetu wa Mikoa ya Kusini kujiunga kiuchumi na Taifa zima. Ni matumaini yangu kwamba, wenzetu wa Mikoa ya Kusini watautumia mlango huo kadri itakavyowezekana na ipasayyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupendekeza kwa Wizara ya Ujenzi, kwa kuwa waliohudhuria sherehe ile ni wachache, basi tungeiomba Wizara ya Ujenzi, hata kwa gharama ichukue kurasa katika magazeti yetu, ionyeshe sehemu mbalimbali za daraja hilo ili na Watanzania wengine popote walipo wajue kazi kubwa iliyofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, kwa kukaribisha Mkutano wa SADC kuja kufanyika Tanzania. Ni matumaini yetu na ni matazamio kwamba, ye ye ndiye atakayekuwa Mwenyekiti na ni lazima tuchukue nafasi hii. Kwanza, Watanzania wote kumuunga mkono kwa kuwapokea wageni wote watakaokuja kwa furaha. Lakini kwa wakati huo huo tukisaidia juhudhi za Mheshimiwa Rais wetu kufanya Tanzania iwe karibu na majirani zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kabla sijaendelea ningependa pia nichukue nafasi hii niwapongeze wale Waheshimiwa Wabunge wenzetu, waliochaguliwa kwenda kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nao ni Prof. David Mwakyusa, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Ninawatakia kila la kheri kwamba, waende wakawakilishe Bunge hili kwa heshima zote zinazostahili na waweze kuinua hadhi ya Chuo chetu Kikuu, ambacho kwa kweli ndiyo Chuo Kikuu cha kwanza ambacho kilijengwa hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ningependa nichukue nafasi hii kwa masikitiko sana kuwapa pole Mheshimiwa George Kahama na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa msiba mkubwa, narudia kwa msiba mkubwa uliowapata wa kufiwa na mtoto wao Kiiza. Namwomba Mwenyezi Mungu, awape subira Mheshimiwa George Kahama na Mheshimiwa Janet Kahama na Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ningependa kwenda kwenye Azimio ambalo limetolewa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 70(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni na ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika (*Africa Union*), dhidi ya Ugaidi wa Mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, ambao wamelipitia Azimio hili na hatimaye kutoa mawazo yao kuyaleta hapa Bungeni na Wajumbe hao ni: Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Frank

Magoba, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Thomas Nyimbo na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa lengo kuu la Mkataba huu ni nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, kushirikiana katika kuzuia na kupambana na vitendo vya kigaidi kwa nchi wanachama wa *African Union*. Umuhimu wa kuridhia Mkataba huu ni pamoja na kuziwezesha nchi wanachama kushirikiana katika kupata na kubadilishana taarifa kuhusu vitendo vya kigaidi vikiwa katika hatua mbalimbali. Aidha, kuziwezesha nchi wanachama kusaidiana kwa njia ya mafunzo ya kupambana na vitendo vya kigaidi vya Kitaifa na vya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, mwaka 2002 Bunge lako Tukufu, lilipitisha Sheria ya Kuzuia Ugaidi (*The Prevention of Terrorism Act, No. 29932*). Hivyo, kuridhia Mkataba huu ni kuimarisha utekelezaji wa sheria hiyo. Hata hivyo, kutokana na utata wa tafsiri ya ugaidi kwa nchi mbalimbali, Kamati ina maoni ya kupendekeza kwenye Bunge hili yafuatayo:-

1. Nchi zote za wanachama wa Umoja wa Afrika zikubaliane tafsiri ya ugaidi na vitendo vya ugaidi ili iwe na mtazamo unaofanana.
2. Nchi na wanachama ziimarishe demokrasia na Utawala Bora ambao tumetoka kuzungumzia ili kuepusha migogoro inayoweza kuwa chanzo cha kushamiri kwa ugaidi.
3. Nchi wanachama zisitangulize mbele itikadi zao katika harakati za kupambana na vitendo vya kigaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mapendekezo hayo, Kamati sasa inaliomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na hatimaye kuridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunisikiliza na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na kusema kwamba, Kamati inaliunga mkono Azimio hili na kuwasihii Waheshimiwa Wabunge wote, waliunge mkono Azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili.

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kueleza machache kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Kuridhia Azimio la Umoja wa Afrika juu ya Vita Dhidi ya Ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu namba 43(5)(b)(c) Toleo la mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo na mimi naomba nichukue nafasi hii kwanza, niipongeze Serikali kwa kitendo cha kihistoria ambacho mimi mwenyewe nilikishuhudia juzi kule Rufiji cha ufunguzi wa Daraja, ambalo kwa kweli ni kilomita moja maana yake limepungua kidogo tu. Nasema ni kitendo cha kihistoria kwa sababu tabu iliyokuwa inapatikana kwa watu wote ambao walikuwa wanatasafiri upande ule na mimi nikiwa mmojawapo, mwaka 1997 nikiwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge hili, tulilazimika kwenda Lindi, Mtwara, kuititia njia ile kwa kweli tuliteseka sana.

Tulilazimika kulala mahali ambapo hatukupanga kulala. Kwa hiyo, nasema kusatikana kwa daraja hilo ni ukombozi wa Watanzania wote, kwa sababu hilo daraja tutalitumia sote, lakini pia ni ukombozi wa Afrika nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzenzu waliochaguliwa asubuhi kuingia katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye mada sasa, Kambi ya Upinzani inasema kwamba, pamoja na ubishi ambao bado upo duniani kuhusu maana ya ugaidi, hasa kutokana na ukweli kwamba, gaidi wa fulani anaweza kuwa mpigania haki na uhuru wa mtu mwengine.

Imetamkwa wazi katika kifungu cha tatu, sehemu ya kwanza ya makubaliano ya *OAU* kuhusu kupambana na ugaidi (kijishehemu cha kwanza) kwamba, harakati zozote za watu kutaka uhuru wa kujiamulia mambo yao wenye, kujikomboa ikiwa ni pamoja na matumizi ya mtutu wa bunduki dhidi ya ukoloni, uvamizi na ugandamizaji wa wananchi, havitahesabika kuwa ni vitendo vya kigaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kijishehemu cha pili katika kifungu cha tatu, kinatahadharisha kwamba, nia na harakati za kisiasa, kifalsafa, kiitikadi, kinasaba, kidini, rangi ya mtu vilevile si kinga timilifu au toshelevu dhidi ya vitendo vya ugaidi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kifungu cha 8 hadi 12 kuhusu “Magaidi” kuhamishwa kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine (*extradition*), inaweza kutumiwa na Mataifa yenye nia za kimaslahi na kimkakati kufanikisha kulalamikia namna wafungwa wa kiarabu na kadhalika kutoka Afghanistan na Pakistan wanavyoteswa kule *Guantanamo Bay*, Cuba na Majeshi ya Marekani. Huko Marekani inakataa kuwatambua wapiganaji wa Al-Qaeda kama mateka wa kivita na inataka dunia isilaani mateso hayo. Watetezi wote wa haki za binadamu, bado wanaishutumu Marekani kufuatia unyanyasaji wa hali ya juu wa wafungwa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Kimataifa inayostaarabika haiwezi kuendelea kuliachia Taifa moja kubwa kujivisha nafasi ya Polisi wa Kidunia (*Global Cop*) na kutumia misuli yake kuyachagiza na kuyafolelisha Mataifa madogo madogo kwa lengo la kujipatia faida iliyokithiri (*Super Profit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Kimataifa pia haina nafasi maalum ya kumwendeleza au kumdekeza ye yote yule anayetumia visingizio vyovoyote kukatisha maisha ya watu wasio kuwa na hatia, hasa akina mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo jema pia kwa hao wanaodaiwa kuwa ni “Magaidi” kumuua ye yote anayekatisha mbele yao, kwa kudaiwa ni mmoja katika wanaokwamisha maslahi yao ya kisiasa, kiitikadi, kidini na kadhalika. Mauaji ya watu wasio na hatia hayawezi yakahalalishwa na kitu chochote kile na ni lazima yalaaniwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalojitokeza katika nchi nyingi za Kiafrika, hasa zile zenye ugaidi wa aina fulani katika demokrasi ya kiushindani, wakati mwengine ni kule kuubandika Upinzani wa kawaida wa kisiasa chapa ya ugaidi wa Kitaifa na Kimataifa. Wananchi wakiandamana mitaani kwa amani kabisa na Wapinzani wakiandaa mikutano mikubwa ya hadhara, hivyo vyote wakati mwengine huovichwa joho la ugaidi, kwa lengo la kuwafanya wachukiwe na watu wa ndani ya nchi husika au Jumuiya ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa nchi na nchi katika upelelezi na mambo ya Kisheria ni lazima utangulize mbele heshima ya kila Taifa, badala ya Taifa moja kuliamrisha na kulipigisha kwata Taifa jingine huru. Hii tabia ya nchi moja kujaza makachero wake kibao katika nchi nyingine ni kitendo cha kuidhalilisha nchi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia hii ya wakubwa pia ijitahidi kukwepa mambo yanayowazalisha hao tunaowaita “Magaidi”. Wakubwa kabisa wa ulimwengu huu wajitahidi sana kukwepa mambo yanayowazalisha hao wanaoitwa magaidi. Ni kweli kuwa magaidi wakati wowote ni tatizo. Lakini vitendo vinavyozalisha magaidi ni tatizo zaidi na zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono kuridhiwa kwa Mkataba huu na inaipongeza sana Serikali kwa kuleta kwa wakati unaofaa. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia. Naomba kabla ya kuanza niwapongeze wenzetu Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwakilisha Wabunge katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nawaomba waende wakafanye kazi nzuri pale Chuoni. Ni Chuo ambacho kimetuzalisha sisi wote, sisi ambao tumepitia kwenye huu mkondo wa Elimu ya Chuo Kikuu ndani ya nchi yetu kwa wakati ule tulioptitia, kwa hiyo, tunawaomba mfanye kazi nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa kujali wananchi wake na kwa kutii matakwa ya Katiba. Suala la ugaidi ni suala la usalama wa Taifa, ni suala la usalama wa raia. Katika Katiba yetu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 14, kila mtu aliye kwenye nchi hii anayo haki ya kuishi na anayo haki ya kupata ulinzi kutoka kwenye Taifa letu. Hakuna mtu ye yote ambaye ata-exercise zile haki zake za kibinadamu katika nchi hii kwa njia ambayo atawezu kumwumiza raia mwengine wa nchi hii. Moja kati ya njia za kutumia uhuru wa mtu na kuumiza mwengine ni hii njia ya ugaidi kwa ajili ya kulazimisha nchi, Serikali au raia kukubaliana na msimamo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu na Serikali ya Tanzania ilishatambua umuhimu wa kutii hayo matakwa ya Katiba. Mwaka 2002, tulipitisha sheria ya kupigana na Ugaidi. Wakati ule tunaipitisha hatukuwa tumeridhia huu Mkataba japo kuwa ulikuwa umeshasainiwa na Rais wetu. Hiyo haidhuru na hakuna jambo lolote baya lililotokea kwa sababu huu Mkataba hauhusu kupigana na ugaidi ndani ya nchi bali unahusu mashirikiano ya Serikali za *SADC* katika kupigana na ugaidi katika eneo letu la *SADC*. Kwa hiyo, hakuna kitu chochote kinachofanya ile sheria na huu Mkataba vipingane au tuonekane kwamba, tulikimbia haraka mno kabla ya kufikia makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkataba huu ibara ya 4(2)(a), wamekubaliana viongozi wetu kwamba, nchi zote za *SADC* ziwe na wajibu wa kuzuia nchi zao kutumika kama vituo vya kupanga au kuendeshea ugaidi. Sasa hivi ugaidi ulio mkubwa zaidi ni ugaidi wa Kimataifa. Wakati tukipitisha ile sheria ya kuzuia Ugaidi, tulikuwa tunapata Upinzani kwamba, sheria ili kuwa inapinga haki za binadamu. Tumeona jambo ambalo limetokea Kenya. Kenya wamekuwa wanapinga sana sheria kama yetu lakini ni juzi tu, mtu amekamatwa kwa kushukiwa ni gaidi anasindikizwa Polisi akajilipua na askari akafa. Kwa hiyo, katika kupigana na ugaidi ni lazima kuwe na hatua ambazo sio za kawaida, sio jinai ya kawaida, ni jinai ambayo inaweza ikaondoa maisha ya mtu mara moja. Kwa hiyo, huwezi kuchukua haki za binadamu chini ya sheria ya jinai katika kupigana na ugaidi kwa sababu hujui ni lini atakuua. (*Makofî*)

Yule maskini marehemu askari wa Kenya, hakuwa amejua kwamba yule gaidi angejilipua. Lakini hata hivyo, ninayo *concern* juu ya haya makubaliano ya kuruhusu *investigation* zifanywe kuruhusu Polisi wa nchi moja kufanya kazi ndani ya nchi nyingine. Ni wazo zuri kushirikiana. Lakini ningeshauri kwamba, nchi zetu ziepuke *scenario* kama *scenario* ya Marekani kupeleka *FBI* katika nchi nyingine, wao ndio wanakuwa wakamataji na badala ya kupitisha wale washtakiwa kwenye mikondo ya sheria katika nchi ile, wanaamu kutorosha watu ambao wanawashuku Magaidi. Ninafurahi sana kwamba, katika Mkataba huu kuna makubaliano kwamba, Gaidi ye yote atakayeshukiwa atashughulikiwa kwa sheria ya nchi ile ambayo amekamatwa na kama ni kupelekwa kwenye nchi nyingine basi zile sheria za *extradition* za ile nchi ambayo amekamatwa huko zitatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hivyo, sina maana katika nchi za *SADC* tuna mbabe kama Marekani. Mimi nafikiri katika nchi za *SADC* tunaishi maisha ya undugu sana na haitatokea kitendo kama kile kilichotokea Malawi kwa washukiwa kutoroshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningeomba kumalizia kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hii hoja na tumechelewa mno kuridhia huu Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika dhidi ya Ugaidi wa mwaka 1999. Mimi kabla ya yote, naunga mkono Mkataba huo mia kwa mia. (*Makofî*)

Nawashukuru pamoja na kuwasifu Waziri wa Mambo ya Ndani, pamoja na Naibu wake, kwa kufanya kazi nzuri ambayo kusema kweli sisi sote tunaishuhudia na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu, awape nguvu waendeleze kazi nzuri. (*Makofî*)

Namsifu pia Mzee Malecela, ambaye kusema kweli amewasilisha maoni ya Kamati na nayaunga mkono maoni yote aliyoyasema na kwamba, kusema kweli yamelenga pale ambapo tunakusudia suala la ugaidi kuufyeka kabisa na kuumaliza. Ahsante sana namshukuru Mwenyezekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kusahau wale waliochaguliwa kutuwakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Professa Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, wote tunawaomba wakatuwalishe vizuri na wakatoe picha ile ya Bunge hasa lililokomaa na la kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda sasa nianzie pale alipoishia Dr. Lamwai. Kwamba, tukio lililotokea Malawi la kuchukuliwa watuhumiwa watano, watuhumiwa wale wakapelekwa Zimbabwe pamoja na Sudan kuhojiwa na kuchunguzwa, kwa bahati mbaya sasa ikaonekana kwamba, hawahusiani kwa karibu au kwa mbali na kikundi chochole cha ugaidi au na ugaidi wa namna yoyote na kuachiwa ni kitendo ambacho kusema kweli kinasikitisha na kinatia mashaka. Kwa nini nasema hivyo?

Wale walikuwa ni walimu, walikuwa wanafundisha elimu ya dini pale Malawi, Elimu ya Kiislamu, wengine wamekwenda kufanya kazi kama ni wahubiri wa dini ya Kiislamu. Sasa hii inaonyesha kana kwamba, hawa wahubiri au Waislamu wanafundisha katika shule au vyuo inaonekana kwamba, wao wakati wote wanawenza wakafanya ugaidi kana kwamba yule anayekwenda kufundisha au kuhubiri uislamu wakati wowote anawenza kufanya ugaidi. Sasa hili ni tukio ambalo kusema kweli zito na baya. Kuhuishwa ugaidi na uislamu au na mwislamu anayefanya kazi ya dini. (*Makofî*)

Hili ni jambo haya kweli kweli na lazima tulikemee hasa hasa likitokea katika nchi moja ambayo hii Itifaki leo tunayoizungumzia yaani katika nchi 14 kati ya zile za *SADC*. Kusema kweli ni jambo zito na ni jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa. Hata hiyo, *Convention* yenye tunakuwa tunaizungumza iko wazi kabisa katika sehemu ya 3 (2) ibara ya 2 ikielezwa kwamba: “*state parties shall adopt any legitimate measures aimed at preventing and combating terrorist acts in accordance with the provision of the convention and their irrespective national legislation in particular. They shall do the following*”. Kuna mambo pale (a), (b) (c), nataka kusoma (d). “*Strengthen the protection and security of persons. Diplomatic and consular, commissions premises of regional and international organizations accredited to a state party, in accordance with the relevant conventions and rules of international law*”.

Sasa kwa maana hii mimi nasema kwamba, hawa watu ni lazima wahifadhiwe wale ambao wanaokwenda katika nchi nyingine isiwe kwa tuhuma ndogo tu basi tayari imeshachukuliwa kwamba wao wanataka kufanya uhalifu, mpaka kuwe na sababu ingawa Mheshimiwa Lamwai, amesema hapa kwamba, hawezi kushughulikia na sheria ndogo yoyote ya jinai kwa sababu lile ni jambo lililokuwa ni la hatari kama ilivyotokea Kenya. Ni kweli ! Lakini pamoja na hivyo tuhuma zile ziwe hasa nzito za kuweza kuona kwamba, kweli huyu anataka kufanya ugaidi na si tu kwa sababu ni kwamba yeze umewwona ana ndevu ndefu, anavaa kofia hivi, amevaa kanzu sasa huyu ni gaidi. Hili jambo halikubaliki, ni jambo halifai kabisa. Au ana sharubu hivi eeh. Sasa katika hali hii nasema na hili ni jambo ambalo linavunja moyo.

Mimi nataka niwaambie Dini ya Kiislamu inapinga ugaidi kwa aina zote za ugaidi na iko kali sana. Nataka kuwaambieni hapa mimi nimesoma Kiarabu, nataka kuwambieni aya hizo za *Qoran* pamoja na hadithi za Kiongozi wa Dini ya Kiislamu akipinga kabisa matukio yoyote ya ukatili na ugaidi na anayefanya hivyo si Mwislamu. Mimi nataka kusoma aya. Katika sura ya 3 aya karibu ya 146 inasema wazi tu “*Mankatala nafsani fakaanama katalani ndassa jamiani. Waman-ayahaya fakaanama ayanasa jamiani*”. “Mtu mwenye kuua nafsi moja (mtu mmoja) ni kana kwamba ameua watu wote duniani na mtu

anayeihoina na kumfanya hai binadamu mmoja kana kwamba amewafanya hai binadamu wote duniani au ulimwenguni". (*Makofii*)

Ni wazi kabisa hizo ni *regulations* na hadithi za Mtume, ambaye Waislamu sisi tunamfuata amesema hadithi ziko chungu nzima karibu 60, ninazisoma 3 tu. Anasema hivi: "*Al Muslim mansaliman-nasa bilisanii wayadihi*". "Muislamu ni yule aliyewasalimisha watu kwa ulimi wake na mkono wake" (Hadithi ya Mtume Muhammad - *S.A.W.*). Watu wawe salama huyo ndiyo Mwislamu, hakuna vingine. Halafu kuna nyingine "*Layuminu ahadukum hata yuhibu liakhini manyahibbu linafsihu*". Hii imesemwa katika dini nyingine. "Hawezi kuwa mmoja wenu anaamini anajitia yeye Mwislamu au muumini mpaka ampendelee ndugu, ampendelee mwenzake lile analopendelea mwenyewe" (Hii ni Hadithi ya Mtume Muhammad *S.A.W.*). (*Makofii*)

Pia hadithi ya mwisho "*La dharar wala dhirar*", "Mtu asifanyiwe dhara wala asimdhuru mwininge wala yeye asidhuriwe aishi katika salama. (Hii ni Hadithi ya Mtume Muhammad *S. A. W.*). Kwa hiyo, uislamu uko mbali kabisa na ugaidi. Sasa mimi naona ajabu kwamba, Waislamu sisi tuna balaa gani jamani, hakuna sababu yoyote ya kuhusisha uislamu na ugaidi, ni kitu ambacho hata hapa Tanzania wamekamatwa Masheikh pamoja na wahubiri kule Tanga, pamoja na Iringa na kadhalika, kwa sababu tu wanafundisha dini. Hili jamani lazima tulikemee, tulipinge kwa nguvu zote, litatuletea matatizo. (*Makofii*)

Hata mtu akionekana Muislamu kama mimi msomi hivi, wakati mmoja nilipokuwa Chuo Kikuu cha Edinburgh, alipita mtu mkubwa tu akaniuliza aah wewe Mswahili uko hapa unafanya nini? Sasa mimi nikashangaa Mswahili maana yake nini, Mswahili anayezungumza Kiswahili au nikajua Mswahili maana yake Muislamu ambaye kusema kweli yeye wakati wa sasa hata akisoma anaonekana ni mshamba tu, mtu limbukeni tu. Eeh ndio! Hapa hapa wakati fulani jamaa mmoja nje hapa aliniita Professa Maji Marefu, hii Maji Marefu amelipata wapi? Mbona kebehi hii ya *yakhe yakhe*, Muislamu hata akisoma akifika wapi ni *yakhe* tu. Ni mtu wa kawaida wala hana lolote au chocchote. Sasa hili jambo litawenza kutufarikisha, watu tuko pamoja, Taifa moja hebu tukubaliane tuwe na msimamo mmoja jamani. Tusidharauliane wala tusishutumiane. (*Makofii*)

Baba wa Taifa ametuasa na wasia ule lazima tuuchukue, tukitaka tuwe Taifa moja ni lazima twende pamoja na kusiwe na *second class citizens*, watu wa tabaka la pili. Lazima tuangalie hizi tofauti za dini, lazima tuzzungumzie, tukizungumza ndio ziondoke kusiwe mtu anazungumza akaidharau dini nyingine, huo ndio udini mkubwa. Watu wengine wakajiona bora kuliko wengine, wa dini fulani wakajiona bora kuliko wengine, huo ndio udini mkubwa kweli kweli kuliko vingine, lazima tuukemee. Lazima tuwe pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha mwisho ni kwamba, utaona sisi tuna bahati mbaya kidogo. Wakati ule alipokuwa Naibu Waziri Mkuu, cheo hicho kilikuwepo wakati wa Ndugu Mrema, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alikuwa wakati huo Naibu Waziri Mkuu. Alimwita kichaa Mheshimiwa Lamwai, leo alikuwa mwenzake *NCCR-Mageuzi* sasa ameshakuwa CCM. Sasa wenzenzu wa Iran walitusaidia kule Rufiji Segeni ili kuweza kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ikawa wameleta *container* la vyombo vyaya umwagiliaji pamoja na ujenzi wa nyumba nafuu. Yule bwana alisema kwamba, Waislamu wanaleta silaha kutaka kufanya Jihad, kwa hiyo, ikawa sokomoko kubwa kabisa *ma-container* yale yakaangaliwa na haikuonekana silaha hata moja, kumbe ni vyombo tu. Ikaingia balaa mradi wenyewe ule mpaka leo hata huo mradi wa umwagiliaji unakwenda ovyo ovyo tu. Hata ule ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ukasimama kabisa.

Sasa nasema jamani mtuone sisi wananchi wenzenu ikiwa katika hali hiyo ya ujenzi wa Taifa tunataka kujenga pamoja. Hiyo *TANU*, *TAA*, tumeanza wote. Sasa suala la ugaidi lisihusishwe na uislamu na mwislamu yeyote. Mkimwona gaidi huyo maana yake ni kwamba, hata uislamu hana. Hata ikiwa ni Mwislamu basi mkisikia ni gaidi uislamu hana. Kwa hiyo, asihusishwe kabisa na uislamu. Ikiwa hivyo mbona hapa kifungu cha mwisho kinachozungumza hapa kifungu namba 3 kwa kusaidia wale waliokuwa wanahujumu kwa mfano, kule Angola nani aliyekuwa anamsaidia Savimbi kwa ajili ya kuihujumu Serikali halali ya *MPLA* ya Angola pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, nani aliyejkuwa anamsaidia Mobutu Seseseko, nani aliyejanya vile? Sasa wale waliokuwa wametokea Palestina kule na ugaidi wa kujilipua mabomu sio wanataka kujiondoa isipokuwa wamevamiwa hawa wamechukuliwa ardhi yao, wamedhulumiwa ndiyo kwa maana sasa hakuna njia yoyote kwa njia ya Baraza la Usalama wameshindwa, kwa njia zozote za usalama wameshindwa. Njia ya sasa ya *violence* wameona hiyo njia pekee ya kufikia Waisrael. *USA* ingemshauri ndugu yake yule Muisrael ili aweze kuacha uhalifu ule.

Lakini kwa vile hakumshauri, ndiyo kwa maana *United States* inaandamwa kila mahali kwa sababu ni kwamba, Muisrael pale ameshindwa kumshauri. Sasa wale hakuna njia ni kujilipua wamekata tamaa katika maisha yao. Isifikie hatua hiyo, msitufikishe hapo jamani Waislamu, msitufikishe kwamba tukate tamaa na maisha, tunataka sisi tuwe raia wema, watu wa kuchangia maendeleo katika nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, inayoitwa Azimio la Kuridhia Mkataba wa Udhibiti wa Magaidi. Pia niwashukuru na kuwapongeza watoa hoja kwa hoja nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumza machache kwa sababu aliyenitangulia, Mheshimiwa Profesa Mndengerek, amezungumza mengi ambayo ningetaka niyachangie. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ugaidi ni tatizo ambalo linasambaratisha uchumi wa dunia lakini pia linatia mashaka ya maisha ya binadamu duniani. Suala la kujiuliza hasa ugaidi ni nini. Mwenyekiti alipokuwa anatoa hoja pale nilimshukuru aliposema neno ugaidi halijatafsirika vizuri.

Neno ugaidi litafsirike kwa makini, ili basi tunapotunga sheria ile sheria imlenge gaidi. Sasa hatuelewi gaidi ni yupi hasa. Kwa sababu kuna mwengine anaua tena watu wengi haitwi gaidi. Lakini kuna mwengine anatenda kitendo labda cha kuashiria kuua watu wachache huyu anaitwa gaidi. Sasa gaidi ni yupi?

Gaidi ni yule aliyeua watu wengi, aliyeua kutumia njia za kisiasa, gaidi ni jambazi, gaidi ni nani haieleweki. Sasa tunapojadili kujua yupi ni gaidi ili tuweze kujadili vizuri inakuwa ni matatizo. Sasa ili sheria iweze kubeba mkondo wake vizuri, neno gaidi basi litafutiwe tafsiri iliyokuwa imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lazima tuangalie chanzo cha ugaidi duniani hasa ni kitu gani. Nini chanzo cha ugaidi katika ulimwengu huu. Chanzo cha ugaidi katika dunia ni kwa sababu ya hitilafu ya kwamba, kuna nchi zingine zinatakiwa ziitwe mabwana, nchi zilizokuwa wababe. Ni ubabe.

Kuna nchi zinazokuwa babe zinataka zionekane sana mbele kuliko nchi zingine zozote zile. Sasa kwa maana hiyo zile nchi ambazo ni changa, ambazo zinapiga hatua za maendeleo, hizi nchi babe hazitaki zile zionekane zinaendelea. Zinatafuta kila namna ya kuzidhibiti ili zisipige hatua za maendeleo.

Sasa chanzo cha ugaidi kimeanzia hao kwamba, zile nchi zinazoendelea hazikubali na hizi zilizoendelea wanafanya mambo ya kudhalilisha zile nchi ambazo zinatakiwa ziendelee. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi kamili ni pale Marekani ilipoombwa kwamba, isiivamie Iraq kwa sababu haikuwa na misingi ya kuivamia Iraq. Wakakiuka Azimio Namba 1441 la *United Nations*, Azimio ambalo lilikuwa ni la kukagua silaha zile zilizodhaniwa kwamba, Iraq ina silaha za maangamizi.

Lakini kwa sababu Mmarekani ni mbabe akajua kwamb,a Iraq hakuna silaha akabadilisha akasema anaiomba *UN* sasa impe ruhusa aivamie Iraq kabla hata taarifa ya ukaguzi wa silaha kali haijapatikana.

Lakini pamoja na *UN* kumwomba kwamba, asiivamie Iraq mpaka taarifa ipatikane, hakukubali. Sasa huo tunasema ni ubabe na ubabe wa namna ile ndiyo chanzo cha ugaidi duniani. (*Makofi*)

Lakini tatizo linalopatikana hakuna hata nchi moja katika ulimwengu ambayo inamshutumu Muamerika kwa kitendo kile, kitendo cha mauaji ya watu wasio na hatia, wamepoteza roho, watoto wadogo wamefariki na nchi imesamaratika.

Lakini hata nchi moja, hata hiyo *UN* haisimami ikamlaani Muamerika kwa kitendo kile, ila ililaani sana kitendo cha ugaidi kilichotokea kule Marekani cha kuvunjiwa ile nyumba ya biashara, dunia nzima ililaani. Ila kitendo cha America kuipiga Iraq na kuua watu wasio na hatia hakilaaniwi hata kidogo! Sasa tukifikia hapo ugaidi unaanza, wale wanyonge wanatumia njia za unyonge ili kulipa visa kwa yule mbabe. Hicho ndio chanzo cha ugaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo dhana pia kwamba Marekani inakusudia kwa makusudi kudhoofisha nchi zile zilizoendelea, lakini hasa nchi za Kiislam. Hiyo dhana ipo. Ndio maana alikuwa anazungumza Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi hapa kwamba, popote pale walipo Waislam ambao wanaendesha Taasisi na Taasisi hizo zinasaidia maendeleo ya nchi yoyote, basi wale wakamatwe kwa utaratibu wa kuitwa magaidi. Ndio maana hapa kwetu wamekamatwa na sehemu zingine wamekamatwa Waislam. Inawezekana kweli wapo magaidi Waislam, wala hatukatai, kwani gaidi ni mtu ye yote yule. Mtu ye yote anaweza kuwa gaidi, hata sisi Watanzania tunaweza kufanya ugaidi katika nchi yetu. Sasa, ikifikia hapo ni lazima Sheria ichukue mkondo wake na katika kuchukua mkondo wake ni lazima iainishe. Unapomkamata mtu uweke uwazi unamkamatia tuhuma gani, lakini mtu anakamatwa haielezwi tuhuma ya kukamatwa hata moja. Anakamatwa tu anawekwa ndani hajulikani alipo. Sasa, utaratibu huu unatia mashaka kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za ugaidi na utaratibu wa kupidisha Maazimio ya Mikataba ya Afrika ya Kuzuia Ugaidi ni mambo mazuri sana. Ni mambo mazuri sana kwa sababu kila nchi ni lazima ichukue tahadhari ya raia wake na mali zake na Sheria ambazo zinaondoa wasiwasi kwa maisha ya binadamu. Lakini ningeomba katika utekelezaji wa Sheria hii, basi nchi yetu iwe makini sana sana, isifuate shinikizo la nchi zingine. Isifuate shinikizo la Marekani wala nchi yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatunga Sheria hapa ya kupambana na ugaidi kuna vikundi vya Kiislam vililalamikia sana hiyo Sheria, lakini kwa wakati ule sikujua kwamba kwa nini wanalamika, kwa sababu ni sheria nzuri tu ambayo inalinda raia wote. Lakini nimekuja kugundua malalamiko yao baada ya matukio yaliyotokea juzi au mwezi uliopita mpaka Waislam wakaffikia kufanya maandamano ya kukamatwa Viongozi wa Taasisi za Kiislam. Viongozi amba walikuwa ni msaada mkubwa sana kwa jamii, wamejenga mashule, wamesaidia kuleta maji, wakati wa matatizo mbalimbali wametoa misaada, wakati wa ajali nyangi tu wametokea, wamesaidia huduma za afya na kadhalika. Sasa watu hao wamekamatwa, lakini maelezo mahsusiy ya kukamatwa kwao hayajulikani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuwa ni kweli au si kweli, lakini ni vizuri basi kubainisha kwamba hawa wanatuhumiwa moja, mbili, tatu, nne na tano, ili yale mashaka ya watu kwamba wamekamatwa kwa uonevu basi yaondoke, kuliko mtu unamkamata tu bila kutoa uainisho wowote ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyo mbele yetu ni nzuri, lakini ninaiomba Serikali katika kutumia Sheria za ugaidi basi isitizame tu upande mmoja wa jamii, kwamba lazima Muislam awe gaidi. Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi ametafsiri aya nzuri tu, aya muhimu kweli katika Koran kwamba: "Mtuyeyote anayekuwa gaidi si Muslim ni kafiri." Wengi sana watatafsiri kafiri vibaya, lakini kafiri ni mtu ambaye hana dini, si muumini. Si Mkristu wala hana Uislam au hamjui Mungu, kwa sababu dini zote zimezuia kuua. Sasa inapofikia mtu akaenda kuua, basi Uislam wake ni batili. Sasa, dhana ya kwamba Waislam wanajihusisha na ugaidi, ni kweli wapo Waislam wanaofanya hivyo, lakini si wote, ni vizuri

inapotokea Sheria hiyo kuchukua mkondo, basi ni lazima uchunguzi wa kutosha ufanyike, siyo mtu anakuja tu na kusema kwamba huyu, huyu na huyu ni magaidi. Ni lazima uchunguzi wa kutosha ufanyike, wakamatwe na iainishwe, itangazwe kwamba amekamatwa anatuhumiwa kwa hili, hili na hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika dhidi ya Ugaidi wa mwaka 1999 (*The OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 1999*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ninampongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kufungua daraja la Mkapa. Pia, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuijunga na Baraza la Chuo Kikuu ambao ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ugaidi hatuwezi kuuzuia sisi peke yetu bila ya kupata msaada. Nchi kama Saudi Arabia walipenya, wakapiga mabomu kwenye Kambi za Majeshi na wakazivunja. Sisi Watanzania hatuna uwezo wa kufanya kazi hii peke yetu, ni lazima tushirikiane. Ushirikiano ni muhimu katika kudhibiti ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusibabaishwe na kauli za nchi za Magharibi kwa kutwambia kwamba kuna ugaidi Kenya, Tanzania Bara au Zanzibar na tukaanza kuogopa. Maneno yao yanatuletea athari mbaya sana katika uchumi. Kwa mfano yalitokea maneno kwamba Zanzibar kuna ugaidi, wakati hakukutokea kitendo chochote cha ugaidi. Zanzibar iliathirika sana kiuchumi, ikawa haina mapato mazuri kwa kipindi kilichopita. Napenda kutoa mfano wa *British Airways* iliyozuia safari zake kwenda Kenya. Lakini baada ya kuona wanapata hasara mbona walirudisha ndege hizo na zimeanza kazi kama kawaida?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Wizara hii kwamba, kuwe na *supervision* ya wageni wanaoingia nchini hasa vijana kuanzia wanapofika uwanja wa ndege, hotelini mpaka wanapoondoka. Wakionekana watu ambao hawajulikani mbele wala ubavuni washtakiwe. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipengele katika ukurasa wa 5 wa mkataba huu (d) kinasema kwamba: “*To strengthen the protection of diplomatic and consular mission.*” Ninashangaa sana kuona watu wamejikusanya pale *Ujamaa House*, wanaamini ule ukuta na ile *security* pale. Unaweza ukapanda *scania* kubwa ukatia *lorry* lenye mzigo wa tani kumi likapita ule ukuta na likavunja jengo lote lile. Ninashauri *consular* hizi ziwe kwenye *isolated places*, badala ya kukaa mahali pamoja wakae sehemu mbalimbali. Ikitokea kitendo kama hiki nchi yetu itaathirika kiuchumi na tutapoteza *credibility* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuzungumzia tafsiri ya ugaidi inayoelezwa katika ukurasa wa tatu: “...any act which may endanger life or cause death” Yaani kitendo chochote kinachohatarisha maisha au kinachosababisha mauti, hapa ugaidi siyo lazima kulipua au kuua kwa mabomu, risasi au vinginevyo. Hata mashoga wanaweza kuwa magaidi, kwa sababu wanaambukiza UKIMWI ambao unaleta mauti. Tuwapige vita mashoga na ndoa zao zipigwe vita. Papa John Paul II hivi karibuni amepiga vita ndoa za mashoga na sisi tupige vita tusikae kimya mpaka ushoga ukatudhuru. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi jirani za Kenya na Nigeria hawakutia saini mkataba huu wa ugaidi. Sisi Tanzania Bunge letu ni shupavu, tunafanya kazi *systematically* tumeipitisha Sheria hii na ninawapongeza na ninawashukuru Waislam wote hawakufanya matatizo yoyote, wametuamini Wabunge wao. Uislam haukuja kwa ncha ya upanga, Mwenyezi Mungu anasema: “*La iqra-fii-din.*” Halazimishwi mtu kuingia katika dini ya Uislam. Ninampongeza sana Mwalimu wangu, Mheshimiwa

Prof. Juma Mikidadi, kwa aya zake na hadithi za Mtume Muhammad *S.A.W.* zimeweka wazi kwamba *Islam* ni dini ya amani na mtu yeyote anayefanya kitendo cha uovu, si cha kuua tu hata cha kuzini, basi wakati anavyofanya kitendo kile na kwa *Islam* wake anakuwa kauweka upande. Kwa hiyo, *automatically* yule si Muislam. Uislam usihusishwe kabisa na ugaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara iunde *standby force* kama nchi za Afrika, *African Union* walivyoamua ili *force* hii kazi yake iwe ni kupambana na ugaidi tu. *There should be the monitoring of arrivals from the airport to departure*, hasa wageni vijana wanaokuja tuwaangalie sana kwa sababu mara nyingi wanaokamatwa ni vijana. *Old people are very dangerous, they don't mind even if the whole world catch fire.* Watu wazima hawajali hatari, hata dunia nzima ikiungua moto wao hawajali. Vijana ndio tuwakamate, tuwafuate. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *united we stand, divided we fall.*

MBUNGE FULANI: Sawa sawa.

MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL: Tukiungana tutakuwa wamoja, tukijigawa tutaanguka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuga ndevu siyo ugaidi. Kule Israel kuna Marabai wana ndevu nyingi. Je, wale wote ni magaidi? Aliyekuwa Kiongozi mmoja wa Chama cha Upinzani katika nchi fulani sipendi kuitaja, aliambiwa na Rais wake: "Njoo kesho saa 11.00 alfajiri utele majina, nitateua Wabunge kutoka katika Chama chako." Bwana huyo alikuwa amegombana na mkewe wakawa hawasemeshani akitaka kumwambia mkewe 'nipikie wali' anamuandikia kwenye karatasi anampa. Mkewe pia anamjibu, 'ahsante' kwenye karatasi. Siku hiyo alivyaoambwa apeleke majina, akamuandikia mkewe kwenye karatasi: "Uniamshe kesho saa kumi alfajiri." Ilipofika muda huo mkewe akamuandikia. Bahati mbaya yule bwana akaamka saa moja asubuhi, akakuta ameshachelewa na Wanachama wake watamlamu. Akamwuliza mkewe: "Mbona hukuniamsha?" Mkewe akamwambia: "Karatasi hiyo hapo." Yule bwana alipoisoma akakuta imeandikwa: "Amka, amka, amka, saa hizi saa kumi alfajiri." Yule bwana akamwambia yule mkewe: "Wewe mke wangu gaidi." (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa wale wenzetu amba wamechaguliwa kwa kura nyingi kutuwakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akiwemo Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Tunamtania kama ni Dr. Chacha Marwa Mwita. Pia, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, tunawatakia kila la kheri katika kutuwakilisha katika Chombo hicho kikubwa kabisa cha elimu ya juu hapa nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kwa njia ya pekee kuwashukuru wale wote amba wamechangia mawazo yao nikianzia na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, Mheshimiwa John Samuel Malecela, tunanufaika sana na ushauri wake katika vikao mbalimbali. Tunaomba aendelee kuwa nasi na aendelee kutushauri katika kuboresha ulinzi na usalama katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nimtambue Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, maelezo yake tumeyapokea na kubwa zaidi lililotia faraja ni kuona kwamba katika hili linalohusu ulinzi na usalama wa watu wetu na mali zao tupo pamoja. Tumekuwa juu ya itikadi, tulikuwa na wasiwasi pengine labda Upinzani wataona kwamba hili si la kwao, ni la watu wengine. Lakini tunashukuru sana kwamba katika hili tupo pamoja na nadhani hii ni afya njema ya mashirikiano ya sisi Wabunge na Vyama mbalimbali vyta Siasa katika ulinzi na usalama wa nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niwatambue wengine wlaiochangia nao ni Mheshimiwa Dr. Masumbuko R. M. Lamwai, Mheshimiwa Prof. Juma M. Mikidadi, Mheshimiwa Alhaji Ahmadi H. Mpeme na Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail. Ninawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja mbalimbali, nikianzia na Kamati ya Ulinzi na Usalama, wametoa mapendekezo ambayo kwa kweli yote tunayakubali na tunayachukua. Kuhusu suala kwamba tujitahidi kuwa na tafsiri moja na mwelekeo mmoja wa namna ya kutafsiri ugaidi katika Bara la Afrika na pia kupanua demokrasia na Utawala Bora tunakubaliana nao na vile vile, kuhusu suala kwamba tuisitangulize wala kuingiza itikadi katika mapambano dhidi ya ugaidi. Haya yote tunayapokea na tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib kwa niaba ya Kambi ya Upinzani alikuwa na mambo ya kutwambia ambayo tumeyachukua. Anauliza ugaidi ni nini hasa? Vile vile, anaungana na Mheshimiwa Malecela kwamba tujitahidi tuwe na tafsiri moja ya ugaidi. Suala hili limezungumzwa na watu wengi kuhusu tafsiri ya ugaidi, ikiwa ni pamoja na Prof. Mikidadi na Mheshimiwa Alhaji Ahmadi Mpeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ile Sheria tulioipitisha hapa kuhusu ugaidi sisi tumejaribu kuondoa mambo ya dini, itikadi na kadhalika katika tafsiri yetu ya ugaidi. Ugaidi tunaona kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Lamwai ni aina fulani/maalum ya jinai. Vitendo vinavyoashiria ugaidi ni ni hivi hivi vya kawaida, vya kuua, kuchoma, kuharibu uchumi na kadhalika, lakini tunatazama nia ilikuwa nini. Ndio maana kesi za ugaidi tunazichunguza sana mpaka tujue kwamba nia ilikuwa nini. Vile vile, tunaangalia kwa sababu ugaidi unakwenda na mtandao, majambazi wawili/watatu wanaweza wakashirikiana wakapiga, wakaua watu, wakaiba mahali fulani na kadhalika, lakini kwenye ugaidi liko suala la mtandao, kwani ugaidi haufanywi na mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo, viko viashiria vingi ambavyo tutavichunguza katika kuhukumu kesi za ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib amezungumzia habari za ubabe wa Marekani na ana wasiwasi kwamba pengine ubabe huo utatuburuza, utaburuza kila mtu. Tanzania tutajitahidi kabisa tusiburuzwe na mtu yeyote. Ndio maana katika vile vita vya Iraq sisi ni mionganoni mwa nchi ambazo hatukuwaunga mkono na wenyeewe wanajua. Katika Mkataba wa Kimataifa unaosema: “Askari wakifanya makosa wapelekwe katika *Court* ya Kimataifa.” Marekani walisema wengine wote wapelekwe huko, lakini Askari wao wakifanya makosa katika nchi nyingine za kigeni wasipelekwe kwenye court hizo na wengine wote ni lazima wakubali. Sisi tumekataa na nyie mnajua kabisa na juzi juzi ametunyima misaada fulani fulani kwa sababu tuliwakatalia hilo, acha watunyime. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib kwamba, haya yote tunayafanya katika kukataa ile kuburuzwa, kwamba mtu mmoja mbabe anaweza akaburuza kila mtu. (*Makofsi*)

Pia, ametahadharisha kwamba Upinzani katika nchi za Kiafrika unaweza ukapewa chapa ya ugaidi. Hilo tumeliweka vizuri sana katika Sheria zetu, kwamba upinzani si ugaidi. Upinzani ukifuata Sheria za nchi katika kufanya shughuli zake hautakuwa ugaidi hata siku moja. Hata hili suala la maandamano, tunaandamana kwa kufuata Sheria na taratibu. Sasa tukiandamana bila Sheria, bila utaratibu, nchi hii itajaa maandamano tu, hatutafanya kazi. Kila mtu atakuwa na maandamano yake, kila mahali maandamano. Kwa hiyo, kwa Vyama vya Upinzani, kama kilivyo Chama Tawala ziko taratibu na Sheria za kufanya maandamano na mpaka sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inapata ushirikiano mkubwa sana kutoka Vyama mbalimbali pamoja na Vyama vya Upinzani. Kama wana maandamano yao wanakuja kutoa taarifa, tunakubaliana *routes* na wanakwenda kwenye maandamano yao. Hata siku moja hatujasema kwamba maandamano ni sehemu ya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Lamwai ye ye ameasa habari ya nchi kutumiwa na magaidi, habari ya nchi fulani kwenda kuchukua magaidi katika nchi hiyo na kuwapeleka kwingine bila kufuata Sheria kama ilivyotokea Malawi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Lamwai na Bunge lako Tukufu kwamba, hilo kwa hapa Tanzania haliwezekani. Kama kuna mtu kafanya kosa atahukumiwa kwa Sheria zetu za hapa hapa na kama si raia wetu ni lazima ahamishwe kwenda mahali pengine ziko Sheria na taratibu zinazofuatwa katika kuhamisha wahalifu. Haiwezekani kwamba wakachukuliwa kiubabe ubabe kama ilivyotokea kule Malawi, Sheria zetu hazisemi hivyo.

Mheshimiwa Prof. Mikidadi pamoja na Mheshimiwa Alhaji Mpeme wamezungumza kwa kirefu sana kuhusu wasiwasi kwamba ugaidi na Uislam vinawekwa katika tafsiri moja. Kusema kweli nia ya Mkataba huu ambao tunauridhia na hata Sheria tulio pitisha hapa haisemi kabisa kwamba Uislam uwe ni sehemu ya Ugaidi, hata kidogo. Mtu hawezu kuhesabiwa kama ni gaidi kwa dini yake au kwa rangi yake, au kwa kabilo lake. Atahesabiwa kuwa ni gaidi kwa vitendo na ni vitendo ambavyo vitakuwa vimechunguzwa kwa makini. Napenda mtuamini kwa hilo. Yamekuwepo maneno Waislam tayari wameishaanza kuchukuliwa Tanga na Iringa kwamba ni magaidi kwa sababu ya Uislam wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda watuamini sisi Serikalini kuliko kuamini magazeti. Magazeti yanasesma: "Ooh kuna mtu amevuliwa uraia huko Iringa kwa sababu anashukiwa kuwa ni gaidi." Hayo ni maneno ya magazeti, anayevua mtu uraia ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi hajamvua mtu yeyote uraia kule Iringa kwa sababu yoyote ile ya Uislam au ya ugaidi, lakini magazeti yakiandika watu wanaamini, hakuna. Pia, kuhusu Tanga kwamba mtu kachukuliwa kwa sababu ni gaidi. Kama yule mtu wa Tanga angekuwa ni gaidi angekamatwa na Polisi na angekuwa yuko mahakamani, ndizo Sheria zinavyosema. Tunayo Sheria ya ugaidi, huyu mtu wa Tanga angekuwa ni gaidi angekamtwa na Polisi na sasa hivi angekuwa yuko mahakamani akishtakiwa kwa kosa la ugaidi kwa mujibu wa Sheria zetu. Lakini ile kesi ya Tanga yule bwana alikuwa na makosa ya kiuhamiasi, lakini hili nalo watu hawataki kuelewa na ndio maana suala lile lilishughulikiwa na Uhamiasi. Uhamiasi hawashughuliki na ugaidi. Kesi za ugaidi zinashughulikiwa na Polisi, ile ya Tanga haikuwa *Police case*, ilikuwa ni kesi ya Uhamiasi na ndio maana ikashughulikiwa na watu wa Uhamiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ya watu kufukuzwa nchini, kupata *PI* kila siku yapo tu, Wakristo, Waislam na wasio na dini ukikosea Sheria za Uhamiasi unapewa *PI*. Lakini sasa hii ya Tanga imebebwa, inashabikiwa kiasi cha ajabu sana! Kwa hiyo, nataka muamini kwamba, ile kesi ya Tanga ingekuwa ni ya ugaidi, ingekuwa ni *Police case* na ingekuwa iko mahakamani mtu yule akishtakiwa kwa ugaidi. Lakini suala zima tangu mwanzo mpaka mwisho limeshughulikiwa na *Immigration* akapata *PI* yake na akaondoka kama wanavyoondoka wengine wote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Prof. Mikidadi na Mheshimiwa Alhaji Mpeme muelewe kwamba hakuna mtu ambaye anamsakama mtu mwininge kwa sababu ya dini yake. Kwa hapa Tanzania halipo na mkiona hizo dalili zipo tuje tuzungumze. Waheshimiwa Wabunge mkiona dalili hizo mahali leteni tuzungumze kwa sababu Sheria yetu na maadili ya nchi yetu hayatuelekezi hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail amesema hatuwezi kuzuia ugaidi peke yetu ni lazima tusaidiane, hilo ni kweli. Pia, amesema sasa tufanye *monitoring*, tuwe waangalifu katika mipaka yetu kuona nani anaingia na kwa sababu gani, ni kweli. Sasa hivi katika Wizara yetu tunajaribu kuweka katika vituo vyetu vya mipakani kumbukumbu za watu wanaoingia kwenye *computer*. Tunataka ku-*computerize border posts* zetu zote. Mtu akiingia pale Namanga wakishaingiza *data's* zake kwenye *computer* vituo vyote nchi nzima vinajua fulani kaingia na taarifa zake. Pia, siku ya kutoka, popote atakapotokea iwe ni Tunduma, *Zanzibar airport*, Pemba au Mtukula, wakisham-click kwenye *computer* itajulikana kwa vituo vyote nchi nzima kwamba fulani katoka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la kufutilia nyendo za wageni wanaoingia ndio litakalotusaidia kuepukana na ugaidi wa Kimataifa. Hili ni zoezi ambalo lina gherama kubwa sana na ndio maana Mikataba kama hii sasa inatuweka katika hali nzuri tuweze kusaidiwa kubeba gherama kama hizi kwa sababu ku-*computerize* nchi yetu ni kubwa sana na ina vituo vingi sana. Mikataba kama hii inatusaidia kupata marafiki na wahisani wa kutusaidia kuzibeba. Baada ya kusema maneno haya, nataka tu niwashukuru wale wote waliochangia, tumepokea hoja zote na tunazifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika dhidi
ya Ugaidi liliridhiwa na Bunge*)

**AZIMIO LA KURIDHIA ITIFAKI YA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA
KUHUSU MAKUBALIANO MAPYA YA MATUMIZI YA MAJI YA KIMATAIFA YA MWAKA
2000**

**(THE REVISED PROTOCOL ON SHARED WATER
COURSES IN THE SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT COUNTRIES (SADC) REGION, 2000)**

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge liridhie Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika Kuhusu Makubaliano Mapya ya Matumizi ya Maji ya Kimataifa ya Mwaka 2000 (*The Revised Protocol on Shared Water Courses in the Southern Africa Development Countries (SADC) Region, 2000*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha Azimio hili, nami napenda kuungana na wenzangu kuwapongeza Wabunge wenzetu waliochaguliwa kuingia kwenye Baraza la Chuo Kikuu. Nampongeza sana Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, mimi naona leo tumeonyesha mambo yao mazuri, pengine hata 2005 yatakuwa mazuri hivi hivi. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuishukuru Kamati ya Ardhi na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa Mbunge wa Mbozi Magharibi, kuchambua Mkataba huu na kuukubali kuwa uletwe mbele ya Bunge lako tukufu ili uweze kuridhiwa. Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) inaunda na nchi 14 ambazo ni Afrika ya kusini, Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelia, Swaziland, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.

Mkataba wa kuunda Jumuiya hiyo ulitiwa saini na Marais wa nchi hizo jijini Winduk Namibia, tarehe *17 August 1992*. Kwenye mkataba huo hususan kifungo 21 na 22 yameainishwa maeneo ya ushirikiano baina ya asasi mbalimbali katika Jumuiya hiyo. Miogoni mwa maeneo hayo ni matumizi ya maji ya kimataifa yaani *Shared Watercourses*. Ili kutimiza azma ya mkataba huo makubaliano ya matumizi ya maji ya kimataifa (*Protocol on Shared Watercourses Systems*) yalitiwa saini na Marais wa nchi hizo za *SADC* huko Johannesburg, Afrika Kusini tarehe *28 August, 1995*. Tanzania ililiridhia makubaliano hayo mwaka 1998.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi za *SADC* ipo mito 15 ambayo maji yake yanatumiwa kwa ushirikiano na nchi hizo za *SADC*. Nchi ya Msumbiji ipo chini yaani *down stream* na inatumia maji ya mito tisa kati ya mito na mito yote hiyo imeanza nchi jirani na Msumbiji. Ingawa Msumbiji ililiridhia makubaliano ya mwaka 1995 juu ya matumizi ya maji ya kimataifa, ilifanya hivyo bado ikiwa na mashaka kuhusu maslahi yake kwenye Mkataba huo.

Maeneo kama vile uhakika wa kupata maji safi na salama ya kutosha kwenye mahitaji yake usimamizi wa vijito na maeneo ya matiririsho ya maji (*Management of Tributaries and Drainage Areas*) na mengineyo ambayo ama hayakuwepo kabisa au hayakuwa bayana. Aidha makubaliano ya kimataifa mwaka 1997 yanayohusu matumizi ya maji ya kimataifa kwa shughuli zilizokuwa za usafirishaji yalichangia sana hoja ya makubaliano hayo kuboreshwa kama ilivyooombwa na Msumbiji na Angola kwenye Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Maji wa nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapungufu yaliyokuwepo katika makubaliano ya awali. Makubaliano ya awali juu ya matumizi ya maji ya kimataifa yameonyesha kuwa na mapungufu mbalimbali ambayo sasa yameboreshwa katika makubaliano mapya. Mapungufu hayo baadhi yake yameainishwa pia katika kiambatanisho Namba 3 nayo ni haya yafuatayo:-

Kwanza, makubaliano ya awali hayakutaja madhumni hasa ya makubaliano yenyewe, kwenye wenyewe makubaliano mapya madhumni hayo yamo katika kifungu Namba 2 (*Article 2*).

Pili, katika makubaliano ya awali baadhi ya tafsiri zilizotumika zinaonekana kutokidhi haja ya madhumni ya makubaliano. Ili kufanikisha utekelezaji wa makubaliano hayo, baadhi ya tafsiri kama vile *Drainage Basin* zimerekebishwa na badala yake kuwa Watercourse na tafsiri nyingine zimeongezwa.

Tatu, pamoja na kwamba makubaliano ya awali na makubaliano mapya yaani kanuni za Jumuiya (*General Principle*) ambazo hazitofautiani sana, *Article Three* ya makubaliana ya awali haina vipengele maalumu vinavyotoa ufanuzi zaidi na kwa uwazi wa kanuni za jumla zilizolezwa kwenye *article* ya tatu. Makubaliano mapya yameongeza vipengele maalum kadhaa kwenye *Article Four* kwa ajili ya ufanuzi huo. Mambo muhimu yaliyoongezwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

- (a) Mipango ya kurekebisha athari mbalimbali;
- (b) Hifadhi ya mazingira;
- (c) Usimamizi wa vyanzo vya maji;
- (d) Uzuijiji na urekebishiwa wa sehemu zilizoathirika;
- (e) Namna ya kushughulikia dharura.

Nne, kifungu namba 3 cha makubaliano ya awali hatukutaja vyombo mbalimbali vinavyohusika na utekelezaji wa makubaliano hayo watusika na majukumu yao. *Article* namba tano ya makubaliano mapya imeonyesha vyombo vinavyohusika kwa kila ngazi, watusika na majukumu yao.

Tano, aidha kwenye makubaliano ya awali hapakuwepo na kifungu ambacho kilitambua na kuruhusu kuwepo kwa mikataba mingine kati ya nchi wanachama wa *SADC* au kati ya nchi moja au zaidi za *SADC* na nchi ambayo siyo mwanachama wa *SADC* kuhusu matumizi ya maji ya kimataifa kwa lengo la kutekeleza makubaliano hayo. Katika makubaliano hayo. Katika makubaliano mapya imeongezwa *article* 6 ili kuhusisha mikataba hiyo na makubaliano hayo mapya.

Mheshimwia Naibu Spika, matokeo ya utekelezaji wa makubaliano mapya. Manufaa yatakayopatikana kwa nchi yetu kutokana na utekelezaji wa makubaliano mapya ya matumizi ya maji ya kimataifa ni kuimarika kwa ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi wanachama wa *SADC* na kuweka matumizi na endelevu ya maji ya kimataifa katika nchi hizo kwa ajili ya maendeleo yake. Manufaa mengine ni kama ifuatavyo:-

Kwanza kurahisisha uanzishwaji wa ushirikiano kwa nchi zinazohusika hasa uanzishwaji na utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya wanachama inayohusiana na mali za maji.

Pili, kuwezesha nchi wanachama kubadilishana taarifa na takwimu mbalimbali zinazohusiana na raslimali za maji.

Tatu, nchi wanachama zitaweza kutumia vyanzo vilivyomo kwenye nchi zao kwa kufuata makubaliano hayo. Tanzania itanufaika na vyanzo kama vile Mto Ruvuma, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, pamoja na mito yake.

Nne, makubaliano haya yatapunguza uchafuzi wa vyanzo vya maji kutoka nchi moja hadi nyingine kwa vile mkataba unamatka kuwa kila anayetumia maji ayarudishe kama aliviyoyachukua ili kudhibiti ubora wa maji. Tano, maji yatakuwa ni kwa ajili ya matumizi ya amani (*Peaceful Use*) tu na si vinginevyo. Madhara yanayoweza kutokea endapo makubaliano hayo mapya hayataridhiwa na Serikali ni kwa Tanzania kutoweza kutekeleza miradi ya pamoja ya nchi wanachama wa *SADC* inayohusu matumizi ya raslimali za maji na uboreshaji wa hifadhi ya mazingira kwa lengo la kupunguza umaskini. Madhara mengine ni pamoja na kukosa baadhi ya manufaa niliyoyaeleza hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ambazo tayari zimeridhia makubaliano mapya hadi kufikia mwezi Agosti, 2002 (mwaka jana) ni (n ane) 8 kati ya nchi 14 za *SADC*. Nchi hizo ni Afrika ya Kusini, Botswana, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zambia na Zimbabwe. Tanzania ikiridhia itakamilisha

theluthi mbili ya nchi wanachama kiwango ambacho kitaruhusu mkataba huu kuwa na nguvu ya kisheria. Baada ya kusema hayo naomba sasa kuwasilisha azimio la Bunge kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge kuhusu Tanzania kuridhia itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu mapya ya matumizi ya maji ya Kimataifa ya mwaka 2000 (*Revised Protocol on Shared Watercourses in the Southern African Development Community 2000*)

KWA KUWA Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika, *SADC* na zinatumia maji ambayo vyanzo vyake ni mabonde ya mito mikubwa kama vile Ruvuma, Zambezi, Limpompo, Sabi, Nkomati, *Orange, Cunene* na *Okovango* na vile vile yapo maziwa ya kimataifa kama Nyasa, Tanganyika na mabwawa yaliyojengwa kama vile Kariba, *Cabora Basa* na Inga ambavyo kwa pamoja ni vyanzo vikubwa vya maji katika nchi hizo;

NA KWA KUWA maji yaliyopo katika nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo za Kusini mwa Afrika yanatumiwa kwa ushirikiano wa nchi hizo kwa kunywa, kuzalisha umeme, kilimo, usafirishaji, uvuvi na kadhalika;

NA KWA KUWA Tanzania inatambua kwamba maji hayo yanapita kwenye mamlaka tofauti za nchi hizo na kwa sababu hiyo upo umuhimu mkubwa wa kuweka utaratibu kuhusu matumizi ya maji hayo kwa kufanya makubaliano kupitia itifaki ya matumizi ya maji ya kimataifa (*Protocol on Shared Watercourses Systems 1995*) ambayo kwa kupitia Bunge hili, Tanzania iliridhia mwaka 1998;

NA KWA KUWA utekelezaji wa makubaliano yaliyomo kwenye itifaki ya matumizi ya maji ya kimataifa ya mwaka 1995 umebaini mapungufu kadhaa ambayo yamesababisha baadhi ya nchi wanachama kuomba kufanyika kwa marekebisho kwenye makubaliano ya awali kwa kuzingatia mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu matumizi ya maji ya kimataifa kwa shughuli zilizokuwa za usafirishaji ya mwaka 1997;

NA KWA KUWA Tanzania inatambua ukweli kwamba uchafunzi wa vyanzo vya maji ya kimataifa haujali mipaka ya nchi na kwa dhati hiyo, usimamizi madhubuti wa vyanzo hivi unaweza kufanikiwa tu endapo nchi zinazohusika zitashirikiana kikamilifu katika uendelezaji endelevu wa vyanzo hivyo;

NA KWA KUWA Tanzania itanufaika kwa kuimarisha ushirikiano wa nchi *SADC* katika uanzishwaji na utekezaji wa pamoja wa miradi inayohusiana na rasilimali za maji na hifadhi ya mazingira ili kupunguza uchafuzi wa vyanzo maji katika nchi hizo;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii kwa taifa letu kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 12 sasa linaazimia Tanzania kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu makubaliano mapya ya matumizi ya maji ya kimataifa ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunisikiliza na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja ilitolewa iamu liwe*)

MHE. MUSA A. LUPATU (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI): Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha maoni ya kamati naomba kwanza nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, pamoja na Serikali yake kwa kuwezesha Daraja la Mto Rufiji kukamilishwa juzi na hatimaye kufunguliwa. Kufunguliwa kwa daraja hili nina imani kwamba kutaibua fursa za kiuchumi na kijamii katika Mikoa ya Kusini. (*Makofî*)

Pili naomba, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge watatu amba o asubuhi hii wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakiwa ni Mheshimiwa Profesa David H. Mwakyusa, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Wote hawa nawapongeza kwa kuchaguliwa kwao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi juu ya azimio kuhusu Tanzania kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika, kuhusu makubaliano mapya ya matumizi ya maji ya kimataifa ya mwaka 2000 (*Revised Protocol on Shared Watercourses in the Southern African Development Community 2000*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa mujibu wa Kanuni ya 43 (5) (b) naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya azimio tajwa hapo juu.

Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge kwa jinsi alivyowasilisha kwenye kamati maelezo ya kina yenye ufanuzi juu ya maudhui ya azimio hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyooleza Waziri, chimbuko la azimio hili ni mikataba mbalimbali ya kimataifa ya ushirikiano ambayo nchi yetu imeridhia. Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika wa mwaka 1992, ulianisha maeneo mengi ya ushirikiano baina ya asasi mbalimbali katika Jumuiya hiyo ikiwemo matumizi ya maji ya kimataifa. Mkataba halisi wa makubaliano ya matumizi ya maji ya kimataifa (*Protocol on Shared Watercourses Systems*) ultiwa saini na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika tarehe 28 Agosti mwaka 1995 na kuridhia na Bunge lako tukufu mwaka 1998.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati pia iliona kwamba upo mkataba mwingine wa kimataifa wa mwaka 1997 unaohusu matumizi ya maji ya Kimataifa kwa shughuli zisizokuwa za usafirishaji (*UN Convention on non Navigation uses of International Watercourses*) Mkataba huo wa Kimataifa unaona vizuri na mabadiliko haya mapya ya makubaliano ya Itifaki hii ya matumizi ya maji katika nchi za SADC.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano haya mapya hayakubadilisha makubaliano ya awali ya matumizi ya maji ya kimataifa bali yanaboresha tu baadhi ya vipengele ambavyo havikuwepo awali kama vile madhumni na baadhi ya tafsiri zilizotumika kama alivyooleza Mheshimiwa Waziri. Makubaliano haya mapya yalitiwa saini na Wakuu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika tarehe 7 mwezi 8 mwaka 2000. Mabadiliko haya mapya yanatoa ufanuzi zaidi na kuongeza uelewa wa pamoja katika Itifaki hii ya matumizi ya maji ya Kimataifa kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo za Nchi za Kusini mwa Afrika ili kurahisisha utekelezaji wa Itifaki yenewe.

KWA KUWA kimsingi itifaki hii ilikwisha kuwepo na kwamba mabadiliko haya mapya yataondo utata katika utaratibu mzima wa matumizi ya kimataifa hususan maji yanayotumiwa na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambayo vyanzo vyake ni mabonde na mito mikubwa kama vile mto Ruvuma, Zambezi, Limpopo, Sabi, Nkomati, Orange, Cunene na Okavango pamoja na maziwa ya kimataifa kama vile Nyasa, Tanganyika na mabwawa yaliyojengwa kama vile Kariba, Cabora Basa na Inga ni dhahiri kuwa Tanzania ambayo ni mwanachama wa SADC itanufaika na maboresho ya mabadiliko hayo.

KWA KUWA Tanzania kama Mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, itafaidika na mabadiliko haya mapya ambayo wakuu wa nchi wa SADC 13 kati ya nchi 14 wanachama walikwishaweka saini tarehe 7/8/2000 Kamati inaliomba Bunge lako tukufu, likubali kujadili na kuridhia makubaliano haya mapya kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kutamka kuwa kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Kilimo naunga mkono hoja hiyo ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MHE. THOMAS NGAWAIYA - MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Tanzania kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu makubaliano mapya ya matumizi ya maji ya Kimataifa ya Mwaka 2000 (*Revised Protocol on Shared Watercourses in the Southern Africa Development Community*) kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge kifungu cha 43 (5) (c) toleo la 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kambi ya Upinzani inapongeza wenzetu ambao wanakwenda kutuwakilisha Chuo Kikuu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Tunawaombea watuwakilishe ipasavyo na kulingana na heshima la Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo zuri sana kuwa na makubaliano ya matumizi ya maji kwani vyanzo vya maji ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi, taifa na ulimwengu wa kimataifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni raslimali ambayo inaweza kusababisha mfarakano mkubwa katika jamii, kama haikutunzwa na kuheshimiwa ipasavyo. Hatuna taifa au jamii inayoweza kujienda na kuishi bila raslimali hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ya miradi mingine ya aina hii ilikwisha anzishwa sehemu zingine duniani. Ninaomba kugusia mifano michache.

Mikataba wa mwaka 1999 Bonde la Mto Plata uliuhusisha nchi tano kutoka America ya Kusini ambao ni Argentina, Bolivia, Brazil, Paraguay na Uluguay. Utekelezaji wake ulishindikana kutokana kutokuaminiana kati ya nchi husika. Hali hii ilitokana na kutowashirikisha wadau wa ndani ya nchi, mwanachama katika kubuni, kuutambua na kuuratibu mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba mwininge ni ule wa *Niger Basin Authority* wa mwaka 1980 ulioshirikisha nchi tisa, kilichotokea ni waratibu kuandika ripoti na jinsi ya utekelezaji tu. Watoaji maamuzi walishindwa kukubaliana kuhusu uehangiaji sawa wa fedha za uendeshaji kati ya nchi mwanachama, ambapo nchi moja yenye wanufaikaji wa mradi 100,000 iliona si haki kuchangia sawa na nchi yenye wanufaikaji zaidi ya milioni 20. Matokeo yake ni uchumi wa nchi wanachama katika mwaka 1994 ulianguka na nchi wanachama waliacha kuchangia ambako kulisambabisha wananchi kukosa imani na uongozi wa nchi zao. Huu ulikuwa ni usumbufu mkubwa kwa nchi wanachama.

Mkataba wa matumizi wa maji kama ule wa Ziwa Victoria masharti yake yalikuwa hayawatendei haki nchi za Uganda, Tanzania na Kenya kwani ilikuwa ili watumie maji hayo ilikuwa lazima nchi hizo ziombi ruhusu *Egypt* kutumia maji na *Egypt* ilikuwa na uhuru wa kukubali au kukataa.

Tanzania ilipotaka kujenga mfereji wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Dodoma, *Egypt*, ilikataa kwamba itapata hasara japo sasa wamekaa nakukubali mawazo na kuruhusu maji ya ziwa Victoria yatumiwe kwa shughuli mbalimbali nchi Tanzania.

Je, katika mkataba huu kuna tahadhari gani imewekwa kuzuia matatizo kama haya ya mkataba wa matumizi ya maji yasitokee tena kama ya Ziwa Victoria? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu wa maji umeundwa kwa Sheria za Kimataifa. Hivyo haukutilia maanani kuwa nchi kama nchi ina sheria zake na nchi hizo zinatakiwa kuheshimiwa na kutambuliwa. Aidha nchi husika zina sheria zake kuhusu uendelezaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji na utunzaji wa mazingira. Tunauliza je, mkataba ulizingatia haya kwa maana ya kushirikisha wadau? Mkataba pia hauainishi mashirika yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi nafasi zao ni zippi katika kuendeleza mradi kwa ujumla?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba hauwapi au kuonyesha kuwafikiria mawakala wazawa wa maeneo husika katika upangaji wa mwanzo na uendelezaji wa mradi wenywewe. Kwa maana hiyo, mkataba unawanyima haki wananchi waishio maeneo ya pembezoni mwa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yanaweza kutokea iwapo kutakosekana au kutoelewa kwa nchi wanachama, thamani halisi ya maji kwenye udhamini wa kifedha. Kwa hiyo, basi baadhi ya nchi wanachama zinazolewa thamani hiyo ya maji zinaweza kunufaika zaidi kwa mradi huu. Matumizi ya maji yanaweza kutofautiana kwa kiwango kikubwa kati ya nchi na nchi. Mkataba hauonyeshi kuwa pindi utekelezaji wa mradi utakapoanza fedha ya kugharamia uendeshaji itatoka wapi na zinapatikana vipi kama nchi wanachama zinatakiwa zichangie. Je, zichangie katika uwiano upi? Kwani hakika kuna nchi ambazo zitafaidika na mradi huo zaidi kuliko nytingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba pia hauonyeshi au haukutilia maanani utofauti wa nchi katika uchumi na ukubwa wake na sehemu gani ya wakazi wa nchi husika watafaidika na mradi huu. Aidha uhamishaji wa maji toka nchi moja kwenda nchi nydingine kunaweza kusababisha madhara makubwa ya kimazingira kwa nchi zilizo mwisho wa mtiririko wa maji yaingiyo baharini. Mfano Lake Nyasa, Malawi hufungulia maji ghafla kuingia kwenye ziwa na ziwa lina-over flow na kuathiri jamii iliyo kando kando ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya tuliyoyaanisha ni muhimu sana kuzingatiwa kwa ajili ya tahadhari ya athari zinazoweza kujitekeza. Ni muhimu maslahi ya Watanzania yakazingatiwa na kuangaliwa kwa kina katika masuala kama haya ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haina sababu ya kupinga kuridhiwa kwa Mkataba huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji watatu wa azimio hili. Halafu kwa kadri muda ulivyo hatuwezi kumaliza. Nitampa nafasi mchangiaji mmoja wawili watamalizia kesho na Mheshimiwa Waziri pia ata-*wind up* kesho. Kwa sababu kesho ndiyo mwisho wa shughuli zetu, ile hoja ya fedha nayo itakuja kesho. Hapa tayari nina wachangiaji watano.

Nadhani kwa wachangiaji watano kwa kesho inatosha, hoja yenye na wasemaji wakuu na wachangiaji watano atamalizia amalizie Waziri nadhani kwa asubuhi inatosha. Kwa hiyo, nadhani tufunge orodha ya wachangiaji wa fedha kwa hao watano. (*Makofi*)

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Lakini awali ya yote ningependa kushukuru Bunge zima kwa zoezi la leo asubuhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mmoja wa Wabunge watatu tuliohatika kuchaguliwa kwenda kuliwakilisha Bunge katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika Baraza lake. Naomba niahidi mbele yako na mbele ya Bunge zima kwamba nitatumia usoefu wangu na uwezo na vipaji alivyonijalia Mwenyezi Mungu kuweza kuinua heshima ya Bunge katika Baraza hilo kwa manufaa ya Watanzania wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa kwa kuleta hoja hii iliyo mbele yetu. Maji kama tunavyojuu imepata kauli mbiu nydingi maji ni uhai, maji ni maendeleo. Katika submission yake Mheshimiwa Waziri amelizungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyojuu kwamba chanzo kikubwa cha maji ya asili (*Natural Water Sources*) ni mito na maziwa. Kwa bahati mbaya mito na maziwa haviheshimu mipaka ya jiografia katika nchi na nje ya nchi. Tukichukua mifano iliyo hai hapa nchini ni pamoja na Mto Rufiji ambao juzi tumezindua daraja unatoka mbali sana. Unatoka Milima ya Usangu, mingine inatoka Iringa na inapita katika mikoa mingi.

Sasa kwa shughuli nydingi zinazofanyika katika mito ni lazima ina-provoke interest ya wadau wengi. Uktajiki wa miti usipodhibitiwa, umwagiliaji, viwanda vinavyozuka, usafirishaji katika maji, matumizi ya nyumbani, umeme na uchafuzi vyote hivi vinamfanya kila mmoja atake kujua nini kinatokea kwa sababu kinaweza kikaathiri shughuli zake huko maji yanakokwenda.

Kwa hali hiyo ningependa nishukuru Serikali kwamba katika kuliona hilo imeanzisha mabonde ya maji. Sambamba na baadhi bonde maji nililolitaja la Rufiji kuna mabonde mengi, mojawapo likiwa ni Bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mchango wangu ningependa nijielekeza kwenye maji ambayo yanatumika na nchi zaidi ya moja, (*Trans Boundary Water Usage*).

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inatuonesha kwamba maji ambayo yanachangiwa na Mataifa yamekuwa chanzo cha *conflicts* na hata vita hasa kule Ulaya katika karne zilizopita. Hapa kwetu tuna Mto Songwe. Mto Songwe unahama kila mwaka na imebidi tuunde Tume inayoangalia suala hilo kwa sababu tusipoangalia tunawenza tukakosana na wenzetu wa Malawi. Ziwa Nyasa ambalo limezungumzwa sasa hivi linamwaga maji yake katika Mto Shire, lakini asilimia zaidi ya 70 ya maji ya Ziwa Nyasa yanatoka Tanzania. Ziwa Nyasa linachangiwa na Tanzania, Malawi na Msumbiji. Sasa nimesema, linaweza likawa chanzo cha mgogoro.

Kwa mfano, unajiuliza haya maji ya Ziwa Nyasa ni mali ya nani? Tulipokuwa tunajifunza Jiografia, tulikuwa tunaliita Ziwa Nyasa. Wenzetu wa Malawi sasa hivi wanaliita Ziwa Malawi na wao wana-*claim* kwamba Ziwa lote ni la kwao na cha kushangaza ni kwamba hata ramani zinazochorwa siku hizi zinauzwa Mitaani ambazo zinatengeneza hapa hapa Tanzania utakuta mpaka unapita kwenye ufukwe wa Tanzania, ikiwa na maana kwamba sisi Tanzania hatuna lita hata moja ya maji ya lile Ziwa. Sasa hii ni moja ya mambo ambayo Itifaki hii italiangalia na matarajio yetu ni kwamba tutafikia muafaka kwa sababu tulivyokua tulikuwa tunaambiya kwamba mpaka ulikuwa katikati ya lile Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mwanzoni mwa mwaka huu kulikuwa na shughuli fulani katika Mto Shire ambapo ndiyo ziwa letu linamwaga maji. Tukashtukia tu maji yanaanza kumeza Vijiji vyetu eneo la Kyela. Sasa tungkuwa na Itifaki ambayo inafanya kazi hili lisingetokea kwa sababu tungkuwa tumeshaelezwa na wenzetu kwamba wanataka kufanya nini kwa sababu haya maji yote ni yetu wote. Mmoja wa wachangiaji hapa Bungeni amezungumzia kuhusu Mto Zambezi, huu ni mfano wa Maji ambayo tunachangia. Kuna wadau nchi nane, kuanzia Angola mpaka unapomwaga maji katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu ni kwamba hii Itifaki imekuja kwa wakati muafaka ili tuweze kuondoa migogoro ambayo inaweza ikatokea. Lakini vile vile, nina imani kwamba tukiwa na miradi tukaitengeneza kwa pamoja inayohusu nchi nane kama Bonde la Mto Zambezi ambalo na sisi ni wadau, kupata Wafadhili ni rahisi zaidi kuliko tukiwa tunazungumzia nchi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na haya machache. Nimesimama kwa nia moja, kushukuru Bunge lako Tukufu kwa kunipa heshima. Lakini vile vile kuunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward N. Lowassa. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, zimebaki dakika kumi tu na muda wetu wa kuongea ni dakika 15. Sasa kama Mheshimiwa Arid Mwanache Uledi unaweza kutumia dakika kumi nikupe nafasi.

WABUNGE FULANI: Kesho.

NAIBU SPIKA: Nadhani watu wanasema kesho. Jiandae vizuri. (*Makofî/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya kufika hapo, Azimio hili litaendelea kujadiliwa kesho. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 Asubuhi.

(Saa 01.35 Usiku Bunge lilahirisha Mpaka Siku ya AlhamisiTarehe 7 Agosti, 2003 Saa Tatu Asubuhi)

